

**MTINDO UNAVYOENDELEZA MAUDHUI KATIKA NATALA**

NA

**MURUNGI, GRACE KANYUA**

**C50/66103/2011**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**IDARA YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**NOVEMBA 2013**

## **IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kikuu kingine chochote kile, kwa mahitaji ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

---

**MURUNGI GRACE KANYUA**

---

**Tarehe**

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

---

**Daktari Amiri Swaleh**

---

**Tarehe**

**(Mtahini)**

---

**Daktari Rayya Timammy**

---

**Tarehe**

**(Mtahini)**

## **TABARUKU**

Kazi hii naitabarukia mamangu mzazi Bi. Marsellah Gakii Murungi kwa kunilea na kunielimisha kwa kujitolea kwa jino na ukucha. Mama nakuenzi zaidi kwa mawaidha yako si katika masomo pekee bali katika hali zote za maisha. Umekuwa mfano mwema kwangu wa kuiga hasa hulka ya kujitolea na kung'ang'ana pasipo kukosa matumaini. Mama, nehema na rehema za Maulana zikufuate siku zote za maisha yako. Aidha kazi hii naitabarukia mwanangu kipenzi na johari yangu Shanen Kinya kwa kunivumilia kipindi hiki nilikuwa masomoni na hivyo, kukosa kutekeleza kikamilifu majukumu yangu kama mama kwako. Mawaidha yanguni kwamba uyabukue matopa na matopa ya vitabu mpaka ufikie viwango vya juu masomoni. Zaidi ya hayo uwe mcha Mungu. Nakuombea uelekezi wa Mola katika maisha yako sasa na baadaye.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa natoa shukrani za moyoni kwa Maulana Muumba kwa kunijalia siha ya kimwili na amani ya moyoni kwa muda wote nimekuwa masomoni.

Pili, shukrani za dhati ziwafikie wasimamizi wangu Dkt. Amiri Swaleh na Dkt. Rayya Timammy. Sababu ni kwamba, kazi hii haingepiga hatua yoyote wala kukamilika bila ushauri wao. Walisoma kazi hii na kuikosa bila kukawia na kuniongoza kikamilifu. Zaidi ya hayo, walianzisha midahalo ya kiakademia ambayo ilinitumbukiza katika bahari yasijuinakuibu kati ya fahari ya ninafahamu. Midahalo hii iwekatikamaandishi au kupitia mazungumzo ya ana kwa ana ilinisaidia sana katika kuimarisha kiwango cha utafiti huu. Kutoka kwangu, shukrani zisizo na kifani ziwafikie huku nikiwatakia Baraka za Mwenyezi Mungu na fadhili zake siku zote za maisha yenu.

Aidha nawashukuru wahadhiri wengine katika Chuo Kikuu cha Nairobi ambao walinifunza au kunipa mawaidha ya kiusomi kipindi hiki nimekuwa masomoni. Nao ni, Mwenyekiti wa idara ya Kiswahili Prof. John Habwe, Dkt. Iribe Mwangi, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Kineene Wa Mutiso, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Evans Mbutia na Bw. Basilio Mungania. Aidha namshukuru Dkt. Mwenda Mukuthuria wa Chuo Kikuu cha Chuka kwa mawaidha na uelekezi wake wa kiakademia.

Shukrani zingine ziwaendee wanafunzi wenzangu tulioshirikiana katika masomo ya shahada ya uzamili. Lily Koech, Ibrahim Keter, Ann Suakei, Mary Nguti, Ruth Katutu, Lydia Moraa, Makange Ledemi, Justus Ndumbu, George Ogutu, Muriithi Kariuki, Juliet Okeyo, Kennedy Owallah, Angeline Mainga, Florence Vutagwa, Rose Obiero, Caleb Chacha, Perlice Njeri, George Muniu, Paul Motuka, Onyonka, Rono, na Merolyn Otiende. Shukrani za kipekee zikufikie wewe

Merolyn kwa maelekezano na midahalo tuliyokuwa nayo kipindi chote cha masomo ya uzamili. Mawaidha yako yalinifaa sana na uwe wa manufaa kwa wengine kama ulivyokuwa kwangu.

Namshehenezea shukrani za dhati dadangu mpendwa Fridah Miriko Kuria pamoja na mumewe George Kuria kwa kusimama name kipindi hiki cha masomo yangu. Fridah nakuenzi kwani, umekuwa mama na mlezi wa mwanangu. Umekuwa ukinipa moyo wa kuendelea na kunihimiza hata wakati ambapo mambo yalikuwa magumu. Siwezi kuyataja yote ulionifanyia lakini nakuombea Maulana akuhifadhi vyema na akuzidishie wema na fadhili zake pamoja na mahitaji ya moyo wako siku zote za maisha yako. Najivunia kuwa dadako.

Shukrani nyingine na zielekeza kwa tume ya kuajiri walimu T.S.C. pamoja na mwalimu mkuu wa shule yangu Bw. Gitonga Mukunga kwa kuidhinisha likizo ya masomo. Aidha Bw. Gitonga nakuenzi sana kwa mawaidha uliyonipa hasa kunihimiza kuendelea na masomo hadi upeo huu. Shukrani.

Aidha nawashukuru Pamela Kanyangi na Eunice Mudave waliopiga chapa kazi hii kwani haingekuwa kamilifu bila uchapishaji.

Mwisho, singeweza kuwataja wote waliochangia kazi hii mmoja mmoja, lakini natoa shukrani za dhati kwa nyote mliochangia kwa njia moja au nyingine kufanikisha tasnifu hii. Langu ni kuwahimiza muwe mwanga na kielelezo bora kwa wasomi wengine kama mimi.

## **ORODHA YA VIFUPISHO**

Bw. Bwana

Bi. Bibi

Dkt. Daktari

Prof. Profesa

uk. Ukurasa

TUKI Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu jinsi mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Natala* (1997) ya Kithaka Wa Mberia. Tumeshughulikia vipengele vya kimtindo vya wahusika, matumizi ya lugha na maudhui katika ujenzi na uendelezaji wa ukombozi wa wanawake katika jamii iliyotawaliwa na mfumo wa ki-ubabedume unaojitokeza katika *Natala*. Tumetumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kuchanganulia masuala ya mwanamke, na nadharia ya umuundo kuchunguza vipengele vya kimtindo.

Kazi yetu imegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza tumejadili somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, nadharia tete, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

Katika sura ya pili tumeshughulikia historia fupi ya tamthilia, awamu za maendeleo ya tamthilia- kipindi cha kabla ya ukoloni, kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni. Aidha tumeshughulikia muhtasari wa *Natala*.

Katika sura ya tatu tumechunguza mchango wa wahusika katika ujenzi na uendelezaji wa maudhui. Tumeangazia dhana ya wahusika, wahusika wakuu na wahusika wadogo, ulinganuzi wa wahusika, umakundi wa wahusika na dhima yao katika ujenzi wa maudhui.

Sura ya nne imeshughulikia matumizi ya tamathali za usemi na kunga za fasihi na athari zake katika kuendeleza maudhui. Aidha tumechunguza mandhari yalivyohusishwa na matukio katika ujenzi na uendelezaji wa maudhui.

Sura ya tano ni hitimisho la utafiti wetu. Tumejadili muhtasari wa matokeo na mapendekezo ya utafiti wa baaadaye.

## YALIYOMO

IKIRARI.....	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
ORODHA YA VIFUPISHO.....	vi
IKISIRI.....	vii

## SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Tatizo la utafiti.....	2
1.2 Madhumuni ya utafiti.....	3
1.3 Sababu za kuchagua mada.....	3
1.4 Upeo na mipaka.....	5
1.5 Nadharia tete.....	5
1.6.0 Msingi wa nadharia.....	5
1.6.1 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.....	6
1.6.1.1Ufeministi.....	7
1.6.1.2Ufeministi wa Kiafrika.....	11
1.6.2 Umuundo.....	13
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada.....	15
1.8 Mbinu za utafiti.....	19



1.9 Hitimisho.....	20
--------------------	----

## **SURA YA PILI: HISTORIA YA TAMTHILIA**

2.0 Utangulizi.....	21
2.1.0 Awamu tatu za historia ya tamthilia .....	22
2.1.1 Kabla ya ukoloni .....	22
2.1.2 Kipindi cha ukoloni.....	23
2.1.3 Kipindi cha baada ya ukoloni .....	26
2.1.3.1 Miaka ya sabini hadi miaka ya themanini.....	27
2.1.3.2 Miaka ya tisini hadi sasa.....	34
2.2 Muhtasari wa <i>Natala</i> .....	37
2.3 Hitimisho.....	40

## **SURA YA TATU: WAHUSIKA NA UJENZI NA UENDELEZAJI WA MAUDHUI**

3.0 Utangulizi.....	41
3.1 Ubainishaji wa wahusika .....	42
3.1.1 Mhusika na nafasi / majukumu .....	42
3.1.2 Umakundi wa wahusika.....	43
3.1.3 Ulinganuzi wa wahusika.....	44
3.2 Wahusika na ujenzi wa maudhui .....	45
3.2.1 Natala kama kielelezo cha utetezi wa haki na utambulisho wa mwanamke.....	45
3.2.2 Tango Mwina kama ishara ya utegemezi wa mwanamke kwa mwanamume .....	53
3.2.3 Wakene kama mwakilishi wa mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke .....	56

3.2.4 Mama Lime na Tila kama vielelezo vya urengwaji wa mwanamke katika jamii.....	59
3.2.5 Mhudumu katika jingo la ufuo kama mwakilishi wa kutowajibika kwa wahudumu wa umma na unyanyasaji wa kijinsia .....	63
3.2.6 Gane kama mwanamke anayepinga dhuluma dhidi ya jinsia ya kike .....	65
3.2.7 Aliku na Bwanu.....	67
3.2.8 Hitimisho.....	67

### **SURA YA NNE: MATUMIZI YA LUGHA YANAVYOENDELEZA MAUDHUI**

4.0 Utangulizi.....	68
4.1.0 Mbinu za lugha .....	68
4.1.1 Tashihisi/Uhuishi/Uhaishaji.....	68
4.1.2 Kinaya .....	69
4.1.3 Jazanda1`/Taswira.....	71
4.1.4 Maswali ya balagha.....	73
4.1.5 Methali, misemo na nahau .....	75
4.1.6 Takriri .....	76
4.1.7 Chuku/Mubaalagha .....	79
4.1.8 Sitiari.....	80
4.1.9 Usemajikando .....	80
4.1.10 Uzungumzinafsia .....	83
4.2.0 Mandhari na ujenzi wa maudhui.....	84
4.2.1 Utangulizi.....	84

4.2.2 Dhana ya mandhari .....	85
4.2.3 Mandhari katika <i>Natala</i> .....	86
4.2.3.1 Sebuleni mwa Natala Tango na Tango Mwina.....	87
4.2.3.2 Jengo la ufuo .....	90
4.2.3.3 Mazishini.....	92
4.4 Hitimisho.....	93

### **SURA YA TANO: HITIMISHO**

5.0 Utangulizi.....	94
5.1 Muhtasari wa matokeo.....	94
5.2 Mapendekezo .....	98
5.3 Hitimisho.....	99
<b>MAREJELEO</b> .....	100

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Tamthilia ni utanzu wa fasihi andishi unaoandikwa kwa mtindo wa mazungumzo. Tamthilia ni hadithi fupi inayowasilishwa jukwaani au kimatendo kama anavyosema Wamitila (2002:75). Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa, tamthilia ni utanzu wa fasihi unaohusu uigizaji na ndani ya uigizaji huo kuna hadithi inayosimuliwa.

Dhana ya tamthilia inatokana na kitenzi ‘*mithilisha*’ kwa maana ya fananisha. Ni kwa mujibu huu Mugambi (1982) anasema kuwa, tamthilia ni maigizo ya matukio au visa fulani kwa uhalisi wake kwa ajili ya kuyasawiri maudhui au maelezo fulani. Aghalabu tamthilia hutubainishia maisha ya jamii kwa mujibu wa kukejeli dhuluma katika jamii kama vile unyonyaji au hata kuusifu utukufu fulani.

Uhakiki wa utanzu wa tamthilia uliwekewa msingi na mawazo ya Myunani Aristotle katika kitabu chake kiitwacho *Poetics*. Aristotle aliuchunguza utanzu mdogo wa tamthilia uitwao tanzia. Katika uchunguzi wake, Aristotle alivitambua vipengele sita ambavyo aliviona kuwa muhimu katika muundo wa tanzia. Vipengele hivyo ni: msuko, wahusika, dhamira, nyimbo, maonyesho na uteuzi na matumizi ya maneno. Mawazo haya ya Aristotle yanaweza kutumiwa katika uhakiki wa tamthilia mbalimbali hasa yakifanyiwa mabadiliko fulani hata kama yalifungwa kwenye utanzu mdogo wa tanzia.

Utafiti wetu unahusu mtindo unavyoathiri fani na maudhui. Fani na maudhui ni vipengele vya fasihi ambavyo havitengani daima kwani hujengana na kukamilishana. Senkoro (1982:24) anazihusisha dhana hizi mbili kwa kueleza kuwa mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika

kazi ya fasihi, njia ambayo hatimaye, huonyesha ubinafsi na upekee wa mtunzi fulani wa kazi fulani mahsusi.

Katika utafiti wetu, tumechanganua vipengele vya mtindo na maudhui kama vinavyojitokeza katika *Natala* ya Kithaka wa Mberia ili kutathmini mtagusano uliopo baina ya vipengele hivi katika kufanikisha tamthilia husika.

### **1.1 Tatizo la Utafiti**

Tatizo letu ni kutathmini jinsi mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Natala* (1997). Kimsingi, utafiti wetu umehusu kuchunguza jinsi baadhi ya vipengele vya kimtindo vinachangia maudhui na kufanikisha tamthilia husika. Tumevishughulikia vipengele hivi vya fasihi kwa kuunga mkono anayoyasema Bennet (1979:34) kuwa vipengele vyote vya fasihi vinastahili kuangaliwa katika mshikamano wake ili utanzu mzima uweze kukamilika.

Tatizo letu la utafiti limejengeka katika misingi ya falsafa ya umuundo. Umuundo hushikilia kuwa dunia ni umbo lisiloweza kugawika. Dunia haikuumbwa kwa viungo vinavyoweza kutenganishwa na kujisimamia bali imeumbwa kutokana na mahusiano ya miundo. Miundo hii yapaswa kufikiriwa kwa jumla (Scholes, 1974, katika Wafula na Njogu 2007). Mashiko haya ya umuundo yanaungwa mkono na Wafula na Njogu (2007: 98) wanaposema;

Madhumuni ya msanii hayawezi  
kutenganishwa na jinsi msanii  
huyu anavyoiwasilisha kazi yake.  
Kadri mwanafasihi anavyowaza  
Ndivyo vipengele mbalimbali  
vya kuwazia Vinavyomjia.

Tunaafikiana na maoni ya wataalamu hawa kikamilifu. Uafiki wetu unatokana na uelewa kuwa, mtindo unahusisha fani na maudhui ambavyo ni viungo muhimu vya fasihi na ambavyo haviwezi kutenganishwa vikaweza kujisimamia kwa upekee wake katika kuwasilisha ujumbe katika kazi ya fasihi. Vipengele hivi (mtindo na maudhui), vinapaswa kuchunguzwa kiuchangizano na wala si katika upekee wake. Jambo hili ndilo lililotutia msukumo wa kufanya utafiti huu.

## **1.2 Madhumuni ya Utafiti**

Lengo letu la kimsingi lilikuwa kuchunguza jinsi mtindo unavyochangia ujenzi na uendelezaji wa maudhui katika *Natala* (1997). Hivyo basi, tunalenga kutathmini namna mtindo ulivyoweza kutekeleza wajibu wa kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

Malengo ya utafiti wetu hasa ni;

- a) Kuchunguza namna vipengele mbalimbali vya mtindo vinavyochangia uendelezaji wa maudhui.
- b) Kutathmini athari za vipengele mbalimbali vya mtindo kwa ujumbe unaowasilishwa.

## **1.3 Sababu za Kuchagua Mada**

Uteuzi wetu wa mada umeongozwa na sababu kadhaa za kiusomi. Kwanza, mtindo huhusu fani na maudhui ambayo ni mihimili ya kazi za fasihi na ambayo daima haitengani kwani hujengana, kuchangizana na kukamilishana. Kulingana na utafiti wetu wa awali tumeona ya kwamba, watafiti na wahakiki wengi wametafitia na kuhakiki maudhui au fani kwa upekee wake pasipo kushughulikia vipengele vyote (fani na maudhui). Kwa mfano, Mugambi (1982) amehakiki maudhui katika tamthilia za Kiswahili za Kenya zilizochapishwa kufikia mwaka 1982, Nyamberi (1997) anatathmini maudhui ambapo amejikita katika swala la mwamko wa mwanamke katika

tamthilia nne za Peninah Muhando: *Hatia* (1972); *Heshima yangu* (1974), *Nguzo Mama* (1982) na *Lina Ubani* (1984), Mwangi (2005) amehakiki fani katika tamthilia za Wamitila, Onyoni (2012) ameangazia fani katika usawiri wa wahusika wa kike katika *Natala* (1997) na *Mama Ee* (1987). Utafiti kuhusu vipengele vyote kiuchangizano unapatikana katika utafiti wa Nzuki (2003) ambaye ametafiti kuhusu mwingiliano wa fani na maudhui katika diwani mbili za Kithaka wa Mberia: *Mchezo wa karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001).

Hivyo basi ni dhahiri kwamba, uwanja wa mtindo na maudhui kiuchangizano haujashughulikiwa na kama umeshughulikiwa ni kwa ufinyu na hivyo, kuacha pengo la kiusomi. Pengo hili ndilo lililotutia ari ya kutaka kuliziba katika utafiti wetu wa *Natala*.

Aidha, tumechagua utanzu wa tamthilia kutokana na umuhimu wake katika jamii. Tamthilia sawa na utanzu wa ushairi na riwaya, hushughulikia masuala muhimu yanayomhusu binadamu katika ulimwengu wake.

Tumechagua *Natala* kwa sababu inalenga masuala muhimu katika jamii kama ukombozi wa mwanamke na ukombozi wa jamii kwa jumla. Masuala haya yanafaa kutathminiwa ili jamii iweze kujikomboa na kupata maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kiitikadi.

Mwisho na si akali ni kwamba, tumegundua hakuna utafiti wa awali wa moja kwa moja kuhusu mada yetu. Tumechagua somo hili tukitarajia kuwa mchango wetu utawafaa watafiti wa baadaye katika mtalaa wa fasihi na hasa utanzu wa tamthilia.

## **1.4 Upeo na Mipaka**

Kwa ujumla, tumeukita utafiti wetu katika uchanganuzi wa kimtindo na kimaudhui katika *Natala* (1997). Katika uchanganuzi wetu, tumeangazia uamilifu wa vipengele mbalimbali vya kimtindo katika ujenzi na uandelezaji wa maudhui.

Kimsingi tumechanganua uumbaji wa wahusika kwa kutathmini jinsi wanavyosawiriwa, uhalisi wao, nafasi wanazozichukua na kisha kuonyesha michango yao katika ujenzi na uandelezaji wa maudhui. Aidha tumejadili jinsi mandhari yalivyochorwa na jinsi mandhari yanavyohusiana na vitushi katika ujenzi wa maudhui. Mwisho, tumeonyesha jinsi kunga mbalimbali za lugha zinachangia katika ujenzi wa maudhui na kufanikisha lengo la mwandishi.

Japo kazi nyingine zimepitiwa ili kutilia nguvu uchanganuzi wetu, tathmini hizo hazitadhihirika humu. Mifano ya kwingineko imelengwa tu ili kuhimili uchanganuzi wa *Natala*. Aidha mifano hiyo itatumiwa pale tu pasipo budi, kusudi isipotoshe madhumuni yetu.

## **1.5 Nadharia Tete**

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- a) Vipengele mbalimbali vya kimtindo vinaathiri ujenzi wa maudhui kwa njia anuai.
- b) Uwasilishaji mwafaka wa maudhui hutegemea uteuzi na mpangilio mzuri wa vipengele vya kimtindo pamoja na maingiliano ya vipengele hivyo katika kuleta maana.

## **1.6 Msingi wa Nadharia**

Utafiti wetu ni wa kifasihi na hivyo tumeongozwa na nadharia za kifasihi na za kiisimu kulingana na uamilifu wake katika utafiti wetu. Nadharia za uhakiki wa fasihi hugawika katika makundi



matatu makuu; kundi la kwanza linalosisitizia 'kinachosemwa' (maudhui), kundi la pili linalosisitizia kinavyosemwa (fani) na kundi la tatu linalosisitiza 'ni nani anayesema nini na kama nani' ( mtunzi na hadhira ).

Katika utafiti wetu, tumetumia mseto wa nadharia kutoka kundi linalosisitiza ' kinachosemwa ' na kundi linalosisitiza 'kinavyosemwa'. Nadharia zinazosisitiza maudhui au kinachosemwa hushikilia kwamba, kazi ya fasihi huwa fasihi kwa sababu ya maudhui yake. Nadharia hizi hupiga hatua zaidi na kupendekeza aina ya maudhui yanayopaswa kuzingatiwa na fasihi. Hushikilia kwamba, fasihi ni kioo cha jamii kinachopaswa kuchora picha halisi ya maisha ya jamii husika.

Nadharia zinazosisitiza mtindo na muundo (kinavyosemwa) hukataa wazo kwamba, kazi ya fasihi yaweza kuelezwa kwa kuhusishwa na matumizi au hadhira yake au hata na mambo yaliyo nje ya kazi hiyo. Nadharia hizi husisitiza kwamba, lugha ndicho kitovu cha kazi ya fasihi na maudhui hutokea tu kwa sababu pana lugha. Kwa hivyo, shughuli ya nadharia hizi ni kuona jinsi lugha ilivyopangwa na kutumiwa kuibua maana.

Kimsingi utafiti wetu umetumia nadharia mbili: Umuundo kuchanganulia fani na Ufeministi wa Kiafrika kuhakiki maudhui katika *Natala (1997)*.

### **1.6.1 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika**

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ni moja ya matapo ya nadharia ya Ufeministi katika mwegemeo wa kimaeneo. Hivyo basi inakuwa vigumu kueleza ufeministi wa Kiafrika pasipo kueleza Ufeministi kwa ujumla.

### **1.6.1.1 Ufeministi**

Ufeministi ni dhana inayotokana na neno la kilatini 'femina' lenye maana ya mwanamke. Dhana hii inarejelea uwakilishaji wa haki za wanawake kufuatana na imani ya usawa wa kijinsia. Huu ni mwamko wa wanawake unaolenga kupigania na kukomesha udhalimu dhidi ya mwanamke kwa njia yoyote ile.

Ufeministi ni nadharia inayohusu maswala ya wanawake na inayotaribu kufichua matatizo wanayopata wanawake kama tabaka la kiuchumi na pia kama wanawake.

Mbatiah (2001: 87) anaeleza:

Ufeministi ni nadharia ya fasihi ambayo inajishughulisha  
na utetezi wa haki za wanawake dhidi ya ugandamizwaji  
katika jamii yenye mfumo uliodhibitiwa na wanaume.

Hivyo basi, Ufeministi ni nadharia ambayo imewekewa msingi na msukumo mkubwa wa kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kiuchumi, kidini, kijamii na kisiasa. Pingu hizi zimejengeka kwenye misimamo ya itikadi ya kiume.

Maswala ya kifeministi yalianza kuzungumziwa katika karne ya kumi na tisa ambapo yalishika nguvu miaka ya sitini na sabini ya karne ya ishirini. Hivyo basi nadharia ya Ufeministi inafahamika kuwa iliibuka katika muungano wa ukombozi wa wanawake uliopamba moto katika miaka ya sitini huko Marekani (Ntarangwi 2004: 46). Katika kipindi hiki, wanawake hasa wa Kimagharibi walianza kuzungumzia matatizo yao kwa kuyaandikia.

Hata kama maswala ya kifeministi yameanza kuzungumziwa miaka ya sitini, kulikuwa na jitihada mbalimbali za kupigania usawa baina ya wanaume na wanawake ingawa hazikuchapishwa kama anavyosema Onyoni (2002). Kwa mfano, katika nchi ya Ufaransa kuanzia mwaka 1789 hadi mwaka 1795, kulikuwa na maandamano ya wanawake kutetea kushushwa kwa hadhi zao kwa kile

walichokiita '*Msimbo wa Napoleon*'. Mtawala Napoleon alikuwa amesema kuwa, akili za wanawake ni dhaifu zikilinganishwa na za wanaume. Kwa hivyo, wanawake walifaa kupewa elimu ya kiwango cha chini kama ya ushonaji.

Mnamo mwaka 1848 huko Marekani Kaskazini, kuna kundi la wanawake lililoungana katika juhudi za kuleta ukombozi wa wanawake. Kulifanyika mkutano jijini New York ambapo wanawake walitangazwa kuwa huru katika misingi ya; kukubaliwa kupiga kura, kupewa elimu ya kutosha, kupewa nafasi sawa za kufanya biashara, usawa wa kupata fidia, usawa wa kisheria na kupata ajira (Onyoni 2012).

Ithibati za kimaandishi za kifeministi zenye utaratibu na zilizowekea msingi nadharia ya ufeministi ni *A vindication of the Rights of Women* ya Mary Wollstonecraft (1792) na *A Room of One's Own* ya Virginia Woolf (1929). Mary Woollstonecraft anasemekana ndiye wa kwanza kuzungumzia maswala ya wanawake kwa utaratibu maalum.

Simone de Beauvoir katika *The Second Sex* (1952) alichangia pakubwa maendeleo ya uhakiki wa kifeministi. Lengo kuu la Beauvoir lilikuwa kubainisha, kukosoa na kupiga vita asasi zilizomdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Asasi hizi ni dini, ndoa na utamaduni. Beauvoir anasema kuwa dini humkandamiza mwanamke kwa kumfundisha kunyenyekea. Ndoa nayo imejengwa kwenye misingi na imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamume akilinganishwa na mwanamke. Anadai kuwa utamaduni humsawiri mwanamke katika tamathali hasi na duni.

Kate Millett katika *Sexual Politics* (1977) ameleta athari kubwa katika historia ya Ufeministi. Millett aliwashambulia waandishi wanaume kama vile Henry Miller, Norman Miller, Jean Gennet na D.H.Lawrence kutokana na jinsi walivyowasawiri wahusika wa kike. Kutokana na aliyoyagundua katika kazi hizo, Millett anabainisha kuwa miundo ya kijamii pamoja na asasi zake zinashirikiana kumkandamiza mwanamke. Millett aidha anaishambulia mikabala ya saikolojia-

changanuzi ya Sigmund Freud kwani ina mapendeleo makubwa kwa mfumo wa ki-ubabedume. Freud alisema kuwa mtoto wa kike huanza kujichukia mara tu anapotambua kuwa hana kiungo cha kiume. Hali hii husababisha alichokiita 'wivu' wa zubu'. Kutokana na wazo la 'wivu wa zubu' la Freud, Millet anadahili kuwa wivu uliopo ni wa uwezo alio nao mwanamume kutokana na muundo wa kijamii. Mwanamke anakuwa na wivu wa kinachoashiriwa na hilo zubu wala sio zubu kama kiungo cha mwili.

Ogundipe-Leslie (1994) ana maoni kuwa wanawake wamepeva majukumu duni na yanayosawiriwa kwa ubaya kama vile kuwa wachawi na wanaume nao husawiriwa kuwa werevu, wenye nguvu na kuaminika na wenye uwezo wa uongozi kwa kuzaliwa. Ogundipe-Leslie anasema hali kama hii huchangia kumdunisha na kumtesa mwanamke katika jamii.

Kuna wataalamu wengine ambao wamechangia na kutoa maoni yao kuhusu ufeministi. Tuliowataja ni baadhi yao tu.

Ufeministi kama nadharia, hufumbata pamoja mikabala na mitazamo kadhaa. Ni kwa mantiki hii ndipo tunapata matapo mbalimbali ya Ufeministi. Matapo ya Ufeministi hubainishwa kupitia njia mbili kuu: kiitikadi na kimaeneo (Wafula na Njogu 2007:92).

Mkabala wa kiitikadi unahusu mitazamo mitatu mikuu ya Ufeministi: Ufeministi Huru, Ufeministi wa Kijamaa na Ufeministi wa Kimapinduzi (Wafula na Njogu 2007). Ufeministi Huru hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha. Ufeministi wa Kijamaa hulenga kukosoa jamii na hivyo, huwahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhaa nyingine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za wanawake. Ufeministi wa Kimapinduzi pia huitwa Ufeministi wa Kiharakati. Ufeministi huu humchukulia mwanamume kama adui mkubwa zaidi wa mwanamke. Kwa hivyo, Ufeministi huu huhusisha

ukandamizwaji wa mwanamke na tofauti za kimaumbile. Tapo hili hushikilia kuwa wanawake wanapaswa waitawale miili yao na hata wasiolewe.

Njia ya kuainisha matapo ya Ufeministi kimaeneo huhusisha Ufeministi na maeneo ya kijiografia. Waitifaki wa kuainisha Ufeministi kimaeneo ni Mary Eagleton (1991) na Ross Murfin (1991). Wanaugawa ufeministi katika matapo manne: Ufeministi wa Kifaransa, Ufeministi wa Kingereza, Ufeministi wa Kimarekani na Ufeministi wa Kiafrika.

Ufeministi wa Kifaransa unalenga kufafanua jinsi lugha hutoa maana ya mtumiaji wake. Wanadai kuwa lugha kama inavyotumiwa ni zao la taasubi za kiume. Wanasema kuwa lugha inampendelea mwanamume kuliko mwanamke. Jazanda za kuelezea uwezo, nguvu na mamlaka ni za kiume na ilhali zile zenye kusawiria ulegevu na kutoweza ni za kike. Ufeministi wa Kimarekani unahusishwa na kazi ya Mary Ellman *Thinking about Women* (1968). Mary aliangalia jinsi wanawake wanasawiriwa kwa namna mbalimbali katika kazi zilizoandikwa na wanaume na jinsi wanawake walivyoendeleza usawiri huo hasi wa wanawake katika kazi zao. Betty Friedan katika *The Feminine Mystique* (1963) anachunguza maisha ya mwanamke ambayo anasema ni jambo lisiloleweka na wanaume na pia wanawake wenyewe. Wengine waliochangia ufeministi wa Kimarekani ni kama Freud (1950) na hasa kuhusiana na 'wivu wa zuby' pamoja na Kate Millett (1979). Tapo hili linashikilia kwamba, wanawake wana namna yao ya kipekee ya kuandika na kujieleza. Aidha, wanasema kuwa kuna dhamira zinazorudiwarudiwa katika tungo za wanawake. Wanashugulikia kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake na pia wanaume maadamu zinaongea juu ya wanawake. Ufeministi wa Kiingereza huchukulia kuwa, mambo ya kihistoria na siasa ndiyo huathiri matendo ya wanawake.

### **1.6.1.2 Ufeministi wa Kiafrika**

Ufeministi wa Kiafrika ndilo tapo tutakalotumia katika utafiti wetu kwani ni Ufeministi unaohusishwa na bara la Afrika.

Wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vitengo vya utamaduni huu ni ; desturi na mila zinazomdhalilisha kama vile kuonewa kwa mwanamke asiyezaa, kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi wa mwanajamii, tohara na ukeketwaji wa wanawake pamoja na kimya cha kulazimishwa.

Millett (1977) anasema kwamba Ufeministi wa Kiafrika umetokana na utamaduni katika jamii iliyojikita katika kilimo na ushiriakiano wa kijamii. Umejengeka katika misingi thabiti ya kumhusisha mwanamke katika shughuli tofauti za jamii bila kuangalia asasi zinazotawaliwa na mwanamume. Kulingana na Millett, Ufeministi wa Kiafrika husisitiza usawa katika shughuli za jamii na utoaji uamuzi kwa wanawake na wanaume.

Strobel (1980) anauona ufeministi wa Kiafrika kama uliokumbana na changamoto nyingi kutokana na asasi tofauti kwa sababu huwa unataka kujua chanzo cha ubaguzi katika maswala ya kiutawala. Mwelekeo pinzani unasisitiza uongozi wa jinsia ya kiume ambao umeupa changamoto nyingi sana mwelekeo wa Ufeministi wa Kiafrika.

Steady (1981) anasema kuwa Ufeministi wa Kiafrika unajikita katika misingi inayoangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanayotegemeana na kukamilishana, yenye usambamba na usawa katika kuiendeleza jamii. Anaeleza kuwa Ufeministi wa Kiafrika huweka pamoja maswala ya jinsia, ubaguzi, utabaka na mielekeo tofauti ya kiutamaduni ili kuibua Ufeministi unaomwangukia mwanamke kama kiumbe lakini sio kama kiumbe kijinsia. Anaongezea kuwa

Ufeministi wa Kiafrika huchunguza maswala ya kitamaduni yanayomlemaza mwanamke. Aidha hushughulikia maswala ya kijinsia kwa kujikita katika muktadha wa Kiafrika.

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza mihimili ya kimsingi ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Wanasema Ufeministi wa Kiafrika ni kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke wa Kiafrika ili kumsaidia mtu yeyote kuelewa hali hiyo.

Mtazamo wa Ufeministi wa Kiafrika, vilevile hujaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahuosika wa kike wanaoweza kuigwa na ambao hawawategemei wanaume ili kujitambulisha. Aidha, kisaikolojia wawe ni wanawake wanaojielewa na kujiamini wala wasiwe wanahisi kama wana udhaifu kwa ajili ya umenke wao.

Nadharia hii inanuia kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa jinsia na utamaduni. Inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu na wala si za kimaumbile na za kijadi. Ni mtazamo unaokuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

Aidha, lengo muhimu la nadharia hii ni kuvumbua na kuziweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume. Pia inanuia kuchunguza historia ya fasihi ya jadi ya kike na kuwamulika waandishi wa kike waliotambua hali za wanawake na ambao wanaweza kuchukuliwa kama vielelezo kwa wasomaji wao.

Kama anavyosema Mbatiah (2001), lengo kuu la uhakiki wa kifeministi na hasa Ufeministi wa Kiafrika ni kuzua mikakati ambayo itaangazia kutathmini jinsia ya kike, mitazamo, thamani na matakwa ya wanawake sio tu katika fasihi, bali nyanja zote za maisha ya binadamu.

Hatimaye, nadharia hii hunuia kuzindua mwamko kwa wanawake na jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine.

## 1.6.2 Umuundo

Chimbuko la nadharia ya Umuundo ni Urusi kama wanavyosema Fokkema na Ibsch (1995). Wanasema kuwa asili ya nadharia ya Umuundo ni urasimu wa Kirusi ulioanza kutumika katika uhakiki mnamo mwaka wa 1920. Mashiko yao yana uhusiano na madai ya Scholes (1974:60) kuwa, nadharia ya Umuundo ina uhusiano wa karibu na Urasimu huku akieleza kuwa msingi wake ni urasimu na hasa wa Urusi. Wamitila (2002) anaunga mkono mawazo ya Scholes (1974) kwa kueleza kuwa nadharia ya Umuundo inahusishwa na wanaisimu wa shule ya Prague. Mji wa Prague ulikuwa makao ya kikundi cha wanaisimu ambao walitorokea huko baada ya kupigwa marufuku huko Urusi.

Nadharia ya Umuundo iliwekewa msingi na mawazo ya mwanaisimu Mswizi Ferdinand de Saussure na ambayo yalikitwa katika lugha. Alikuwa na mawazo tofauti kuhusu uchanganuzi wa lugha. Hata kama uwanja wake ulikuwa wa isimu, mawazo yake pia yanatumika katika utafiti wa nyanja nyingine kama vile fasihi na anthropolojia. Mwanaisimu de Saussure alibuni dhana za *langage*, *langue* na *parole*. Anaeleza dhana ya *langage* kama kipawa cha usemi ambacho kila binadamu asiye na upungufu wa kusema huwa nacho. Kwa hivyo dhana ya 'langage' inasimamia lugha zote na kwa hivyo, tunaweza kuchukulia 'langage' kama fasihi zote za kilimwengu. *Langue* ni mfumo dhahania wa lugha fulani ambao hutumiwa na jamii fulani. Kwa hivyo, lugha huchukuliwa kama mfumo changamano ambao ndani yake kuna mifumo tofauti kama vile fonolojia, sintaksia, semantiki na morfolojia. Mifumo hii huhusiana na kukamilishana kama vilivyo vipengele vya fani na maudhui katika fasihi. Hawkes (1977:20) anaeleza tofauti kati ya *langue* na *parole* kwa kuonyesha *langue* kama mfumo wa lugha na 'parole' kama ubainikaji wa mfumo-lugha katika usemi. Vipengele hivi viwili ndivyo muhimu katika utafiti wetu. De Saussure vilevile alipendekeza utafiti wa lugha kisinkronia yaani, katika kipindi maalum badala ya



kidaikronia ambao huchunguza lugha kihistoria. Wazo hili ni muhimu katika utafiti wetu kwani tumechanganua matumizi ya lugha katika kazi maalum-yaani kisinkronia.

Kulingana na mawazo ya de Saussure fasihi inastahili kuchunguzwa kama muundo mmoja uliojengwa kwa vipengele tofauti vinavyoshirikiana kukiunda kitu kizima. Kwa mujibu wa kazi yetu tumeangalia jinsi vipengele tofauti vya mtindo vinavyochangia yaliyomo (maudhui) katika kuunda tamthilia nzima ya *Natala*. Nadharia ya Umuundo huchunguza vipengele mbalimbali vya mfumo wa fasihi kwa kuchunguza jinsi vinavyohusiana katika kukamilisha kazi husika. Hili limetokana na mawazo ya de Saussure ya kupinga kuchanganua lugha kwa kuangalia kiungo kimoja kimoja bila kuhusisha viungo mbalimbali. Kwa mfano, tamthilia ina viambajengo kama vile vya wahusika, mandhari, msuko, matumizi ya lugha na usimulizi (dayolojia na monolojia) vyote katika mfumo mmoja wa yaliyomo.

Nadharia hii pia hulenga kwenye matini ya kifasihi na kupuuza maswala mengine nje ya fasihi kama anavyosema (Wamitila 2002:179). Kwa mfano, inapuuza muktadha wa kijamii na mawazo ya mtunzi. Mwelekeo huu unazua utata na hivyo kupelekea kupingwa na wataalamu kama vile Jacques Derrida (1973,1976); Julia Kristeva (1981, 1984, 1986) Jacques Lacan (1977) Michael Foucault (1978, 1979, (a) na (b), 1981, 1986) na Louis Althusser (1971) ambao wanapinga wazo la de Saussure la kuzikita ishara katika matendo ya ‘jamii ya lugha’ na kudai kuwa maana haitokani na mzungumzaji au msemaji binafsi bali hutokana na matokeo ya maingiliano ya kijamii ambayo kwa vyovyote vile, huwahusisha wazungumzaji binafsi. Kwa hivyo, wataalamu hawa wanaieleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuikita kwenye muktadha wa kijamii. Wanashikilia kuwa kiashiriwa hakiwezi kuwa funge kama anavyodai Saussure kwani katika miktadha mingi ya matumizi ya kiashirii, kiashiriwa chake au maana yake huhamishwa au huahirishwa (Wamitila 2002:179).

Ntarangwi (2004:42) anasema kuwa, mhakiki anayezingatia muundo wa lugha zaidi ya matini bila shaka hupuuza dhana ya jadi kuhusu kile matini hiyo huweza kutueleza kuhusu maisha na hivyo basi, hufanya mtindo wa kazi yenyewe kiini cha uhakiki wake. Kwa hivyo, wahakiki wa kimuundo huzingatia matini peke yake huku wakiepuka kuifasiri kazi husika kulingana na kaida zilizowekwa kuhusu jinsi matini hufanya kazi. Nadharia hii inachukulia kwamba, kila kitu kimeundwa katika mpangilio usiotatanika na usiotegemea mambo mengine yaliyo nje yake. Hata hivyo, utafiti wetu umekitwa katika muundo wa kazi nzima kwa kuvihusisha vipengele vyote vya fasihi.

### **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu utanzu wa tamthilia na hasa kuhusu fani na maudhui, lakini hakuna utafiti wa moja kwa moja kuhusu mada yetu.

Mugambi (1982) ametumia nadharia ya U\_marx kuhakiki maudhui katika tamthilia zilizochapishwa nchini Kenya za kipindi kati ya mwaka 1957 hadi mwaka 1981. Katika utafiti wake, Mugambi ameonyesha mbinu (fani) walizotumia waandishi wa tamthilia hizo katika kuendeleza maudhui mbalimbali. Miongoni mwa maudhui aliyoyachanganua ni udhalimu, usaliti, ukombozi, nafasi ya mwanamke katika jamii, utetezi wa haki za wanyonge na hasa haki za mwanamke, ubepari na ukoloni mamboleo. Ameonyesha mazingira, wahusika, matumizi ya lugha na hasa matumizi ya jazanda na tamathali za usemi kama mbinu muhimu katika ujenzi wa maudhui. Kazi ya Mugambi imetufaa katika utafiti wetu hasa kuhusu alivyotumia mbinu za kimtindo kujenga na kuendeleza maudhui. Aidha yapo maudhui yanayoshabihiana na maudhui tutakayochanganua katika utafiti wetu. Hivyo basi, uchanganuzi wake wa maudhui umetusaidia kuchanganua maudhui katika kazi yetu.

Lugano (1989) ameshughulikia usawiri wa mwanamke kisiasa, kiuchumi na kijamii katika riwaya nne za Kezilahabi- *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Gamba la Nyoka* (1979) katika misingi ya 'Ki-Marx'. Katika kazi hizi, Lugano ameonyesha jinsi mwanamke alivyosawiriwa kama mtegemezi wa mwanamume, chombo chake na chanzo cha maovu yote. Hata kama Lugano amejikita katika utanzu wa riwaya, sisi tukiegemea tamthilia, utafiti wake umetufaa kwa sababu unatochorea picha iliyopo kumhusu mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Tumetumia misingi hii kutathmini wahusika wa kike katika utafiti wetu.

Kiango (1992) ametafiti maudhui katika tamthilia kwa kulenga taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili za Kenya. Katika kazi yake, mwanamke amesawiriwa kwa njia hasi kama kiumbe tofauti na mwanamume, mwanamke ameumbwa kama mtu anayeendeleza maudhui mabaya kwa vile amesawiriwa kuwa mzinifu, mbaya na mwuaji. Utafiti wa Kiango umetufaa kuelewa maudhui yaliyoendelezwa na mwanamke na kuonyesha nafasi ya mwanamke na mwanamume katika jamii. Sisi tumeonyesha jinsi mwanamke na mwanamume walivyo na uwezo sawa na kuwa mwanamke, huendeleza maudhui mazuri sawa na mwanamume.

Mosoti (1993) amehakiki maudhui katika tamthilia nne za Emmanuel Mbogo: *Giza limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* (1981(a)), *Watoto Wetu* (1981 (b)) na *Ngoma ya Ng'wanamaludi* (1988). Amehakiki maudhui katika misingi ya nadharia ya uyakini wa kijamaa. Miongoni mwa maudhui aliyohakiki ni ukombozi, dhuluma, usaliti, ubinafsi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Utafiti wa Mosoti umetufaa katika kutuelekeza njia za kuchanganua baadhi ya maudhui katika utafiti wetu.

Musyoka (1996) katika kuhakiki fani katika tamthilia nne za Jay Kitsao: *Uasi* (1980), *Malimwengu Ulimwenguni* (1983), *Bibi Arusi* (1983) na *Tazama Mbele* (1987), amechanganua

vipengele vya fani kwa madhumuni ya kubainisha ufanifu au udhaifu ulioko katika uumbaji wa viambajengo vya fani katika usambamba wa msingi na kaida za utanzu wa tamthilia. Anatubainishia kuwa fani ni umbuji na ufundi wa kipekee ambao huhusishwa na mtindo wa mwandishi mahsusi. Kwa ujumla, ametathmini umbuji wa msanii na jinsi fani ilivyoathiri na kuchangia katika kiwango cha kisanaa cha kazi hizo. Ametumia nadharia ya Umuundo katika uhakiki wake. Utafiti wetu utaegemea mtazamo wa Musyoka kuonyesha jinsi mwandishi Kithaka wa Mberia ametumia vipengele vya mtindo kama msanii na jinsi matumizi ya vipengele vya mtindo yamechangia kujenga maudhui (yaliyomo) ya *Natala* .

Sarara (1997) amechanganua maudhui katika tamthilia za S.A. Mohammed. Sarara ameyashughulikia maswala ya kijamii katika tamthilia tatu: *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995). Amechanganua maudhui katika misingi ya Uyakiniifu wa Kisoshalisti. Maudhui anayoyashughulikia yanalenga jamii ya kisasa kama vile kudhulumiwa kwa mwanamke, mapambano ili kuleta ukombozi, ufisadi na uozo mwingine katika jamii na umaskini miongoni mwa maudhui mengine. Utafiti wa Sarara umetufaa kwa vile maudhui aliyoyazungumzia yameangaziwa katika utafiti wetu. Kwa hivyo, kazi yake imekuwa msingi wa kuchanganulia maudhui katika kazi yetu.

Krugger (1998) katika usawiri wa wanawake kulingana na waandishi wa Kiafrika waliondika riwaya na hadithi fupi, anasema kuwa waandishi hawawasawiri wahusika wanawake kama wahusika wakuu bali kama wahusika wajenzi. Kutokana na madai haya ni dhahiri kwamba, wahusika wa kike hawajatumiwa kukuza maudhui makuu katika kazi hizo kwani maudhui makuu humzunguka mhusika mkuu. Hata kama Krugger amesawiri wahusika wa kike katika utanzu wa riwaya na hadithi fupi, utafiti huu umetufaa katika usawiri wa mhusika mkuu Natala ambaye ni mwanamke katika kazi yetu.

Magare (2002) amehakiki tamthilia ya S.A Mohammed *Amezidi* (1995) kwa kutumia nadharia ya ya Udhanaishi akizingatia kipengele cha ubwege. Katika utafiti wake, Magare anachunguza ni kwa kiasi gani *Amezidi* (1995) ni kazi ya kibwege kwa kuzingatia yaliyomo (maudhui) na fani. Kwa upande wa fani, Magare amefafanua wahusika na uhusika, mazingira, matumizi ya lugha katika mawasiliano na ploti kudhihirisha jinsi vipengele hivi vimechangia ubwege katika kazi husika. Kazi ya Magare imekuwa ya manufaa kwetu kwa sababu, hata kama ameeleza fani ilivyochangia ubwege, tumetumia njia alizotumia kuchunguza mtindo wa mwandishi kwa lengo la kujenga maudhui katika tamthilia tunayoshughulikia.

Momanyi (2002) katika makala, “Swala la Uana katika Utafiti wa Fasihi ya Kiswahili” anajadili Nadharia ya Ufeministi kama nadharia badalia ya Kiafrika inayoweza kushughulikia fasihi za Kiafrika ikiwemo fasihi ya Kiswahili. Aidha ameanisha vigezo vinavyoweza kutumiwa ili kuteua nadharia kama hiyo. Anaeleza lengo la nadharia hii kuwa ni kufufua na kurutubisha sauti ya mwanamke wa Kiafrika ambayo kwa miaka mingi imekuwa imefukiwa na mamlaka ya kiume. Kazi hii ya Momanyi ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa inatupa mwongozo kuhusu Nadharia ya Ufeministi ambayo ni mojawapo ya nadharia zinazoelekeza utafiti wetu.

Nzuki (2003) ameshughulikia mwingiliano wa fani na maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Nzuki amechanganua vipengele vya fani na maudhui katika diwani za *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001) ili kubainisha kuchangizana kwa vipengele hivi vya fasihi katika kuiumba kazi nzima katika kila diwani. Ametumia nadharia za Umuundo na Kisosholojia katika uchanganuzi wake. Utafiti wa Nzuki unakaribiana sana na utafiti wetu lakini tofauti ni kwamba, utafiti wake unaegemea utanzu wa ushairi huku wetu ukiegemea utanzu wa tamthilia. Aidha anatomia mseto wa nadharia ya Umuundo na ya Kisosholojia huku utafiti wetu ukiongozwa na nadharia za Umuundo na Ufeministi wa Kiafrika. Utafiti wa Nzuki ni wa manufaa ya kimsingi

kwetu kwani Nzuki ni mwitifaki wa uchunguzi wetu. Ameshughulikia jinsi vipengele vya fani kama mtindo wa mwandishi huingiliana na kipengele cha maudhui katika kuifanikisha kazi husika. Hata kama Nzuki amekita utafiti wake katika ushairi, utafiti wake umekuwa mhimili mkuu katika utafiti wetu.

Nyaosi (2008) anazungumzia taswira ya mwanamke katika riwaya za *Kiu* ya M.S. Mohamed na *Msimu wa vipepo* ya K.W. Wamitila kwa kutumia nadharia ya ufeministi. Anashughulikia maudhui ya udhalimu na ukandamizwaji wa mwanamke katika asasi ya ndoa. Hata kama utafiti wake umeegemea utanzu wa riwaya utatufaa kwa sababu jambo la kimsingi katika kazi yake ni kuonyesha jinsi mwanamke anadhulumiwa katika misingi ya ndoa. Tumetumia misingi hii kutathmini kama Natala amedhulumiwa katika misingi ya ndoa na wahusika kama vile Mama Lime na wahusika wengine katika ukoo wa Tango akiwemo Wakene nduguye Tango.

Were (2012) anaonyesha jinsi vipengele vya fani: ploti, wahusika, dayolojia na monolojia vinavyohusiana na kufanikisha ujenzi wa tamthilia ya *Kilio cha Haki* (1981) ya Alamin Mazrui na *Kijiba cha Moyo* (2009) ya Timothy Arege kwa kutumia nadharia ya umuundo. Kazi yake imetufaa katika kushughulikia wahusika na uhusika kwa lengo la ujenzi wa maudhui.

### **1.8 Njia za utafiti**

Tumetumia njia tofautitofauti katika utafiti wetu. Kwanza, tumeisoma kazi teule kwa kina kwa misingi ya Ufeministi wa Kiafrika ili tuweze kupata mwanga na mihimili ya kufikia upeo mpevu wa kiuchanganuzi na wenye ithibati za kisanaa na kinadharia.

Uchanganuzi wetu umekuwa wa kinaelezo na wala si wa kitakwimu. Hivyo basi utafiti wetu umejifunga katika udurusu wa vitabu, tahakiki na makala kwa lengo la kupanua mawanda ya

uelewa. Tumetalii na kurejelea maoni ya wasomi wengine waliochangia mawazo na maoni kuhusu mtindo na maudhui aghalabu katika utanzu wa tamthilia katika misingi ya umuundo.

Kimsingi, utafiti huu umekuwa wa maktabani. Hata hivyo, tumeshiriki mahojiano ya moja kwa moja na baadhi ya wataalamu wa fasihi na nadharia wa Idara ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu Cha Nairobi pamoja na vyuo vikuu vingine ili kupata maarifa zaidi kuhusiana na utafiti wetu.

Tumetia maanani utandaridhi katika usomi na kwa hivyo, tumetumia mtandao kuongeza tuliyoyasoma vitabuni.

## **1.9 Hitimisho**

Katika sura hii ya kwanza, tumeshughulikia mambo ya kitangulizi ya utafiti. Tumejadili juu ya masuala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti wetu. Masuala hayo ni utangulizi, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia tete zitakazotuongoza katika utafiti, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, njia za utafiti na hatimaye, hitimisho la sura.

## SURA YA PILI

### HISTORIA YA TAMTHILIA YA KISWAHILI

#### 2.0 Utangulizi

Tamthilia ya Kiswahili zinahusishwa na Afrika Mashariki hususan nchi za Kenya, Tanzania na Zanzibar. Historia ya tamthilia ya Kiswahili kama tunavyojua hii leo, ina asili yake kutoka fasihi ya Kiingereza kwani kazi za mwanzo zinazochukuliwa kuwa ni tamthilia za Kiswahili zina muundo wa tamthilia ya Kimagharibi kama anavyosema Mugambi (1982) akiungwa mkono na Bertoncini (1989). Kenya inachukuliwa kuwa chanzo cha tamthilia ya Kiswahili kama anavyosema Bertoncini (2009). Inasemekana kuwa tamthilia ya Kiswahili nchini Kenya ilianzishwa na mzungu Graham Hyslop katika awamu ya pili ya miaka ya hamsini. Hyslop katika mwaka wa 1957 aliandika michezo miwili mifupi ya kuigiza: *Mgeni Karibu* na *Afadhali Mchawi*. Kazi ya Hyslop iliendelezwa na wanafunzi wake wawili Henry Kuria aliyeandika *Nakupenda Lakini* (1957) na Gerishon Ngugi aliyeandika *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* (1961). Tamthilia za Hyslop pamoja na za wanafunzi wake zilichukua muundo wa tamthilia ya Kimagharibi. Ni tamthilia zilizokitwa katika ujumisia na hivyo lengo lake kuu lilikuwa kufurahisha. Masuala yaliyoangaziwa hayakuwa na ukweli wowote kwa jamii ya Mwafrika bali yalilenga kumsifu Mwingereza huku Mwafrika akibezwa.

Nchini Tanzania, uandishi wa tamthilia umeanza mwishoni mwa miaka ya sitini baada ya Kenya. Hata hivyo, uandishi wa tamthilia nchini humu ulishika kani na kuendelea zaidi ya ilivyokuwa nchini Kenya hadi kufikia miaka ya 1980. Hata kama Zanzibar ndiyo asili ya hadithi fupi na riwaya ya Kiswahili ya kisasa, uandishi wa tamthilia ya Kiswahili haukuendelezwa sana nchini humo (Bertoncini 2009: 222). Mwasisi wa uandishi wa tamthilia ya Kiswahili Zanzibar ni Farouk



Topan aliyekuwa mhadhiri wa isimu katika chuo kikuu cha Dar es Salaam aliyeandika *Mfalme Juha* mnamo mwaka wa 1963 lakini ikachapishwa mwaka wa 1971 kwa lengo la kutumbuiza.

Tumeangalia historia ya tamthilia katika awamu tatu: kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya uhuru.

## **2.1.0 Awamu Tatu za Historia ya Tamthilia**

### **2.1.1 Kabla ya Ukoloni**

Tamthilia kama tanzu zingine za fasihi andishi ina misingi katika kama fasihi simulizi. Fasihi simulizi ndiyo ujumla wa maisha ya jamii kwani inahusu matukio, imani, mwelekeo, kazi, itikadi, mwonoulimwengu, mila na tamaduni katika mazingira maalum. Fasihi simulizi ni mfumo mzima wa jamii na hivyo barani Afrika imechukuliwa kuwa tukio la kijamii kwa kuwa inamhusisha kila mtu katika jamii. Matukio katika fasihi simulizi yalihusu maisha halisi ya wanajamii husika. Ruyendo (1974) katika Bertocini (2009) anasema kuwa katika uwasilishaji wa fasihi hii, hadhira hushiriki kama wapendavyo kwa kupiga makofi au kupiga mbinja kwa maana, hadhira kushirikishwa kiutendaji.

Inasemekana kuwa uigizaji ambao ni asili ya tamthilia ya Kiswahili ulikitwa katika nyimbo, ngoma na matambiko barani Afrika. Sifa muhimu katika uigizaji huo wa kijadi na ambayo ina umuhimu sana katika tamthilia iliyoandikwa ni kuwa fasihi ni zao la jamii na wala si mali ya mtu binafsi kama ilivyo katika tamthilia ya kimagharibi. Maonyesho ya kiafrika yalisuta tabia ambazo hazikuambatana na maadili ya Kiafrika na hivyo, kusifu hulka zilizokubalika katika jamii ya

Mwafrika. Hivyo basi, kila mwanajamii alinufaika kimaadili na hivyo kustawi kijamii kupitia maelekezo yaliyotokana na fasihi hiyo.

Majilio ya wageni na Wakoloni barani Afrika, yalikatiza maendeleo ya ukuaji wa uigizaji wa Kiafrika. Uigizaji wa ngoma, matambiko na hadithi ulichukuliwa na Wamisheni kuwa mambo ya kishenzi na kishetani kama anavyosema Bertoncini (2009: 172). Mlama (1975) katika Bertoncini (2009) anasema, Waafrika enzi ya ukoloni walitawaliwa na fikra za wamisheni hao na hivyo, kukubali mtindo wa tamthilia za kimagharibi za Shakespeare, Sheridan na Moliere kama tamthilia bora zaidi na za kipekee. Hivyo basi, mtindo huu wa kidrama ukaingizwa katika mtalaa wa elimu, vikundi vya drama vya wakati huo na vikundi vya maonyesho vilivyoongozwa na Wakoloni. Kuanzia wakati huo, michezo iliyoandikwa, matumizi ya jukwaa ya kawaida na pazia ziliingizwa katika uigizaji. Kwa jumla uigizaji nchini Kenya na nchini Tanzania katika kipindi cha ukoloni ulitawaliwa na tamthilia za kimagharibi.

### **2.1.2 Kipindi cha Ukoloni**

Wakati wa ukoloni unajumuisha kipindi cha miaka ya hamsini hadi miaka ya sitini. Kipindi cha kabla ya uhuru tamthilia ilichukuliwa kama mchezo ulioandikwa na hivyo michezo iliyoandikwa katika kipindi hiki ilikusudiwa kumrahisishia mkoloni utawala. Kwa hivyo, maudhui yalimlenga mkoloni na utawala wake ambao ulisifiwa sana huku utamaduni wa Mwafrika ukibezwa na kudunishwa.

Kulingana na Mugambi (1982) akiungwa mkono na Bertoncini (1989), tamthilia zilizochapishwa katika lugha ya Kiswahili katika muundo wa fasihi ya Kiingereza ziliandikwa kuanzia mwaka wa

1957. Tamthilia hizi zilikuwa vichekesho na tamthilia fupifupi ambazo ziliigizwa katika mashule mwishoni mwa muhula au kama mashindano wakati wa sherehe maalum.

Mifano ya tamthilia zilizochapishwa katika kipindi hiki ni pamoja na; *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu* za Graham Hyslop (1957), *Nakupenda Lakini* (1957) ya Henry Kuria pamoja na *Nimelogwa Nisiwe Na Mpenzi* (1961) ya Gerishon Ngugi.

*Afadhali Mchawi* inaonyesha mandhari ya hospitalini ambapo wahusika wakuu ni Issa na Ali. Issa ambaye ni mhusika mkuu amejenga maudhui ya ufisadi ambao unatokana na ubinafsi. Issa anauza dawa ambazo zinastahili kutibia wagonjwa bila kujali maslahi ya wengine. Hyslop amedhihirisha ufisadi huu miongoni mwa jamii ya Mwafrika aliyoibuni kupitia Issa. Maudhui mengine yanayojitokeza katika tamthilia hii ni ukoloni , udhalimu wa ukoloni kupitia kutozwa kodi, elimu inayochukuliwa kama msingi wa Mwafrika wa kubatiliza mila na desturi za Waafrika huku waliosoma wakiiga tabia za kigeni kama vile, mavazi, lugha na hata taratibu za maisha.

Hyslop ameisawiri jamii ya Mwafrika kama kielelezo cha kutoaminika, ufisadi, wizi na mtu duni. Kwa upande mwingine amemjenga Mwingereza kuwa wa tabaka tawala, kibepari, unyonyaji na lisilomthamini Mwafrika. Kwa upande wa wahusika, Hyslop katika kuusawiri ufisadi wa Issa, amewaumba wahusika waadilifu kama Ali ambaye ni tabibu mwadilifu pamoja na wazazi wake.

*Mgeni Karibu* inamzunguka mhusika mkuu Said. Kupitia Said tunauona usultani na utawala ambao alirithi kupitia ufisadi wa babake. Maudhui mengine yanayojitokeza katika tamthilia hii ni pamoja na ubinafsi na tamaa inayoendelezwa na mjombake Said -Shabani. Lengo la Hyslop katika tamthilia hii ni kuwapotosha Waafrika wasiupinge utawala dhalimu. Ameichora jamii iliyochochwa na utawala dhalimu lakini jitihada za kumwondoa mkoloni zinapingwa. Kwa jumla,

tamthilia hii inalenga kuudunisha utu wa Mwafrika na kutukuza vitendo vya udhalimu vya Waingereza.

*Nakupenda Lakini*, inahusu suala la mapenzi na ubinafsi. Mhusika mkuu Kangwana kwa kuongozwa na ubinafsi, anashiriki wizi na mauaji mradi apate pesa na kutajirika ili apendwe na Roda. Mapenzi baina ya Kangwana na Roda yanaonekana si ya dhati. Roda hampendi Kangwana lakini mali yake. Mapenzi haya ndiyo yanayompelekea Kangwana kushiriki kitendo cha mauaji na wizi.

Tamthilia za Hyslop *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu* na tamthilia ya Kuria *Nakupenda Lakini*, ni zimejikita katika tamasha na ulimbwende huku wananchi wakiteswa na kuuawa chini ya ukoloni katili na dhalimu.

*Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi*, inaangazia mapenzi baina ya vijana wa Kiafrika. Inaangazia mgongano baina ya wazee na vijana unaotokana na mabadiliko ya mazingira katika jamii. Wazee wanashurutisha ulipaji wa mahari ilhali vijana wanauona kama ‘ununuzi’ usio na msingi katika mapenzi ya dhati. Mapenzi ya dhati yanadhihirika baina ya Beatrice na Ben ambao ni wahusika wakuu.

Tamthilia zilizoandikwa katika kipindi cha ukoloni zimejikita katika ulimbwende ambao lengo lake ni kufurahisha tu. Ni tamthilia ambazo hazikuonyesha uhalisia katika jamii bali zilichukua muundo wa vichekesho. Wahusika walisukwa kwa namna ambayo walijenga tamthilia hizo. Misuko sahili ilitumika katika tamthilia hizo huku lugha ikiambatanishwa na mazingira ya matumizi.

Kutoka mwaka wa 1965, baadhi ya tamthilia zilitungwa moja kwa moja katika lugha ya Kiswahili huku nyingine zikitafsiriwa kutoka lugha za kigeni au kutoka lugha ya Kiingereza. Kwa mfano,

tafsiri ya Morrison- *Mchuuzi Muungwana* (1966) ya J.B.P. Moliere. Mwaka wa 1967 E. N. Hussein aliandika *Wakati Ukuta* na Alikiona naye Crispin Hauli akaandika *Dunia Iliyofarakana*. Mwaka wa 1968, Nkwera aliandika *Johari Ndogo* huku S.S. Mushi akiandika tafsiri ya Macbeth ya Shakespeare. Tafsiri nyingi zilichapishwa mwaka wa 1969 ambazo ni pamoja na *Tufani* ya S.S. Mushi, *Juliasi Kaizari* na *Mabepari Wa Venisi* za J.K Nyerere na *Kinjeketile* ya E. Hussein.

### **2.1.3 Kipindi cha Baada ya Uhuru**

Kabla ya uhuru kulikuwa na waandishi watatu nchini Kenya ambao waliandika tamthilia zilizochapishwa ambao ni Hyslop na wanafunzi wake Kuria na Ngugi. Kuanzia miaka ya sabini, waandishi wengine walichipuka ambao waliandika kazi ambazo ziliangazia uhalisia wa jamii nchini Kenya na nchini Tanzania. Tamthilia katika kipindi hiki zimemulika matatizo ya jamii baada ya ukoloni. Penina Muhando Mlama (1983) katika Wafula (1999) anasema futuhi ziliendelea kuandikwa lakini katika kipindi hiki ziliwasuta Waafrika walioiga mienendo ya wazungu kikasuku. Kulingana na maoni yake Mlama, waandishi nchini Tanzania walianza kufungamanisha tamthilia na mahitaji ya nchi ya Tanzania. Hivyo basi, maudhui yaliyodhihirika katika tamthilia za kipindi hiki ni pamoja na; ukoloni, ukoloni mambo leo, umaskini, elimu, swala la mwanamke na utabaka.

### 2.1.3.1 Miaka ya Sabini hadi Miaka ya Themanini

Mwanyengela Ngali mnamo mwaka 1971, alichapisha mkusanyiko wa michezo mitatu- *Mwana Taabu* na michezo mingine. *Mwana Taabu* ni mchezo unaozungumzia masuala muhimu katika jamii wakati huo. Mchezo huu unamhusu msichana ambaye amelimishwa na wazazi wake kwa taabu wakidhani atawafaa katika maisha yao ya baadaye. Kinyume na matarajio ya wazazi wake, Taabu anaolewa pindi tu baada ya kukamilisha masomo yake na kukatiza mahusiano na wazazi wake. *Kifo cha Penzi* ni mchezo unaochukua mkondo wa melodrama na unamhusu Maryamu mchumbawe Juma ambaye anajiua kwa sababu ya mapenzi yake kwa Juma. *Mwervevu Mjinga* nao ni mchezo unaohusu mwanamume mlevi ambaye anamdhulumu mkewe na kisha kumtaliki lakini pindi tu anapofahamikiwa kuwa mkewe amepata mwanamume mwingine, anataka warudiane. Udhaifu wa michezo ya Ngali ni kuwa, inaishia kwa vifo vya ghafla na hivyo kukosa mantiki (Bertoncini 2009).

Mchezo wa kuigizwa ulioigizwa na wanafunzi wa shule ya upili ya wasichana ya Matuga – *Ng’ombe Akivunjika Mguu* (1975) ni mchezo unaochukuliwa kuwa mchezo bora wa kuigizwa wa wakati huo. Mchezo huu unaafiki methali ya Kiswahili ‘ng’ombe akivunjika mguu hukimbilia zizini’. Mchezo huu unahusu msichana Liza ambaye amepitia masaibu mengi mjini Nairobi na pindi tu anaporejea nyumbani kumwona mamake, mamake anaaga. Hata hivyo Liza ambaye amejengwa kuwa mhusika mkuu wa kike amesawiriwa kuwa muovu. Mandhari ya pwani yametumika na matukio ni ya kuaminika huku sifa ya uigizaji ikijitokeza bayana. Hata hivyo suluhu katika mchezo inafikiwa kwa kasi.

Aidha Farouk Muslim aliandika mchezo – *Mbio za Sakafuni* (1976) unaozungumzia mhusika mkuu wa kike Halima ambaye analazimishwa na wazazi wake kuolewa na Ahmad kwa sababu ya utajiri wake na kisha kushawishiwa atalikiwe na Ahmad na kuolewa na ambaye ni tajiri kuliko Ahmad. Jambo la kusikitisha ni kuwa Halima anabakia bila mume na hivyo kuwalaumu wazazi wake kwa kumpa mawaidha mabaya ya kumpotosha. Mchezo umeendelezwa kwa mfuatano wa matukio. Hata hivyo, katika onyesho la kwanza, kuna mgogoro na wahusika wanaotangulizwa ambao hawana umuhimu wowote katika sehemu za baadaye za mchezo. Aidha hakuna kilele cha mchezo kama anavyoeleza Bertonchini (2009).

Mwaka wa 1980, Said Mzee na Muslim waliandika *Mkuki wa Moto*, mchezo ambao ulishughulikia masuala ya kihistoria ya Kenya tangu 1919 wakati walowezi wazungu walivamia ukikuyuni hadi wakati wa kujinyakulia uhuru. Bertoncini (2009) anadai hii ndiyo tamthilia ya kwanza kuhusu vita vya mau mau.

Waandishi katika kipindi hiki –Jay Kitsao, Zachariah Zani Na Felix Osodo walitaka kuonyesha uhalisia wa kihistoria katika kazi zao lakini walishindwa kuzingatia uhalisia wa maisha katika kuunda maudhui yao. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Mwana Mpotevu* ya Zani, ukarimu unaojengwa ndani ya Hewala babake Mpotevu katu haujashuhudiwa katika mazingira ya Kiafrika ambayo yamejawa na ugandamizwaji wa kisiasa, kiuchumi na hata kiutamaduni pamoja na dhuluma za ukoloni mambo leo katika kizazi cha ubepari. Tamthilia yenyewe ni kielelezo cha ubadhirifu kama anavyosema Mugambi (1982). Maudhui yamejengwa kupitia mhusika mkuu Mpotevu, ambaye ni mwana wa Mzee Hewala, mzee tajiri. Tamthilia hii inlandana na hadithi kwenye Bibilia ya ‘mtoto mpotevu’.

Maudhui makuu katika tamthilia *Mwana Mpotevu* ni tamaa na ukarimu. Tamaa inadhihirishwa na kitendo cha mhusika Mpotevu anayeogopa babake afe kabla hajagawiwa mali. Ukarimu unajitokeza katika kitendo cha Hewala babake Mpotevu kusema Mpotevu afanyiwe karamu arudipo.

Zani ametumia majazi kwa usahihi kujenga maudhui na kwa upande mwingine ametumia methali ambayo haizingatii maudhui. Kwa jumla, Zani hajazingatia uhalisia wa maisha ya jamii katika muktadha wa kihistoria.

Tamthilia ya Jay Kitsao, *Jirani Kanyolewa* (1975) imeangazia mambo mawili; msimamo wa wanaume kuhusu wanawake kwa jumla na jitihada za kutekeleza wajibu kwa kujitolea kama anavyosawiriwa mwalimu wa Chadi.

Babake Chadi na mwenzake Dadazha wanashikilia kuwa mahali pa mwanamke ni jikoni tu na kuwa hakuna maana ya elimu. Kwa upande mwingine mwalimu anafanya juhudi za kuona Chadi amepata elimu kwa vyovyote vile. Kitsao ameangazia maudhui kama vile elimu, tamaa na ubinafsi, umaskini, uonevu wa mwanamke katika jamii, athari za mali katika jamii pamoja na mgongano wa kitamaduni. Mbinu alizotumia kuendeleza tamthilia yake ni pamoja na mfululizo bayana wa kisa chake na utani wa wazee unaodhihirisha msimamo wa dharau na kuwabeza wanawake kwa jumla.

Kwa jumla, tamthilia hii hailandani kihalisia na mandhari ya mazingira yake. Sanaa ya Kitsao inaishia kuidhalilisha jamii kwani maudhui yake hayaonyeshi jamii ambayo ina uwezo wa kujikomboa.



Mchezo wake wa pili –*Mafarakano* (1975), unahusu uchawi. Mchawi katika mchezo huu analazimishwa kuacha uovu wake wa uchawi. Mchezo umeandikwa bora kuliko *Jirani Kanyolewa* lakini suluhu yake inafikiwa pasipo na taharuki yenye motisha.

Kitsao ni mwandishi mtajika katika kipindi hiki na hivyo aliandika tamthilia nyingine nne: *Uasi* (1980), *Tazama Mbele* (1981), *Bibi Arusi* (1983) na *Malimwengu Ulimwenguni* (1983). *Uasi* inahusu wasichana wa kipindi hicho wanaolazimishwa katika ndoa zisizoelekezwa na mapenzi huku ikizungumzia masuala ya ndoa ambapo wasichana wanalaumiwa kwa kutaka kuolewa na mabwanyenye wazee huku wakiwakataa wanaume wa rika lao ambao ni fukara.

Tamthilia ya Osodo, *Hatari kwa Usalama* pia haijazingatia uhalisia wa jamii katika uundaji wake wa maudhui.

Tamthilia za Kitsao, Zani na Osodo zinasawiriwa kama ‘fasihi vimelea’ kama anavyoeleza Mugambi (1982: 168). Maoni ya Mugambi yanatokana na sababu kwamba, kazi hizi ni fasihi ambayo inaonyesha kutoimarika kwa waandishi kisanaa na kiitikadi pamoja na kukosa dhamira elekevu.

Johnson Alex Mwangudza aliandika *Thamani Yangu* (1976) inayohusu mila na tamaduni za katikati ya pwani ya Kenya. Mchezo unamzungumzia Fundi Mganga ambaye anatoa uamuzi kuhusu malezi ya mtoto. Fundi Mganga anaamua mchumba aliyeachwa na baba mtoto apewe mtoto kama njia ya baba mtoto kumlipa mchumba aliyemvunjia uchumba.

Kinyume na waandishi hawa, tumeangazia waandishi wa tamthilia ambazo zinaafiki uhalisia wa kijamii. Tamthilia hizi ni pamoja na; *Mashetani* (1971) ya Ebrahim Hussein, *Mzalendo Kimathi* (1978) ya Ngugi na Micere Mugo, *Mukhwava wa Uhehe* (1979) ya M.M Mulokozi na *Kilio Cha Haki* (1981) ya A. Mazrui. Hussein, Ngugi, Micere Mugo, Mulokozi na Mazrui wanazingatia

uhalisia wa kihistoria. Tamthilia hizi zinadhihirisha mwamko wa kisiasa. Wameonyesha fasihi ya mapambano dhidi ya unyonyaji na ugandamizaji wa mkoloni dhidi ya Mwafrika.

Maudhui makuu katika *Mashetani* ni mtafaruku wa kitabaka chini ya ukoloni mambo leo. Mtafaruku huu unadhihirishwa na wahusika wakuu wawili Juma na Kitaru. Tamthilia hii iliandikwa kutokana na yaliyotokea nchini Tanzania baada ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Tamthilia hii imegawika katika sehemu mbili: sehemu ya kwanza inaeleza juhudi za mkoloni kumtawala Mwafrika kiakili kama inavyojitokeza katika mchezo ndani ya mchezo baina ya Juma na Kitaru juu ya 'mashetani'. Sehemu ya pili inajadili matatizo yanayowakabili Watanzania chini ya ukoloni mambo leo. Sehemu hii inaendelezwa katika akili ya Kitaru ambaye ni kielelezo cha Mwafrika aliyepumbazwa na elimu na athari za mkoloni. Sehemu hii inafafanua migongano ya kitabaka iliyoendelea na inayoendelea baada ya uhuru.

Maudhui yanayoangaziwa ni pamoja na; utabaka, elimu ya kikoloni, ukoloni mambo leo, na ubepari kama mfumo wa kuwanyanyasa wanyonge kiuchumi. Hussein ameoanisha fani zifuatazo katika kuendeleza maudhui; nyimbo za sherehe zilizofuata uhuru, ndoto inayoonyesha ulimwengu ambao Kitaru anaona ni wa tabaka lake na matumizi ya kina ya jazanda- kwa mfano, shetani (mkoloni), binadamu (Mwafrika) na kisu (elimu).

Kwa jumla, matatizo anayoeleza Hussein katika *Mashetani* si yanayowakumba Watanzania pekee bali mataifa ya Afrika Mashariki kwa jumla. Anaeleza jinsi matatizo yalianza wakati wa ukoloni na kuendelea hata baada ya uhuru wa bendera chini ya ukoloni mambo leo. Ujumbe wa Hussein kwa Mwafrika ni kwamba Mwafrika asake nafsi yake pasipo kuzingatia maisha ya Kizungu ambayo hayalingani na hali halisi ya jamii yake.

Ngugi na Micere Mugo katika *Mzalendo Kimathi* (1978), wanadhihirisha mwamko wa kisiasa. Tamthilia hii inaangazia utetezi wa hadhi ya Mau Mau kama vita vya ukombozi vya kitaifa kwa jumla, vita ambavyo bado vinaendelezwa dhidi ya ukoloni mambo leo ambao unawadhulumu wafanyikazi na wakulima wadogo wadogo kiuchumi na kisiasa. Masuala yaliyoangaziwa ni pamoja na uzalendo, ukombozi, ujasiri na usaliti. Tamthilia ya *Mzalendo Kimathi* imetumia mandhari yanayoambatana na uhalisia wa kihistoria wa jamii kwa kumtumia Kimathi kama mhusika pamoja na kuhukumiwa kwake Nyeri.

Tamthilia ya A. Mazrui *Kilio Cha Haki* (1981) inatudokezea mapambano ya wafanyikazi dhidi ya udhalimu wa makaburu uliowakilishwa na Delamon. Tamthilia inaanza kwa hamasa na ghadhabu ya hali ya juu ya wafanyikazi ambao wameamua kupigana dhidi ya kunyanyaswa na ukaburu. Kama anavyoeleza Mugambi (1982: 160), *Kilio Cha Haki* ndiyo tamthilia ya kipekee ya Kiswahili iliyofikia kilele kabisa katika kubainisha hisia za ukombozi wa jamii iliyobanwa katika ulitima. Baadhi ya masuala yanayozungumziwa katika *Kilio cha Haki* ni pamoja na:- ubepari unaoendelezwa na Delamon ambaye ni kaburu mdhalimu, ukabaila, utabaka, ujasiri wa mhusika mkuu wa kike Lanina, Musa na Dewe katika harakati za kupigania haki za wafanyikazi, udhalimu, usaliti, ukombozi – wa wanawake, wa kisiasa na wa kiuchumi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwanamke amesawiriwa kuwa kiumbe anayedhalilishwa.

Tamthilia nyingine katika kipindi hiki ni pamoja na; *Mfalme Juha* (1971) ya Farouk Topan, na tafsiri ya *Mfalme Edipode* ya S.S. Mushi (1971), *Hatia* ya Mlama na *Kifo Barabarani* ya Ngahyoma zote za mwaka wa 1972, *Aliyeonja Pepo* ya Topan na *Tambueni Haki Zetu* ya Mlama zilizochapishwa mwaka wa 1973, *Heshima Yangu* ya Mlama na A.S. Yahya akatafsiri *Masaibu ya Ndugu Jero* mwaka wa 1974. Mwaka uliofuata, tamthilia zifuatazo zilichapishwa; *Pambo* na *Kortini Mtu Huyu* za Mlama, na *Mwanzo wa Tufani* ya Kulikoyela Kahigi na Ngerema. Mwaka

wa 1976, Hussein alichapisha *Jogoo Kijijini* na *Ngao Ya Jadi*. Mnamo mwaka wa 1977, *Machozi ya Mwanamke* iliandikwa na Ibrahim Ngozi. Mwaka wa 1978, Katalambulla alichapisha tamthilia mbili, *Imani Yangu* na *Unono wa Mizani*. M.M.Mulokozi alichapisha mchezo wa kuigizwa *Mukwava wa Uhehe* mwaka wa 1979 pamoja na tafsiri ya Christon Mwakasaka.

Mwaka wa 1980 kulikuwa na tamthilia nyingi zilizochapishwa kama vile *Maalim na Hukoo Darisalama* ya L.M. Muba, *Dhamana ya Mabatiniya* G.Z. Kaduma na *Giza Limeingia* ya E. Mbogo. Mwaka wa 1981 Mbogo alichapisha *Tone la Mwisho* na *Watoto Wetu*. Mwaka wa 1982, N. Balisidya na Mlama waliandika *Harakati za Ukombozi* na Mlama akaandika *Nguzo Mama*, huku Chacha N. Chacha akiandika *Mke Mwenza* naye C. Kibugi akatafsiri *Nitaolewa Nikipenda*. Mwaka wa 1983, David Mulwa na A.S. Yahya wakaandika mchezo wa kuigiza wa *Buriani* na tamthilia ya *Uchafu* ikaandikwa na V.A. Malima. Mulwa na Yahya waliandika *Ukame* (1984), Ongeti Khaemba akaandika *Visiki* (1984) naye S.A. Omar akachapisha *Maisha Subira* (1985). *Zinduko* ya S. Ryanga na *Marejeo* ya Chacha zilichapishwa mwaka wa 1986. Tamthilia zilizofuata ni, *Wingu Jeusi*(1987) tamthilia ya Chacha na *Mama Ee* (1987) ya Ari Katini Mwachofi, *Kwenye Ukingo Wa Thim* (1988) ya Hussein, *Mkimbizi* (1988) ya Mulwa na Yahya na *Ngoma Ya Ng'wanamalundi* (1988) Ya E. Mbogo.

Tamthilia katika miaka ya sabini hadi miaka ya themanini zimeonyesha maendeleo makubwa. Zinatubainishia ujasiri wa waandishi ambao unatudhihirishia ujasiri wa jamii kwa jumla. Jamii imezinduka kimawazo na hivyo inaelewa bayana kuhusu dhuluma na ugandamizwaji waliopitia wakati wa ukoloni na hivyo wameamua kupigana na udhalimu huu. Tamthilia katika kipindi hiki hazionyeshi kudhalilishwa kwa Mwafrika wala utamaduni wake bali zinaonyesha kupigania haki za Mwafrika kupitia mapinduzi yanayoongozwa na Waafrika jasiri kama vile Kimathi na Lanina. Kipindi hiki kinadhihirisha kilele cha mwamko wa kisiasa, kilele cha kuzinduka na kilele cha

ujasiri ambao msingi na mhimili wake ni katika jamii. Miongoni mwa tamthilia zilizoandikwa katika kipindi hiki zinagusia masuala ya mapenzi pia. Mtindo unaotumiwa na waandishi katika kipindi hiki unaonyesha ukomavu mzuri unaowezesha dhamira na maudhui yajitokeze kwa nguvu na mnato wa kuridhisha.

### **2.1.3.2 Miaka ya Tisini hadi Sasa**

Tamthilia za kutoka miaka ya tisini hadi sasa zinachukua mkondo mpya tofauti na miegemeo ya tamthilia za hapo awali ya ujumisia na uhalisia wa kihistoria. Tamthilia katika kipindi hiki zinachukua mwelekeo wa nadharia ya usasa na usasa leo. Hivyo basi, tamthilia za kipindi hiki zimekitwa katika uhalisiajabu uliochanganywa na uhalisi uliopo katika jamii ya kisasa. Kwa mfano, tamthilia ya Wamitila, *Wingu la Kupita* (1999) imejengwa katika misingi ya fasihi ya kimajaribio.

Maudhui katika tamthilia za kipindi hiki, yanalenga changamoto zilizopo katika jamii kama vile; ukosefu wa kazi, umaskini, uongozi mbaya, ugonjwa wa ukimwi na matatizo katika asasi ya ndoa. Wahusika katika tamthilia za kisasa wana mchocheo wa kutaka kujua ukweli na hivyo kuzuka kwa wahusika jasiri wa kimapinduzi. Masuala ya teknolojia na lugha ya utandaridhi yanajitokeza katika tamthilia hizi. Kwa jumla, tamthilia katika kipindi hiki zinaangazia masuala yanayoizunguka jamii ya kisasa.

Mifano ya tamthilia katika kipindi hiki ni kama vile *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995) za S.A. Mohammed, *Mawimbi* na *Kiumbe* (1991) za Ernest Eshamwata, Chacha N. Chacha-*Hukumu* (1992), *Mkutano wa Pili wa Ndege* (1992) ya Amandi na Lihamba, *Morani* (1993) na *Sundiata* (1994) za E. Mbogo, *Kaptula La Marx* (1996) ya Euphrase Kezilahabi na *Unga* (1996) ya Ali

Shaaban Juma, *Mnara Wawaka Moto* (1998) ya Rocha Chimerah , *Wingu La Kupita* (1999) ya K.W. Wamitila na *Manamba* (1999) ya Ongeti Khaemba.

Tamthilia za kuanzia mwaka wa 2000 ni pamoja na:- *Upotovu* (2000) ya Njiru Kimunyi, *Siri* (2000) ya Farouk Topan, *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) ya S.A Mohamed , tamthilia za Kithaka wa Mberia *Natala* (1997), *Kifo Kisimani* (2004) na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (2004), *Mazonge* (2004) ya Ali Mwalim Rashid, *Sudana* (2005) ya A. Mazrui, *Pango* (2004) na *Sumu ya Bafe* (2006) za K.W. Wamitila, *Zilizala* (2006) ya Kimani Njogu, *Migogoro* (2006) ya Mwenda Mbatiah, *Chamchela* (2007), *Mstahiki Meya* (2009) na *Kijiba cha Moyo* (2012) za Timothy Arege.

*Natala* (1997) ya Kithaka wa Mberia, ni tamthilia inayoonyesha jinsi mwanamke alivyokumbwa na matatizo katika jamii inayotawaliwa na mfumo wa kuumeni wa ubabedume. Matatizo anayoyapitia mhusika mkuu Natala, ni kibainisho cha jinsi jamii nzima ilivyokumbwa na matatizo hasa ya kijamii. Natala baada ya kinachosemekana kuwa ‘kifo’ cha mumewe Tango, ukoo wa mumewe wanataka arithiwe na Wakene nduguye mume wake na anapokataa wanaamua kumnyang’anya watoto, hati ya shamba na nyumba. Natala anapigania haki yake mpaka Tango anaporejea na kutoa suluhu ya matatizo yake ya ndoa.

Maudhui yanayoangaziwa katika *Natala* ni uonevu wa mwanamke katika jamii, ukatili, umaskini, ufisadi, mila na tamaduni zilizopitwa na wakati, unyanyaswaji wa raia na serikali, umbea na masuala-ibuka katika jamii kama vile ugonjwa wa ukimwi. Mandhari katika tamthilia hii yanaafiki hali halisi ya maisha ya siku hizi.

Kithaka wa Mberia aidha ametuchorea uongozi mbaya katika jamii kupitia tamthilia ya *Kifo Kisimani* (2004). Amebuni jamii ya Wanabutangi walionyanyaswa chini ya uongozi mbaya wa

Mtemi Bokono. Mtemi Bokono amejawa na ufiada wa kujinyakulia mali pasipo kujali maslahi ya Wanabutangiri. Anawanyanya watu wake kwa kuwakataza kuchota maji katika Kisima Cha Butangi na kiwanja cha michezo cha watoto kinanyakuliwa chini ya uongozi wake na bado anaendelea kuusifu uongozi wake. Ni katika kuukomesha uongozi huu mbaya, kunapotokea kijana aliyesoma Mwelusi ambaye ana ari ya kuwaongoza wenzake katika mgomo wa kimapinduzi. Tamthilia inaishia kwa kushindwa kwa Mtemi Bokono pale anatiwa kizuizini hata kama Mwelusi ameuawa.

Tamthilia ya S.A Mohamed *Amezidi* inachunguza athari za misaada ya kigeni kwa uchumi wa mataifa machanga. Badala ya misaada kuleta mafanikio na maendeleo, inazidisha umaskini na uhitaji kama anavyosema R.M. Wafula (1999).

*Sumu ya Bafe* (2006) ya K.W. Wamitila ni tamthilia iliyojengwa kijazanda. Wamitila ametumia kichwa cha tamthilia kijazanda ambapo 'sumu' inarejelea athari za ukoloni na 'bafe' kuwa Mkoloni. Tamthilia hii inaonyesha kuwa, hata kama jamii imejinyakulia uhuru, bado kuna athari za ukoloni katika jamii. Ni katika kutumia jazanda ya 'sumu ya bafe' tunapopata maudhui makuu ya ukoloni mambo leo. Maudhui mengine katika sumu ya bafe ni pamoja na uhuru wa bendera kwa wanajamii wa Dahimu chini ya uongozi wa Mapepe, elimu kama mbinu ya ukombozi kwa kizazi kipya pamoja na matumaini ya kizazi kipya.

Wamitila ametumia sitiari (jazanda) kwa kina katika ujenzi wa maudhui. Mbinu nyingine alizoitumia ni pamoja na chuku, matumizi ya nyimbo za kuusifu uongozi mbaya wa Mapepe na nyimbo za kumwondoa Mapepe mamlakani, takriri na taswira. Mandhari yanaoana vizuri na maudhui.

Timothy Arege katika *Mstahiki Meya* (2009), anatudokezea matumizi mabaya ya mamlaka yaliyojengwa kupitia mhusika mkuu Meya (Bwana Sosi). Meya ni mnaofiki anayejilimbikizia mali pamoja na marafiki zake huku anawanyanyasa watu wa eneo lake na kudharau matibabu na madaktari wa eneo lake akisifu matibabu ya ng'ambo. Masuala yanayoangaziwa katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni pamoja na:- ukoloni mambo leo, ufasidi wa viongozi, unafiki, ushauri mbaya kwa viongozi pamoja na utabaka wa kiuchumi na kisiasa.

Waandishi katika kipindi hiki wamesawiri elimu kama njia ya kipekee ya kujiepusha na uongozi mbaya na kujikomboa katika misingi ya kisiasa, kiuchumi na kimawazo. Aidha wamefanikiwa kumjenga mwanamke ambaye ana uwezo sawa na mwanamume katika misingi ya kisiasa kiuchumi na kielimu kama vile Natala katika *Natala*.

## **2.2 Muhtasari wa *Natala***

*Natala* (1997) ni tamthilia ya kwanza ya Kithaka wa Mberia. Anwani ya tamthilia ni jina la mhusika mkuu wa kike Natala ambaye anapigana na mila na desturi zilizopitwa na wakati za ukoo wa mumewe. Baada ya kusemekana Tango mumewe 'ameaga dunia', Wakene kakake Tango anataka kumrithi Natala na Natala anapomkataa Wakene anaamua kumnyang'anya mali yake yote pamoja na watoto. Hata hivyo, Tango anarudi kileleni mwa matukio na kutoa suluhu kuhusu maisha ya Natala

*Natala* imegawika katika maonyesho matano. Onyesho la kwanza linaanza sebuleni mwa Natala Tango na Tango Mwina ambapo Tango hayupo kwani ameenda kufanya kazi Ruma mbali na nyumbani na Natala yu nyumbani akishughulikia kunga za nyumbani. Akiwa pale nyumbani baada ya kuondoka mumewe, Natala anakumbana na matatizo mengi. Tila mkewe Wakene



anapokuja kuomba chumvi anamdharau Natala kwa kumwona kama mwanamke asiye na sauti katika familia kama alivyo mwanamume. Natala anapomfukuza kwake baada ya kuzua ugomvi, Tila anakatalia huku akimwambia yuko kwa Tango na wala si kwa Natala.

Baada ya kilichochukuliwa kuwa 'kifo' cha Tango, Wakene nduguye Tango anataka kumrithi Natala kwa kuzingatia mila na desturi za ukoo wake ili aendeleze familia ya ndugu yake. Wakene hivyo basi, anamchukulia Natala kama kifaa cha kurithiwa na wala si kama binadamu aliye na uwezo wa kujiamulia atakalo. Wakene ametawaliwa na kasumba ya ubabedume na hivyo kumwona Natala kama kiumbe dhaifu asiye na uwezo alio nao mwanamume kama yeye. Ukoo wa Tango ambao ni pamoja na Mama Lime na Mzee Palipali wanamuunga mkono Wakene kumrithi Natala. Mama Lime badala ya kupigania haki za mwanamke mwenzake, ndiye anayetumiwa na wanakijiji kumshawishi Natala kuitikia mwito wa wanakijiji wa kushirikiana na Wakene katika asasi ya ndoa. Mama Lime anatumiwa kama sauti ya ukoo wake na mshawishi wa Natala ili akubali kuolewa na Wakene kama mke wa pili. Tila anapofahamikiwa kuwa, Wakene mumewe anataka kumrithi Natala, anamfokea Natala kwa matusi na mabezo. Hata hivyo, Natala anajiamini kuwa mwanamke aliye na uwezo sawa na mwanamume na hivyo anakataa katu kurithiwa wala kusaidiwa kulea watoto wake. Anasimama kidete kutetea haki yake kama mwanamke na jinsia ya kike.

Mbali na matatizo ya kifamilia anayokumbana nayo baada ya 'kifo' cha mumewe, Natala anakumbana na matatizo chungu nzima kutoka kwa wafanyi kazi wa umma. Chifu anataka hongo ya kimapenzi na fedha ili amhudumie katika kumpa kibali cha kumzika mumewe. Mtunza jengo la ufuo aidha anamtaka Natala kutoa hongo ya fedha na ya mapenzi ili ampe Natala mwili wa mumewe aende kuuzika. Vilevile, polisi barabarani, wakati wa kurejesha mwili wa Tango nyumbani kwa mazishi, aidha wanataka hongo. Hata hivyo, uwajibikaji wa Natala haumruhusu

kutoa hongo yoyote- fedha au mapenzi kwa kuwaeleza bayana kuwa, wao ni wafanyikazi wanaolipwa na serikali ili kuhudumia umma. Aidha anajiheshimu kama binadamu na hivyo, kuwaambia wazi wanaotaka mapenzi naye kuwa yeye si mlango wa jengo la umma wa kuguswa na kila mtu (uk 22) kama anavyomwambia mtunza jengo la ufuo.

*Natala* inafikia tamati katika onyesho la tano palepale sebuleni, nyumbani mwa Natala ambapo Wakene akiungwa mkono na watu wa ukoo wake anamnyang'anya Natala shati ya shamba akiwa na lengo la kumtimua nyumbani kwake. Ni katika harakati hizi za Wakene za kung'ang'ania cheti na Natala, anaporejea Tango ambaye anatokea kwa ghafla na kuzua hali ya hofu kwa wote waliokuwa ndani sebuleni. Tango anapofika kila mtu anamchukulia kuwa ni mzuka kwani iliainika katika familia yake na kijiji kizima kuwa Tango amefariki na ameshazikwa. Wakene anapomwona Tango anashikwa na wasiwasi na kumwachilia Natala huku Natala naye akiangusha hati ya shamba na kujitetea mbele ya mumewe kuwa alikuwa anatetea haki yake na ya watoto wake. Natala anamweleza Tango mumewe kisa chote kuhusu walivyofahamishwa kuwa Tango amekufa na jinsi walivyomzika. Kwa upande mwingine, Tango naye akaeleza jinsi mambo yalivyomwendea. Alieleza alivyovamiwa na wezi na kunyang'anywa mavazi na kitambulisho na baadaye akashikwa katika msako wa polisi; na kwa kukosa hongo, akabandikwa makosa ya uongo ya kulewa na kuzurura akiwa na lengo la kufanya maovu na kufungwa jela. Natala na Tango wanapoelewa mkondo wa matukio ya awali wanafurahiana kuwa pamoja tena huku Natala akimchukulia Tango kama mwokozi wa maisha yake kutoka 'zimwi' la utamaduni na mfumo wa ki- ubabedume unaotawala jamii yake.

### **2.3 Hitimisho**

Katika sura hii, tumejadili historia ya tamthilia ya Kiswahili huku tukionyesha maendeleo yake kiwakati, kimtindo na kimaudhui kwa kijumla. Hata hivyo, ni vigumu sana kutaja tamthilia zote za Kiswahili zilizoandikwa katika vipindi hivi hasa zilizoandikwa nje ya nchi za Afrika Mashariki. Aidha tumeangazia muhtasari wa tamthilia ya *Natala* (1997).

## SURA YA TATU

### WAHUSIKA NA UJENZI NA UENDELEZAJI WA MAUDHUI

#### 3.0 Utangulizi

Wahusika ni viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi ili wawe sauti yake katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Wahusika katika kazi ya fasihi wanaweza kuwa watu, wanyama, wadudu, mimea, miungu, mazimwi, vivuli vya mawazoni kama vile viumbe ambavyo ni nusu watu na viumbe visivyo hai kama vile milima na mawe. Hivi karibuni kutokana na ubunifu wa kisayansi, kumetokea wahusika ambao ni vibonzo na maroboti.

Hali kadhalika, wahusika katika tamthilia aghalabu huwa watu na hivyo huwa na sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayosema na yale wanayotenda au yale yanayosemwa na msimulizi au wahusika wengine; hali inayodhihirika katika *Natala*. Mawazo haya yanatokana na wazo la Forster (1949:43) kuwa,

Wahusika katika fasihi aghalabu

huwa Watu kwani, hata kama wanyama

wametangulizwa kama wahusika, hawajafaulu kwa

sababu,saikolojia yao haijulikaniwazi na binadamu. (Tafsiri yetu).

Wahusika huwa ni vielelezo vya watu wanaopatikana katika ulimwengu halisi ingawa wataalamu wa fasihi wanakubaliana kuwa, si lazima sifa zote zifungamane moja kwa moja na sifa za wanadamu (Wamitila 2008).

Wahusika wa kazi za kifasihi ikiwemo tamthilia, huwa wazuri au waovu kama walivyo watu halisi katika jamii. Uovu au uzuri wa wahusika hutegemea uamuzi wa kidhamira wa mwandishi kwani mwandishi huwatumia wahusika kama njia ya kupitisha ujumbe wake kwa hadhira kama ilivyo katika *Natala*.

### **3.1 Ubainishaji wa wahusika**

Kimsingi wahusika katika tamthilia huainishwa kama wahusika wakuu au wahusika wadogo kutegemea wadhifa wao katika kazi husika. Hata hivyo, sifa zifuatazo ni muhimu katika uchunguzi wa wahusika katika *Natala*.

#### **3.1.1 Mhusika na nafasi / majukumu**

Wahusika katika *Natala* wamegawika katika vikundi viwili vikuu kulingana na nafasi au majukumu aliyowapa mwandishi. Kuna wahusika wakuu na wahusika wadogo. Wahusika wakuu katika tamthilia hupatikana kutoka mwanzo hadi mwisho wa tamthilia. Wahusika hawa huwa wenye ukadiri mpana na wenye uchangamano wa sifa na aghalabu hukua kadiri tamthilia inayovyokunjuka (Wamitila 2008). Mhusika mkuu Natala ametangulizwa tangu mwanzo wa tamthilia na kuendelezwa hadi mwisho huku matukio na masuala muhimu ya kimzingira yeye. Ameumbwa na mwandishi kuwa shujaa, jasiri, mtetezi wa haki za mwanamke na mpevu wa akili, sifa ambazo zinatambulisha uchangamano wake. Wahusika wakuu huchukua nafasi muhimu katika uendelezaji wa tamthilia na hivyo, maudhui makuu huwazunguka wao; sifa anayoakisi Natala. Ni wahusika ambao hujitokeza mara kadha na hivyo, kuwa na upana wanapolinganishwa

na wahusika wadogo. Ni wahusika ambao wamejengeka kikamilifu na ukuaji wao ni wa kina (Rimmon-Kenan 2002). Kwa mfano, Natala amesawiriwa kikamilifu kwa kuhusishwa katika masuala ya kijamii kiuhalisia. Ameonyeshwa kuwa ni mke, mama, mwanakijiji na mwanajamii aliyekumbwa na matatizo yanayowakumba wanajamii wengine kama vile kufiwa na mumewe. Maisha ya Natala yanashabihiana na maisha yakinifu ya mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika. Aidha msimamo wake wa kutetea haki za mwanamke katika jamii umejengwa kwa kina.

Wahusika wadogo hupatikana katika tamthilia na hujengwa kwa hulka moja na hivyo, kuwa wahusika wenye ukadiri finyu. Kutokana na ukadiri finyu wao, hawakuzwi na hivyo, huelezwa kwa maneno machache na hivyo, huwa na sifa chache. Katika *Natala* wahusika wadogo ni pamoja na, Tango, Mzee Balu, Bala, Mama Lime, Tila, Wakene, Mzee Palipali, Bwanu, Alika, Mhudumu katika jengo la ufuo na polisi. Wahusika hawa wametumiwa katika *Natala* kumjenga na kumkamilisha mhusika mkuu Natala huku wakiendeleza na kuchangia ujenzi na uendelezaji wa maudhui.

### **3.1.2 Umakundi wa Wahusika**

Wahusika katika tamthilia wanaweza kujumlishwa katika makundi ya kijamii kama vile marafiki, maadui, wanaomuunga nguli mkono au wakinzani wake. *Natala* imehusisha kundi la watoto linalowakilishwa na Bwanu na Alika; kundi la watu wazima, wanaume kwa wanawake, wanaomuunga nguli mkono na wakinzani wake. Watu wa ukoo wa Tango ambao ni Wakene, Mama Lime, Mzee Palipali wakinzani wa mhusika mkuu Natala. Mberia ametumia umakundi wa wahusika kuibua maudhui kwani umakundi huo unadhihirisha misimamo na mielekeo yao. Kwa mfano, kundi la ukinzani katika *Natala* ni kundi ambalo linashikilia na kuendeleza mila na desturi

potovu za jamii na ambazo zimepitwa na wakati. Wanapendekeza Natala arithiwe na Wakene nduguye Tango baada ya kilichosemekana kuwa ‘kifo’ cha Tango, mumewe Natala.

### **3.1.3 Ulinganuzi wa Wahusika**

Ulinganuzi wa wahusika ni mbinu ya kumchunguza mhusika kwa kumlinganua na mwingine. Sifa inayojitokeza katika ulinganuzi huu ni kwamba, mhusika mmoja ni kinyume cha mhusika mwingine. Aghalabu sifa ya ulinganuzi hutokea baina ya nguli na mkinzani wake. Kwa mfano, katika *Natala*, Mama Lime anaungana na wanaume kumdhulumu mwanamke mwenzake Natala (nguli). Badala ya Mama Lime kumuunga mkono Natala katika kupinga kurithiwa na Wakene, tunamwona akitumwa na ukoo wa Tango kumshawishi Natala akubali kurithiwa (uk 36). Hivyo basi, wazo lake linakinzana na la Natala ambaye kamwe, hataki kurithiwa. Tukio hili linadhihirisha msimamo thabiti alio nao Natala kuhusu heshima na haki yake kama mwanamke.

Mberia ametumia ulinganuzi huu masuala yanayoendelezwa na mhusika mkuu Natala, lugha anayotumia, msimamo na mwelekeo wake kwa kumlinganua na Mama Lime. Ametumia ulinganuzi wa wahusika kama mbinu muhimu katika ukuzaji wa wahusika na uendelezaji wa maudhui. Amefanya hivi kwa kujenga sifa za mhusika mmoja huku akiangazia sifa kinyume za mhusika mwingine.

### **3.2 Wahusika na Ujenzi wa Maudhui**

Katika *Natala*, mwandishi amewasawiri wahusika kwa njia tofautitofauti kwa lengo la kufanikisha maudhui yake. Amewaumba wahusika wa kike pamoja na wa kiume ambao amewapa

majukumu tofautitofauti kulingana na wadhifa aliowapa katika tamthilia hii. Mwandishi amemuunba mhusika mkuu wa kike kama anavyopendekeza Momanyi (2001) kuwa, waandishi wanapaswa wawaumbe wahusika wa kike ambao ni wahusika wakuu katika kazi za fasihi tofauti na ilivyozoeleka kuwa wahusika wakuu katika kazi nyingi za fasihi ni wanaume. Hivyo basi *Natala* ndiye mhusika mkuu katika tamthilia hii na ambaye anasaidiwa na wahusika wengine wajenzi. Mberia kama waandishi wengine wa tamthilia, hana uhuru wa kueleza fikra na hisia za wahusika wake kama ilivyo kwa mwanariwaya. Mazungumzo na vitendo vya wahusika ndivyo vinavyotupatia vuguvugu la hisia na fikra za wahusika wenyewe. Hivyo basi, wahusika katika *Natala* kupitia hulka zao, mielekeo yao, maneno yao, usawiri wao, majukumu pamoja na nafasi walizopewa na mwandishi wamechangia pakubwa ujenzi na uendelezaji wa maudhui. Kila mhusika amechangia maudhui tofauti kwa njia tofauti na mwingine.

### **3.2.1 Natala kama kielelezo cha utetezi wa haki na utambulisho wa mwanamke**

*Natala* ni mwanamke wa umri wa makamo na ambaye ndiye mhusika mkuu katika *Natala*. Ni mkewe Tango Mwina na mamake Alika na Bwanu. Ni mkaza mwana wa Mzee Balu na ni shemijiye Wakene.

*Natala* ameshikilia wadhifa mkuu katika kujenga, kukuza na kuendeleza tamthilia yenyewe. Amechorwa kama sauti ya utetezi wa mwanamke na hasa kwa lengo la kukomboa kutoka jamii ya ki-ubabedume. *Natala* amesawiriwa kama kielelezo cha mwanamke halisi katika jamii inayomwona mwanamke kama chombo. Maudhui makuu katika *Natala* na ambayo yanahusu matatizo ambayo mwanamke anakabiliana nayo katika jamii yanamzunguka *Natala* na hivyo, kuifanya tamthilia yenyewe kuwa tamthilia tatizo kama anavyoeleza Mbatiah (2001:78).



Tamthilia tatizo ni aina ya tamthilia ambayo inajenga dhamira yake juu ya tatizo mahsusi la kijamii. Dhamira hiyo hujengwa kupitia mhusika mkuu ambaye anakabiliana na utata ambao ni kielelezo cha mazingira yake ya kijamii. Dhamira ya tamthilia ya *Natala* imejengwa kupitia Natala ambaye anakabiliana na tatizo la kudunishwa na kudhalilishwa mwanamke ambalo ni kielelezo cha mazingira yake ya kijamii. Tatizo la kudunishwa kwa mwanamke ambalo Natala anakabiliana nalo ni kiwakilishi cha hali ya mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika.

Natala kama mhusika mkuu katika *Natala* amechangia katika uendelezaji na ujenzi wa maudhui tofauti.

### **Utetezi wa haki za mwanamke**

Natala ni mtetezi wa haki za mwanamke na hivyo, amechorwa na mwandishi kama mhusika wa kike ambaye anapinga udunishwaji na jamii nzima ya wanawake kwa wanaume ambao wametawaliwa na fikra za ki-ubabedume. Mwanamke katika hali halisi ya kijamii, amedhalilishwa na utamaduni na kuwekwa katika nafasi ya pili baada ya mwanamume. Kwa hivyo, kudunishwa kwa Natala kunatokana na mtazamo wa kijamii kuwa mwanamke hana haki sawa na mwanamume.

Mchango wa Natala katika kujenga na kuendeleza maudhui ya udhalilishwaji wa mwanamke kunajitokeza kwa njia kinzani. Anakinzana na wenzake katika tamthilia wanaoendeleza kudunishwa kwa mwanamke huku yeye akijitokeza kwa njia ya kuupinga udunishwaji huo. Kinyume na uchukulizi wa jamii wa kumdunisha mwanamke, Natala anasimama kidete pasipo kutetereshwa na lolote wala yeyote kutokana na sifa ya ujasiri uliojengeka katika hulka yake kutetea haki na nafasi yake kama mwanamke na jinsia ya kike kwa ujumla. Anakataa katakata kudhulumiwa hasa kwa misingi ya kuwa mwanamke.

Kwanza, Natala anapomfukuza Tila kutoka nyumbani kwake anapokwenda kuomba chumvi, Tila anang'ang'ania kuwa yuko kwa Tango kaka ya mumewe bali si kwa Natala. Natala anamwambia dhahiri atoke kwake. Hivyo basi, Natala hakubali kamwe kudunishwa na kudharauliwa na Tila kwa kukatalia kwake kwa madai kuwa kwa Natala ni kwa kakake Tango (uk. 5). Anajitambulisha kama binadamu anayestahili hashima na maisha kama mwanadamu yeyote yule.

Aidha Mama Lime anapokwenda kwa Natala kwa lengo la kumpasha matakwa ya wanakijiji, anadai kuwa Natala ni mwanamke na hawezi kujikimu hasa wakati huo mumewe anaposemekana ameaga dunia. Anamwambia Natala kuwa njia nzuri ya kuwalea watoto bila shida ni kwa kushirikiana na mwanamume ili apate usaidizi (uk. 36). Natala anatupilia mbali wazo la Mama Lime kwa kumjuza kuwa atawalea watoto wake kwa kutumia fahamu zake (uk. 36). Mwanamke wa Kiafrika, akiwemo Mama Lime, anafaa aelewe kuwa, kanuni za kitamaduni na ugawaji wa majukumu kwa misingi ya jinsia ndiyo mambo yanayomletea mwanamke dhiki anazokumbana nazo na kwamba, hali hii inaweza kubadilishwa na wanawake wenyewe kwa kujichukulia kuwa wao ni binadamu sawa na wanaume kwa kila njia na kudai haki na heshima wanazostahili. Hivyo basi, Natala anapinga wazo la kudunishwa mwanamke kwa kusimamia ukweli kuwa, ana akili sawa na za mwanamume na ndiyo sababu anasema atatunza familia yake kwa kutumia fahamu zake pasipo kushirikiana na mwanamume mwingine baada ya kifo cha mume wake. Kwa kufanya hivyo, Natala anamzindua kimawazo mwanamke wa Kiafrika kwa kuonyesha kuwa ana uwezo wa kujitegemea na kuupinga utegemezi wa mwanamume ambao unajitokeza kuwa ni udhalimu dhidi yake na sababu ya kumdunisha na kumnyima uhuru wake.

Katika mchezo ndani ya mchezo baina ya Natala na Bala kuhusu waliyoyashuhudia katika jengo la ufuo, Natala anamkabili mtunza jengo la ufuo kwa kumwambia waziwazi kuwa mwanamke si mpumbavu wala gogo la mgomba. Zaidi ya hayo, ni binadamu. Huu ni wakati ambapo mhudumu

katika jengo la ufuo anaiambia maiti kuwa imelala ‘kipumbavu kama mwanamke’. Natala anamjibu kwa ukakamavu kuwa, “*Mwanamke si mpumbavu wala si gogo la mgomba,.....mwanamke ni binadamu*”. [uk. 19]

Natala anapinga kudunishwa kwa mwanamke na kuonyesha kuwa mwanamke ana haki sawa na mwanamume katika kumiliki mali. Suala hili linadhihirishwa na vitendo vya Natala vya kukataa kunyang’anya cheti cha shamba, nyumba na watoto (uk. 54). Anakabiliana na Wakene vikali anapojaribu kumnyang’anya cheti cha shamba. Anamwambia hawezi kumnyang’anya hata kama yeye ni mwanamke.

*Kazi bure hauondoki hapa na hicho*

*cheti.... Bila shaka mimi ni mwanamke.*

*Lakini utagundua kuwa sio kila mwanamke*

*hutetemeka mbele ya wanaume.* [uk. 54]

Kutokana na vitendo vya kujaribu kumdunisha mwanamke kama inavyodhihirika katika *Natala*, ni dhahiri kuwa, kudunishwa kwa mwanamke hakutokani na udhaifu wa kimaumbile bali jinsi kiumbe huyu anavyochukuliwa kuwa duni katika asasi za utamaduni kupitia mfumo wa ki-ubabedume kama anavyodai Momanyi (2001:54). Mfumo wa kuumeni ni mfumo wa kijamii ambao unamtweza mwanamke na kumtwaza mwanamume.

## **Ufisadi**

Natala hajashiriki katika ufisadi kwa njia ya moja kwa moja lakini ni mhusika ambaye amechangia pakubwa katika kudhihirisha maudhui haya. Sababu ni kwamba, wafisadi wengi katika *Natala* wamemtumia Natala katika kuibua vitendo vya ufisadi japo yeye mwenyewe hashiriki katika ufisadi. Kwa mfano, anapokwenda kuchukua maiti inayodhaniwa kuwa ya Tango akiwa na Bala, wanaitishwa hongo na polisi barabarani kama anavyoeleza Bala uk.16:

*“...isitoshe, tulisimamishwa mara kadha na*

*polisi. Wakiona gari barabarani akili zao hupiga*

*neni moja tu: “kitoweo!” mmoja wao hata alituambia*

*kwamba mtu mmoja akifariki haimaanishi wanaobaki duniani wafe njaa.”*

Hivyo basi, Natala anachangia kuyaangazia maudhui ya kupinga ufisadi kwani anahusishwa katika mazungumzo yanayoibua vitendo vya ufisadi.

Hata kama Natala anahusishwa katika kuviangazia vitendo vya ufisadi, anapinga vikali ufisadi wenyewe. Mhudumu katika jengo la ufuo alimtaka Natala atoe hongo ili apewe ‘mwili wa mumewe’ Tango jambo ambalo analikataa katakata kwa kumwambia mtunza jengo la ufuo kwamba, analipwa mshahara kila mwezi kwa hivyo, afanye kazi ambayo analipwa kuifanya

(uk. 22).

Wakati wa ‘mazishi’ ya Tango, Chifu anataka hongo ili atoe kibali cha kujumuika. Natala alipinga wazo la Chifu vikali kwa kumweleza bayana ya kwamba yeye ni adui mkubwa wa utoaji hongo kama inavyodhihirishwa na maneno yake kwa Chifu:

*Bwana Chifu, mimi ni adui mkubwa wa mambo hayo*

*(hongo). Moyo wangu unayapinga sana. [uk 32].*

Anaeleza wazi kwamba, Chifu analipwa mshahara kila mwezi na hivyo hastahili kupewa hongo ndipo atoe kibali cha mazishi (uk. 32).

Natala kama mhusika, amechangia katika kuangazia ufisadi huu. La muhimu ni kwamba, Natala hajashiriki ufisadi bali anajitokeza kama mhusika anayepinga ufisadi kwa kukataa katu kutoa hongo ndipo ahudumiwe na wafanyikazi ambao wanalipwa mshahara kwa kazi hizo. Aidha, anawakataza wengine kushiriki ufisadi kama anavyomkanya Mzee Balu asitoe hongo kwa chifu kwa kumwambia asikubali “kuutilia ugonjwa wa ufisadi mbolea” (uk. 33).

## **Umaskini**

Maudhui ya umaskini umekithiri katika *Natala* kama ilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika. Natala anachangia ujenzi wa maudhui ya umaskini katika *Natala* kwani yeye mwenyewe ameathiriwa na umaskini. Katika onyesho la kwanza, tunamwona Natala akipiga nguo pasi akiwa amewekelea pasi juu ya kikombe kitendo ambacho kinaakisi uchochole usiomwezesha kununua vifaa vya kisasa vya kupigia nguo pasi. Aidha chifu anapomhitaji atoe hongo, Natala anapinga wazo hilo (uk 32).

*Mzee Balu: Una chochote mfukoni tumpe?*

*Natala: Sina.....[uk. 32].*

Natala vilevile anahusishwa katika kudhihirisha maudhui ya umaskini. Kwa mfano, Tila anamwomba Natala vitu vya kawaida sana kama chumvi, sukari na mafuta ya taa katika kipindi cha wiki moja (uk. 3-4). Kwa hivyo, umaskini wa Tila unadhihirishwa kupitia Natala kwani ndiye anayeombwa vidhaa hizo.

### **Desturi na mila zilizopitwa na wakati**

Katika *Natala*, desturi na mila zilizopitwa na wakati na ambazo zinamkandamiza mwanamke ni pamoja na urithi wa wanawake. Mhudumu katika jengo la ufuo ndiye anayeshiriki urithi wa mwanamke. Urithi wake unajulikana katika tamthilia kupitia mazungumzo baina yake na Natala. Hivyo basi, Natala anachangia katika kuibua maudhui haya. Hata hivyo, urithi wa wanawake ni jambo ambalo Natala haungi mkono kwani hata linamshangaza anaposikia kuwa mhudumu katika jengo la ufuo, anajigamba amemrithi mke wa kakake na kumwuliza kama hilo ni jambo la kuonea fahari (uk. 19). Matamshi ya Natala yanaonyesha kwamba, yeye ni mwanamke ambaye haungi mkono utamaduni na mila potovu ambazo hazina mchango wowote katika maendeleo ya jamii bali zinakwamiza ukombozi wa jamii.

### **Uasherati**

Uasherati unadhihirika kama ukosefu wa maadili miongoni mwa wanajamii na ambao unajadiliwa kupitia wahusika Wakene, Chifu na Mhudumu katika jengo la ufuo. Hata hivyo, kuna wahusika wengine ambao hawajachangia moja kwa moja lakini wamehusishwa kwa njia moja au nyingine katika kudhihirisha na kujenga maudhui haya kama vile Gane na Natala.

Katika hali ya kawaida katika jamii nyingi za Kiafrika, uasherati ni kitendo ambacho kinashusha hadhi ya mwanamke pasipo kumhusisha mwanamume. Ni kitendo ambacho Natala kama mwanamke, hakubaliani nacho kamwe kwani kinadhihirisha uonevu wa mwanamke katika jamii.

Katika onyesho la kwanza, Natala ametumiwa kujenga maudhui ya uasherati hata kama yeye mwenyewe hashiriki mambo hayo. Gane anadhani kuwa Natala ana uhusiano wa kimapenzi na Chifu alipokuwa akimpasha Natala habari kuwa Chifu atampitia (uk. 2). Gane anaposema hatajua siri za watu wazima ana maana, Chifu anakuja kumwona Natala kuhusiana na mapenzi.

Mhudumu katika jengo la ufuo anaibua wazo la uasherati kupitia Natala. Anamwambia Natala lau hawezi kutia mkono mfukoni, pana njia fupi, njia ya mkato na iliyo rahisi (ya kushiriki kimapenzi) ili amtotee maiti ya mumewe (uk. 22).

Natala pia anapinga vikali wazo la wanakijiji la yeye kushirikiana na Wakene kimapenzi ili amsaidie katika malezi ya watoto baada ya 'kifo' cha mumewe (uk. 37-38).

Vitendo vyote vya uasherati katika *Natala* vinamhusisha Natala lakini kinyume na matarajio ya wanaomhusisha katika vitendo hivyo, anapinga vikali usherati kwa kujiheshimu kama mwanamke na kujitambulisha kama mtu mwenye msimamo thabiti. Anadhihirisha haya anaposema kwamba, kushirikiana na mwanamume si njia thabiti ya kutatua shida za kuwalea watoto kwani ana akili zake (uk. 36) na kwamba, ana uwezo wa kukabiliana na ujane wake pasipo usaidizi wa mwanamume (uk. 38). Aidha, anamwambia mhudumu katika jengo la ufuo kuwa yeye “ *si mlango wa jengo la umma kuguswa na kila mtu.*” (uk. 22). Natala anafanikiwa kupinga dhuluma kupitia ulumbi unaomwezesha ajieleze waziwazi.

Kutokana na vitendo vya Natala vya kupinga uasherati ambao unajitokeza kama uozo miongoni mwa wanajamii, Natala anajitokeza kama kielelezo bora kwa wanawake wengine katika jamii. Anastahili kuigwa kwa lengo la kuikomboa jamii kutokana na minyororo ya uasherati unaoisakama.

### **3.2.2 Tango Mwina Kama Ishara ya Utegemezi wa Mwanamke kwa Mwanamume**

Tango Mwina ameumbwa na mwandishi kama mjenzi wa mhusika mkuu Natala Tango. Ni mumewe Natala na babake Aliko na Bwanu. Ni mwanawe Mzee Balu na ni nduguye Wakene. Tango anafanya kazi mjini Ruma mbali na nyumbani (uk 9).

Tango amechangia ujenzi wa maudhui katika Natala kwa njia ya moja kwa moja na wakati mwingine kwa njia isiyo dhahiri. Hivyo basi, amechangia kukuza na kuendeleza maudhui yafuatayo:

#### **Kudhulumiwa na kudunishwa kwa mwanamke**

Tango ndiye chanzo cha kudunishwa na kunyimwa haki Natala. Pengo analoacha katika familia yake kupitia kilichosemekana kuwa ‘kifo chake’, kinamfanya Natala adunishwe na wanakijiji kwa kudai kuwa hana uwezo wa kuikimu familia yake na hivyo, anahitaji kutafuta mhimili (mwanamume) mwingine kama anavyoelekezwa na Mama Lime (uk. 36). Aidha Tila anajaribu kumdunisha Natala kwa kudai kuwa hayuko kwa Natala bali yuko kwa kaka ya mumewe (Tango) na kuwa Tango hawafukuzi kwake (uk. 5). Kwa hivyo, Tila anamdharau Natala kwa misingi kuwa mwanamke hana kwake bali ni kwa mumewe.

Matusi ya mtunza jengo la ufuo ndani ya chumba cha kuhifadhia maiti, ni matusi ambayo Natala anakabiliana nayo katika harakati za kupata ‘maiti’ ya mumewe Tango. Mtunza jengo la ufuo anamdunisha mwanamke kwa kumwona kama mpumbavu. Anasema kuwa maiti imelala kipumbavu kama gogo la mgomba alalavyo mwanamke (uk. 19).



Mwandishi anamchora Tango kama mhusika ambaye anakuja kutatua shida za Natala baada ya kuvamiwa na wanakijiji wakiongozwa na Wakene katika harakati za kumnyang'anya cheti cha shamba. Kitendo cha kutatua mafarakano baina ya Natala na watu wa ukoo wa Tango, kinaonekana kama kinachomdhalilisha mwanamke kwani mwandishi angeonyesha ushindi wa Natala katika kunyakua cheti pasipo kumpenyeza Tango pale kileleni mwa tukio la unyang'anyanaji wa cheti (uk. 57). Kitendo hicho kinadhihirisha kwamba mwanamke hawezi kujitetea wala hana uwezo wowote bila usaidizi na utegemezi wa mwanamume.

### **Uasherati.**

Kutokuwepo Tango ndiyo sababu wanaume wanataka kumfanyia Natala uovu ukiwemo kumtaka kwa mapenzi. Kupitia 'kifo chake', Chifu anamtuma Gane kwa Natala kumjulisha kuwa Chifu atapitia kwa Natala. Gane anachukulia kwamba, Chifu anakuja kumwona Natala kuhusiana na mapenzi (uk. 2-3).

Wakene nduguye Tango, anataka amrithi Natala kwa sababu Tango anasemekana 'ameaga dunia'. Iwapo Tango angekuwapo, Wakene asingetaka mapenzi ya Natala. Hivyo basi, tamko la Wakene na pendekezo la wanakijiji la kurithiwa kwa Natala, linaibuliwa na 'kifo' cha Tango.

Mhudumu katika jengo la ufuo anahitaji hongo ya mapenzi ndipo ampe Natala 'maiti' ya mumewe Tango. Kwa hivyo, kama hakungekuwa na mwili wa Tango katika chumba cha kuhifadhia maiti, Natala hangekabiliana na maneno ya mhudumu katika jengo la ufuo kuhusu mapenzi. Hii ina maana kwa kiasi kikubwa, mwandishi ameshindwa kumnasua mwanamke kutoka kwa pingu za kumtegemea mwanamume ndipo awe salama, aheshimike na awe na hadhi na heshima katika jamii yak i-ubabedume.

## **Urithi wa mwanamke**

Tango Mwina anachangia kujenga na kuendeleza maudhui ya urithi wa mwanamke kwa njia isiyo wazi. Tango mwenyewe hajamrithi mwanamke yeyote lakini amehusishwa na kutaka kurithiwa Natala. Tango anaposemekana ‘amefariki’, watu wa ukoo wake-Mama Lime, Mzee Palipali na Wakene wanapanga jinsi Natala angerithiwa na Wakene nduguye Tango ili aendeleze familia ya ndugu yake. Kwa hivyo, ‘kifo’ cha Tango ndicho kiini cha Wakene kutaka kumrithi Natala. Hili ni dhihirisho la jinsi mwanamke anavyochukuliwa kuwa mali ya mwanamume katika jamii hii.

## **Ufisadi**

Tango hajachangia ufisadi kwa njia ya moja kwa moja lakini vitendo vya ufisadi vinamzunguka. Mhudumu katika jengo la ufuo anadai hongo ili apeane ‘maiti’ iliyosemekana ni ya Tango (uk. 21-22), huku bwana Chifu ‘mwili’ wa Tango uzikwe kabla hajatoa kibali cha kujumuika katika mazishi ya Tango akiwa na nia ya kutaka hongo (uk. 30). Aidha polisi walisimamisha gari lilobeba maiti ya Tango na kuitisha hongo (uk. 16).

Vilevile, baada ya kuibiwa nguo na kitambulisho akiwa mjini Ruma, askari katika harakati za msako, wanamwitisha Tango aliitishwa hongo ya shilingi hamsini ambazo hakuwa nazo. Kwa sababu ya kukosa hongo, yeye na wenzake wanabandikwa kosa la kulewa na kuzurura wakiwa na nia ya kufanya maovu (uk. 60). Anashikwa na kufungiwa seli ambapo baada ya kufikishwa mahakamani na kukataa mashtaka, wanapelekwa rumande ambako wanateseka na kunyimwa kuwasiliana na jamaa zao kwa siku kadhaa na baadaye, wanakubali mashtaka na wanafungwa kifungo cha mwaka mmoja jela au kulipa faini ya shilingi elfu tano (uk. 60).

Kupitia maudhui haya, ni dhahiri kuwa Tango ni kitovu cha kudhihirisha vitendo vya ufisadi ingawa yeye hajashiriki ufisadi. Hili ni dhahirisho la umuhimu anaopewa mwanamume na mume katika jamii ya ki-ubabedume.

### **Uwajibikaji**

Tango anadhahirisha uwajibikaji kwani anaondoka kijijini kwao na kwenda mjini Ruma kufanya kazi ili aweze kuikimu familia yake. Anajitokeza kama mwanamume anayewajibika kwa familia yake. Kwa mfano, anamwarifu mkewe kupitia barua kuwa angefika nyumbani baada ya wiki moja kutoka kazini (uk. 5-6). Baada ya kupatwa na mkosi wa kuibiwa nguo na kitambulisho pamoja na kufungwa mwaka mmoja, anarejea nyumbani kwa furaha na unyenyekevu ambapo anachutama na kuwapokea watoto wake huku akiwajibika kwa kuwaletea vinyago, vibofu na vitabu vya picha (uk. 60). Kwa mkewe Natala, anamshawishi kuwa ni yeye mumewe anayempenda. Aidha anamwokoza kutokana na mateso na dhuluma alizopata kutoka kwa watu wa ukoo wake za kutaka kumnyang'anywa shamba, watoto na nyumba tukio linalodhihirisha utegemezi wa mwanamke kwa mwanamume.

### **3.2.3 Wakene kama mwakilishi wa Mila na Desturi Zinazomkandamiza Mwanamke**

Wakene ni mhusika mjenzi ambaye anatumiwa na mwandishi hasa katika ujenzi wa mhusika mkuu Natala pamoja na mhusika Tango. Ni mwanamume wa makamo. Ni mumewe Tila, mwanawe Mzee Balu na nduguye Tango Mwina.

Wakene anachangia ujenzi na uendelezaji wa maudhui yafuatayo:

## **Urithi wa wanawake**

Wakene anaungwa mkono na wanakijiji katika azima yake ya kutaka kumrithi Natala kwa kisingizio kuwa Natala hataweza kujikimu pamoja na watoto wake baada ya ‘kifo’ cha Tango. Hiyo basi, Wakene anachangia kujenga maudhui ya urithi wa wanawake. Anachangia katika kuendeleza maudhui haya kwa kuwaunga mkono Mama Lime na Mzee Palipali. Wanataka kumnyang’anya Natala cheti cha shamba, nyumba pamoja na watoto, kwa madai kuwa Natala amekataa kurithiwa.

Kupitia kitendo cha kutaka kumrithi shemijiye, Wakene anachangia kumdhalilisha mwanamke kwa misingi ya jinsia yake hasa pale anapomchukulia Natala kuwa hataweza kuwalea watoto wake pasipo kushirikiana naye. Aidha anachukulia kuwa mali na watoto ni milki ya mwanamume na ndiyo sababu anasema kuwa watoto wa Natala watabaki kwa familia ya Tango huku wakichukua cheti cha shamba na nyumba. Wakene hamchukulii Natala kuwa anaweza kumiliki chochote kama inavyochukuliwa na utamaduni wa jamii hii.

Uchukulizi kuwa wanawake hawamiliki mali ni dhahiri. Walichokuwa nacho mume na mke ni milki ya mwanamume. Kwa hivyo, mwanamke hahebiwi kama mrithi na anapoolewa, yeye na watoto wanachukuliwa kama sehemu ya mali ya mume. Wazo hili la kijamii si mwafaka na hivyo, linahitaji kubadilishwa kwani linamdhalilisha mwanamke ambaye ana wajibu sawa na mwanamume katika ndoa na jamii. Natala katika tamthilia anapinga wazo hili kwa kung’ang’ania cheti cha shamba na kukataa kurithiwa na Wakene.

## **Umaskini**

Wakene amesawiriwa na mwandishi kama mwanamume asiyewajibika kwa familia yake. Ni mlevi na huenda ikawa ulevi huu ndio unaochangia kutowajibika kwake. Mkewe anaonyesha hali ya umaskini wa hali ya juu kwa kuomba vitu vidogovidogo kama mafuta ya taa, sukari na chumvi. Anaomba vitu hivi mtawalia katika kipindi cha wiki moja kama anavyodai Natala (uk. 4).

Aidha, Wakene anasema kuwa ana matarajio ya kuwa mbunge. Hata hivyo, anaonekana hana pesa na hivyo, anasema atauza nusu ya shamba apate pesa za kufanyia kampeni (uk. 51). Kitendo hiki cha kuuza Shamba apate fedha za kufanyia kampeni ni dhahirisho la uchochole alio nao, kutojali na kutowajibika kwake.

## **Ubabedume**

Wakene anaongozwa na hisia za ki-ubabedume mwingi katika vitendo vyake. Kwa kutaka kumrithi Natala, anaonyesha ubabedume kwa kumwona Natala kama mtu duni asiyeweza kukosa kukimu mahitaji yake pamoja na watoto. Wakene anajiona kuwa na uwezo zaidi ya Natala kwa misingi kuwa yeye ni mwanamume na kuwa Natala ni mwanamke.

Wakene pia anamwona Natala kama mtu asiye na haki kama alivyo mwanamume anapomwambia Babake Mzee Balu kuwa, anamwuunga mkono mwanamke huyo (Natala) kwa mabaya na mazuri (uk 29) wakati Mzee Balu anamuunga Natala mkono kwa kuheshimu hisia zake kuwa jeneza lisifunguliwe wakati wa mazishi kwani mwili wa 'marehemu' Tango, haukuwa katika hali nzuri (uk. 28). Wakene kwa kuongozwa na fikra za kiubabedume anaona kuwa, mwanamke hana haki wala sauti katika jamii, na sauti inayostahili kusikizwa na kuheshimiwa ni ya mwanamume. Ni

kutokana na wazo hili potovu ndipo tunamwona Wakene akisema kuwa wazo la Natala lisiheshimiwe na hivyo, jeneza lifunguliwe.

Wakene ni kielelezo cha wanaume wasiowajibika katika jamii kutokana na tabia ya ulevi. Aidha ni mfuasi mila potovu katika jamii na ambazo hudunisha na kudhalilisha jinsia ya kike. Mila hizi zimepitwa na wakati na zina madhara katika jamii. Ni mwanamume anayeongozwa na hisia za ki-ubabedume katika kumtazama mwanamke pasipo kuzingatia uwezo alio nao, bali jinsia yake tu. Hivyo basi, Wakene anaakisi sifa ambazo hazistahili kuigwa na mwanamume yeyote katika jamii.

#### **3.2.4 Mama Lime na Tila kama Vielelezo vya Urengwaji wa Mwanamke katika Jamii**

Mama Lime ni mwanamke mzee wa ukoo wa Tango naye Tila ni mkewe Wakene. Mama Lime na Tila ni wanawake waliosawiriwa na mwandishi kama wahusika wajenzi. Wamesawiriwa kwa njia ya ulinganuzi na Natala kwani wanaonyeshwa kama wasio na msimamo thabiti kuhusu jinsia ya kike kama alivyo Natala. Wameumbwa kama wakinzani wakuu wa Natala katika kutetea haki za wanawake kwani wamerengwa na utamaduni unaotukuza ubabedume na hivyo, wanaungana na tapo la kuumeni kumdhalilisha mwanamke mwenzao.

Mama Lime na Tila wamechangia katika kuibua, kujenga na kuendeleza maudhui ya kudunishwa mwanamke, urithi wa mwanamke pamoja na umaskini wa wanawake.

#### **Kudunishwa kwa mwanamke**

Mama Lime amechangia maudhui ya kudunishwa kwa mwanamke kwa kushiriki vitendo vinavyodunisha. Mama Lime amechorwa na mwandishi kuwa mdadisi na mshawishi mtajika katika tamthilia. Kupitia sifa yake ya ushawishi, anatumwa kwa Natala na wazee wa ukoo wa

Tango kumshawishi Natala arithiwe na Wakene. Anamwonyesha Natala umuhimu wa kubakia katika familia ya marehemu mumewe, na kupendekeza njia mwafaka ni ya kurithiwa na Wakene. Kupitia kitendo cha kumshawishi Natala kurithiwa na Wakene ili abakie katika ukoo wa Tango, ni dhahiri kuwa anamdunisha Natala kwa sababu, Mama Lime anamwona Natala kama chombo cha kumilikiwa na wala si kama mtu ambaye anaweza kujisimamia na kuwa na maamuzi kuhusu maisha yake. Natala anapinga wazo hili kwa kusema wazi yeye ni binadamu na wala si kifaa (uk 40).

Mama Lime anamwona mwanamume kama kiumbe mwenye uwezo anaozaliwa nao na hivyo, kumfanya mwanamke kuwa mtegemezi wake kama anavyodai Lugano (1989). Mama Lime anadhihirisha utegemezi huu kwa kumweleza Natala atafute 'mhimili' (mwanamume) mwingine kama inavyodhihirishwa na mazungumzo baina yao. Anamweleza Natala, iwapo amefikiria kutafuta mhimili mwingine (uk 35-36).

Natala anapinga wazo la Mama Lime la kumtegemea mwanamume kwani ana uwezo wa kutosheleza mahitaji yake na familia yake. Tofauti na Mama Lime, Natala anaafiki madai ya Nnaemeka (2005) kuwa wanamke wa Kiafrika, kama wanawake wengine ulimwenguni, ana uwezo wa kujipatia mahitaji yake. Hili ni wazo ambalo linastahili kuzingatiwa katika jamii ili wanajamii waweze kupiga hatua ya kimaendeleo kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Tila amesawiriwa kama mwanamke mwenye kiburi na mgomvi. Kutokana na sifa hizi, anaonekana akizua ugomvi na Natala alipoenda kuomba chumvi (uk. 3-4). Anapopewa chumvi kidogo kwa sababu Natala amebakia na chumvi kidogo, haridhiki bali anazua ghasia kwa kujivuna kuwa yeye si mwombaji na hawezi kupimiwa chumvi kidogo kama inayopewa mdudu. Anapoendelea na vurugu, Natala anamwamuru aondoke kwake. Anadinda na kusema kuwa,

hakuwa kwa Natala lakini kwa Tango kakake mume wake (uk. 5). Kutokana na madai kwamba, kwa Natala si kwake bali kwa Tango, Tila anamdunisha mwanamke kwa vile anamchukulia Natala kama asiye na uongozi wa kiwango sawa na mwanamume katika familia.

### **Urithi wa mwanamke**

Mama Lime amechangia ujenzi wa maudhui ya urithi wa mwanamke kwa kuwa anashikilia mila na desturi potovu na zilizopitwa na wakati. Mama Lime alitumwa na wazee wa ukoo wa Tango kumpasha Natala ujumbe wa kurithiwa na Wakene. Anamshawishi Natala arithiwe na Wakene kwa kumwonyesha manufaa ya kurithiwa na hasa kuwa mke wa pili. Anamwonyesha jinsi kazi za nyumbani itakuwa rahisi akiwa na mke mwenza (uk. 38). Anamjulisha majukumu ya mwanamke ni kupata watoto, kuwa na malazi, nguo na shibe (uk. 39) na ambayo atayapata tu kwa na raha akirithiwa na Wakene. Natala mwenyewe anapinga mila ya kurithiwa mwanamke kwani anaiona kama inayombagua mwanamke kwa kumpembeza pasipo kushughulikia hisi na haki zake huku ikizingatia kukimu haja za mwanamume kama inavyodhihirishwa na mazungumzo baina yake na Mama Lime (uk. 39)

Tila anaongozwa na mila na desturi za ukoo wake kumwona Natala kama mtu asiyeweza kuishi bila mume baada ya 'kifo' cha mumewe Tango. Anajua fika kuwa mume akifa katika jamii yake, sharti mjane arithiwe hususan na kakake mumewe. Hivyo basi, Tila anachangia uendelezaji wa maudhui ya kumwona mwanamke kama bidhaa au chombo. Anamgombeza Natala kwa kumwambia ya kwamba, anajua njama zake na Mama Lime za kutaka yeye Natala arithiwe na Wakene.



## Umaskini

Tila ni kielelezo cha umaskini uliosakini katika jamii hasa unaotokana na ukosefu wa ajira. Tila amechorwa kama mtegemezi wa mume hata kwa vitu vidogo kama vile chumvi, sukari na mafuta ya taa. Kwa upande mwingine, mumewe Wakene si mwajibikaji kwa familia yake kwani ni mlevi wa kupindukia. Kutokana na kutowajibika kwa Wakene na Tila kukosa ajira, tunamwona Tila akimwendea Natala kumwomba vitu vya thamani ndogo katika kipindi cha wiki moja kama inavyodhihirishwa na maneno ya Natala,

*Lakini tila ulikuwa hapa juzi nikakupa*

*sukari – gilasi mbili. Ulikuwa hapa siku*

*nne zilizopita nikakupa mafuta ya taa.*

*Leo tena unataka chumvi! [Uk 3].*

Mama Lime na Tila ni wanawake waliosawiriwa kuwa wenye mtazamo hasi kuhusu mwanamke mwenzao katika jamii. Ni wanawake wanaoakisi madai ya Okome (1999) kuwa, wanawake wa Kiafrika hawana uwezo, wamechanganyikiwa na pia wasioweza kujiamulia mambo wenyewe. Kauli yao si sahihi katu kwa kuzingatia wahusika wa kike kama Natala katika jamii inayowakilishwa katika *Natala* na ambayo ni kiwakilishi cha jamii pana ya Afrika. Natala ni kiwakilishi cha mwanamke shupavu katika jamii na anajitokeza kama mwenye uwezo sawa na mwanamume, aliye na akili timamu na aliye na uamuzi katika masuala yanayomhusu binafsi na jinsia ya kike kwa ujumla. Hivyo basi, Mama Lime na Tila ni wanawake ambao wanahitaji kuhamasishwa kuhusu haki za binadamu na hususan haki za mwanamke ili wasimchukulie kama kifaa cha kutumiwa na mwanamume tu na kisicho na sauti wala uamuzi maishani. Vivyo hivyo,

wanafaa wazinduliwe wasirengwe na jamii ya ki-ubabedume wakaendelea kuona yanayofanywa kupitia utamaduni, ni mambo ya kawaida.

### **3.2.5 Mhudumu katika jengo la ufuo kama mwakilishi wa kutowajibika kwa wahudumu wa umma na unyanyasaji wa kijinsia**

Mhudumu katika jengo la ufuo ni mhusika wa kiume na mhudumu wa umma. Uhusika wake umejengeka kupitia mbinu ya mchezo ndani ya mchezo. Ni uhusika ambao umetokea kama kisengerenyuma kuelezea kilichotokea awali katika *Natala* na sehemu yake imeigizwa na Bala. Mchezo ndani ya mchezo unahusu matukio yaliyofanyika wakati Natala na Bala walienda kuchukua ‘maiti’ ya Tango katika chumba cha kuhifadhia maiti. Ni mhusika ambaye anayeendeleza taasubi ya kiume katika wasifu wake jambo linalodhihirishwa na maneno yake, matendo yake pamoja na hulka yake.

Mhudumu katika jengo la ufuo anachangia katika kukuza na kuendeleza maudhui yafuatayo:

#### **Ufisadi**

Mhudumu katika jengo la ufuo anachangia ufisadi kwa kushiriki vitendo vya ufisadi. Anamtaka Natala atoe hongo ya fedha na mapenzi ili ampe mwili wa marehemu mumewe Tango. Anaitisha hongo kudai kuwa maisha yana gharama kubwa na hasa kwake mwenye watoto saba wa kulisha na mshahara wake mdogo kama inavyojitokeza katika kauli yake (uk. 21).

#### **Umaskini**

Mhudumu katika jengo la ufuo amesawiriwa kama maskini. Ni dhahiri kuwa kazi yake ya kuhudumu katika chumba cha kuhifadhia maiti ni ya kiwango cha chini katika jamii na inampa

mshahara mdogo kama inavyodhihirishwa na maneno yake anaposema kuwa mshahara wake ni wa pesa nane (uk. 21). Anasema kwamba, ana watoto saba na wana mahitaji mengi – karo, mavazi ya shule pamoja na fedha za ujenzi wa shule na ameshindwa kuwalea kwani anasema kuwa ana wiki moja hajatuma pesa zozote za matumizi kwa familia yake (uk. 21).

Tabia yake ya kula mandazi kwenye chumba cha kuhifadhia maiti ni hali inayoonyesha umaskini. Anatoa mandazi mfukoni na kuyalia mle ndani ambapo ni pahali pachafu, panaponuka na hata hana chai (uk. 18).

### **Utamaduni uliopitwa na wakati**

Mhudumu katika jengo la ufuo anachangia maudhui ya utamaduni uliopitwa na wakati kwa kushiriki mila zilizopitwa na wakati. Kitendo hicho kinajitokeza katika mazungumzo baina yake na Natala. Anamwambia Natala ya kwamba, amemrithi mke wa kaka yake (uk. 19). Amesawiriwa kama mfuata mila za kijamii pasipo kuangazia na madhara yake na huenda ikawa sababu ya kumrithi mke wa kaka yake na ambapo yeye mwenyewe hawezi kukimu mahitaji ya familia yake kubwa.

Mhudumu katika jengo la ufuo aidha anachangia maudhui ya uasherati. Anamtaka Natala atoe hongo ya kimapenzi pasipo kuzingatia madhara ya kufanya mapenzi kiholelaholela hasa kipindi hiki kilichokumbwa na janga la ugonjwa wa Ukimwi. Anasema,

*... Tuelewane. Palipo na nia, hapakosi*

*njia. Ikiwa hutaki kutia mkono mfukoni,*

*si hoja.Njia fupi.Njia ya mkato.Njia rahisi.*

[uk. 22]

## **Taasubi ya kiume**

Mhudumu katika jengo la ufuo anaongozwa na taasubi ya kiume kumnyanyasa mwanamke. Maneno yake yanaonyesha taasubi nyingi. Kwanza, anapokula mandazi katika chumba cha kuhifadhia maiti, anafikiria kwa vile ni mwanamume na kwamba Natala anahitaji kuhudumiwa naye, atakubali kuchukua kipande cha andazi alichompa. Pili, anaongozwa na mtazamo wa ki-ubabedume kumrejelea Natala kama mwanamke kwa azimio la kumbeza badala ya kutumia lugha ya heshima. Anasema, “.... *Mwanamke, unataka nini?*” [uk. 17]

Aidha anadhihirisha taasubi ya kiume katika kuizungumzia maiti katika jengo la ufuo. Kwa mfano, anaiuliza maiti kama inainua shingo kama kwamba haijawahi kumwona mwanamke (uk. 17). Aidha anasema maiti imelala kipumbavu ‘kama mwanamke’ (uk. 19). Mifano hii ni dhihirisho kwamba, mhudumu katika jengo la ufuo, anamchukulia mwanamume kuwa mwerevu na mwungwana kinyume na mwanamke.

Mhudumu katika jengo la ufuo ni kielelezo cha watu wa ajira muhimu katika jamii lakini wanatumia nafasi zao kuwadhulumu wengine katika jamii hasa wanapohitaji huduma zao. Anaendeleza ufisadi, uasherati na ubabedume-tabia ambazo zinahitaji kupigwa marufuku katika jamii ili iweze kujikomboa kikamilifu.

### **3.2.6 Gane kama mwanamke anayepinga dhuluma dhidi ya jinsia ya kike**

Gane ni binamuye Tango na rafikiye Natala. Ni mhusika mdogo na ambaye amechangia katika ujenzi wa mhusika mkuu Natala. Amesawiriwa kama ambaye amewajibika kwa jinsi ambayo anashughulikia watoto wake na hata watoto wa Natala.

Katika Natala, Gane amechangia ujenzi na uendelezaji wa maudhui yafuatayo:

### **Uwajibikaji**

Gane amechangia uwajibikaji kwa kufanya mambo yanavyoonyesha uwajibikaji. Anaiwajibikia familia yake na jamii kwa ujumla. Kwanza, anaonyesha uwajibikaji kama mzazi pale ambapo anaonekana akiwafanyia watoto wake sherehe ambapo watajumuika na watoto wengine kama wa Natala na jirani mwingine kwa jina Amita (uk. 1-2). Aidha, Natala alipokwenda kuchukua mwili wa Tango, Gane alibakia nyumbani kwa Natala akiwashughulikia watoto wa Natala (onyesho la pili).

Gane anaonyesha uwajibikaji wake kama mwanajamii pale anapotumwa na Chifu kupeleka ujumbe kwa Natala na anaufikisha kwa wakati ufaao (uk. 2).

### **Umbea**

Gane hachangii umbea moja kwa moja bali anachangia katika kuudhihirisha, kama inavyojitokeza katika mazungumzo yake na Natala. Anapotumwa na Chifu kwa Natala amwambie kuwa chifu angempitia Natala baadaye, Gane alijiwa na wazo kuwa chifu anakuja kumwona Natala kuhusiana na mapenzi. Wazo kama hilo la Gane ni wazo potovu na ambalo linapaswa kumulikwa sana katika jamii na kutupiliwa mbali kwa sababu ni wazo ambalo linadunisha na kushusha hadhi ya mwanamke.

### **3.2.7 Alika na Bwanu**

Alika na Bwanu ni watoto wa Natala Tango na Tango Mwina. Alika ni mtoto wa kike wa miaka sita hivi ambaye ni kifungua mimba katika familia yake. Bwanu naye ni mtoto wa kiume ambaye ni mdogo wa Alika mwenye umri wa miaka minne.

Watoto hawa wametumiwa katika tamthilia hii kwa lengo la kuwakamilisha Tango na Natala kama wazazi. Ni wahusika ambao wamekamilisha lengo la ndoa ya Natala ambayo ni kielelezo cha ndoa katika jamii ya Kiafrika ambayo haioni ndoa kuwa kamilifu pasipo watoto na hivyo, kutumiwa kama kisingizio cha kumdhalilisha mwanamke.

### **3.2.8 Hitimisho**

Wahusika katika *Natala* wanaakisi mahusiano ya kijamii tunamoishi ambayo ni mtagusano wa wanawake kwa wanaume, wazee kwa vijana na watoto kwa watu wazima. Kithaka wa Mberia amewaumba kwa njia ambayo wanachangia kujenga na kuendeleza maudhui mbalimbali. Amefanikiwa kufanya hivi kwa kuwapa nafasi mahsusi, kuwahusisha katika vitendo maalum ambavyo vinatukia katika mazingira teule, kwa kutumia lugha zao, mitazamo yao wasifu wao na mienendo yao wakafanikisha maudhui. Baadhi yao kama Mama Lime, Mhudumu katika jengo la ufuo, Chifu, Polisi na Wakene wamedhihirisha vitendo viovu ambavyo vinastahili kupigwa marufuku katika jamii kama ufisadi, urithi wa wajane, uasherati na kudunishwa mwanamke kwani ni mambo yanayorudisha jamii nyuma. Kwa upande mwingine, wapo walioakisi hulka njema kama Natala kwa kuwajibika na kutetea haki za binadamu na hasa jinsia ya kike iliyokandamizwa kupitia mfumo wa kuumeni uliojengeka katika jamii.

## SURA YA NNE

### MATUMIZI YA LUGHA YANAVYOENDELEZA MAUDHUI

#### 4.0 Utangulizi

Kithaka wa Mberia ametumia mbinu mbalimbali za lugha katika kufanikisha kazi yake na ambazo zimechangia ukuzaji wa dhamira na uendelezaji wa maudhui katika *Natala*. Miongoni mwa mbinu alizotumia ni pamoja na: Takriri, tashihisi, sitiari, kinaya, jazanda, methali, misemo, chuku, usemaji kando, uzungumzinafsiya na maswali ya balagha,

#### 4.1.0 Mbinu za Lugha

#### 4.1.1 Tashihisi/ Uhuishi /uhaishaji

Tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai au vyenye uhai huwasilishwa au kusawiriwa kwa namna iliyo sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi. Aghalabu tamathali hii hutumiwa pia kurejelea sifa ya kuwapa wanyama sifa za kibinadamu. Dhima ya uhuishi ni kutilia mkazo wazo au jambo fulani.

Tashihisi ni mbinu iliyotumiwa na Kithaka wa Mberia kuibua maudhui ya umaskini katika *Natala*. Natala na Gane wanapoenda kuchukua ‘mwili wa Tango’ wanakawia na wanapoulizwa na mzee Balu sababu za kuchelewa, wanaeleza kuwa gari walilosafiria halikuwa katika hali nzuri. Lilikataa kuwaka zaidi ya mara tatu. Kila lilipogoma, iliwabidi kulishawishi kwa muda mrefu (uk 16).Gari ambalo halikuwa katika hali nzuri linadhihirisha umaskini wa Natala ambaye hana ajira kwa vile jamii inachukulia mahali pa mwanamke ni nyumbani na kazi yake kuu ni kulea watoto huku mwanamume akiwa mwenye ajira na ndiyo sababu Tango alienda mjini Ruma kufanya kazi

huko. Kwa vile hawakuwa na uwezo mwingine, walilishawishi gari kama mtu kwa muda mrefu ili waweze kuendelea na safari. Uhuishi huu unatumiwa ilikusisitiza matatizo waliyoyapata njiani na sababu ya kuchelewa kufikisha mwili kwa wakati waliotarajiwa.

#### **4.1.2 Kinaya**

Kwa mujibu wa Chimera na Njogu (1999), tamathali hii ya usemi inahusisha ukinzani kati ya hali ilivyo na inavyosemakana kuwa. Ni kauli ambayo ina maana ya kinyume. Kinaya cha drama hujitokeza kwa njia ya maigizo yanayoonyesha kinyume cha matarajio au matumaini ya mhusika fulani. Ni aina ya kinaya ambayo ina sehemu ya dayalojia yenye maana mbili: ya msemaji na ya msikilizaji. Msemaji ana maana tofauti na anavyojua msikilizaji (Msokile 1993). Dhima ya kinaya ni kuibua ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kukejeli au kwa kutia chuku kwa lengo la kusesitiza.

Mwandishi wa *Natala* ametumia mbinu ya kinaya kuibua na kujenga maudhui kama

#### **Umaskini**

Wakene anadai kuwa yeye ni “Wakene BankInternational” kuonyesha kwamba, yeye ni tajiri ilhali anaomba usaidizi wa fedha kidogo kama shilingi thelathini kutoka kwa Gane (uk 13). Ombi la shilingi thelathini ni dhihirisho la umaskini alio nao Wakene na bado anajiita ‘Wakene Bank international’ benki imara iliyo na riba nzuri na njia rahisi ya kuzalisha akiba. Wakene anajitia majigambo ya kuwa yeye ni tajiri ili ajipendekeze kwa Gane rafikiye Natala kwani ana lengo la kumrithi Natala. Hivyo basi, umaskini wa Wakene umejengwa kupitia kinaya kinachokejeli.



## **Urithi wa mwanamke**

Wakene anamwambia Natala wimbo wa mapenzi badala ya kuomboleza baada ya kufikiwa na habari ya kifo cha nduguye Tango (uk 11-12).Wimbo wa Wakene ni kinaya kwa sababu unaonyesha furaha ya kutaka kumrithi Natala badala ya huzuni ya kifo cha Tango.

Aidha Natala anaonyesha kutoridhishwa kwake na jambo la kurithiwa na Wakene kwa njia ya kinaya drama .Wakati Tila anamwendea Natala kwa kuzua ugomvi kuwa Natala na Mama Lime walikuwa na njama ya Natala arithiwe na Wakene, Natala anakubali kuwa, wana mradi wa thamani kubwa kama dhahabu ambao ni wa kuchangiwa mume na Tila ili kutimiza ndoto ya kukumbatiwa na kuhisi mpigo wa moyo wa mumewe Tila kwenye kifua chake na kunawa kwenye jasho lake. Licha ya hayo yote, aishi maisha mazuri kutoka wakati huo hadi kifo kiwatenganishe (uk 43).

Natala anayasema haya yote kuonyesha jinsi asivyoridhishwa na jambo la kurithiwa kwake na Wakene, lakini anasema kwa njia ya kinyume cha anayoyasema.

Uamuzi wa wazee wa ukoo wa Tango kuwa, Natala arithiwe na Wakene kwa sababu Wakene atamsaidia Natala kulea watoto ni kinaya. Hali halisi ya Wakene ni kuwa ni mtu asiyewajibika hata kwa familia yake kutokana na ulevi wake. Anaonekana akiomba shilingi thelathini kutoka kwa Gane na Wakene yuyo huyo ambaye ni fakiri tayari ndiye anayesemekana atamsaidia Natala kutosheleza mahitaji yake na ya watoto.

### 4.1.3 Jazanda/ taswira

Jazanda ni kunga ya utunzi ambapo lugha inatumiwa kusawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno mateule au tamathali za usemi. Kwa njia hii, mtunzi anamwezesha msomaji kuona, kuhisi au kunusa kitu kinachoelezwa (Mbatiah 2001).

Kithaka wa Mberia ametumia jazanda katika *Natala* kuibua maudhui kwa njia iliyo fiche pasipo kutumia lugha wazi. Maudhui yaliyojengwa kijazanda ni haya yafuatayo:-

#### Taasubi ya kiume

Mazungumzo baina ya Gane na Wakene nyumbani kwa Natala baada ya 'kifo' cha Tango, yanaonyesha majigambo ya Wakene ya kwamba yeye ni mwanamume kamili, 'kwa kujiita mtambo wa umeme' kama inavyodhihirishwa na nukuu hii.

Wakene anadai,

*Mtambo! Ungepata fursa ya kujua kwamba*

*Wakene ni mtambo wa umeme! (Akijipigapiga*

*kifuani) Mtambo wa umeme;*

(uk 12)

Kutokana na nukuu hapo juu, Wakene anatawaliwa na taasubi ya kiume kwa kujiita mtambo wa umeme jambo ambalo Gane analiona tofauti kabisa. Gane haoni uwezo huo wa Wakene bali anamwona kuwa mtu ovyo kabisa na hivyo kumfananisha Wakene na 'mboga'. Ni dhahiri kuwa tabia na kauli za Wakene, zinarutubishwa na mfumo wa ki-ubabaedume unaotawala jamii hii.

## **Matatizo ya ujane**

Natala anatumia jazanda kudhihirisha ujane wake. Akizungumza na Gane baada ya kufikisha ‘mwili wa Tango’ nyumbani kutoka chumba cha kuhifadhia maiti, kuwa kusema; *“Maskini watoto wangu; hawajui maisha yao yamekabiliwa na uhalisi mpya. Hawajui kutoka sasa hawatakuwa na mikono miwili ya kuwahimili. Umebakia mkono mmoja tu.”* (uk 23). Natala anamaanisha ya kwamba baada ya kifo cha mumewe Tango, sasa malezi ya watoto yamebakia mikononi mwake pekee. Kwake Natala kama ilivyo kwa mwanajamii yeyote, mama na baba ni walezi wa watoto ambao hufanya kazi kwa kusaidiana, na hivyo basi anahofia maisha ya watoto wake baada ya kufiwa na mumewe. Maneno ya Natala yanadhihirisha hali ngumu ya ujane uliomfika baada ya kumpoteza mume. Lakini ni dhahiri kuwa, mfumo wa jamii hii kupitia utamaduni na ubabedume ndio unaomrenga mwanamke hadi ajione mnyonge kwa kuondokewa na mlinzi, tegemeo la kiuchumi, kijamii na kiongozi wa maisha yake kama mke na mwanamke.

## **Urithi wa wajane**

Mama Lime anatumia lugha shawishi na iliyo fiche kwa Natala ili kujua kama ana fikra ya kurithiwa baada ya ‘kifo’ cha mumewe Tango. Mama Lime anamwuliza Natala, *“Je! Umefikiria umuhimu wa kutafuta mhimili mwingine?”* (uk 36)

Mama Lime anatumia jazanda ya mhimili kwa maana ya mume atakayeshikilia nafasi iliyoachwa na Tango.

Tila anataka kupinga wazo la wazee wa ukoo wa Tango la kurithiwa kwa Natala na Wakene. Anamwambia Natala kuwa Wakene hayumo mikononi mwa mwanagenzi bali yumo kwenye viganja vya mganga mahiri (uk 44). Kwa kujita mganga stadi, Tila anamaanisha ya kwamba,

anamtosheleza Wakene kimapenzi na hivyo hakuna haja ya Natala kufikiria Wakene anamhitaji kimapenzi. Lengo kuu la Tila nikukomesha kurithiwa kwa Natala na Wakene.

Aidha, Tila anapofika kwa Natala kuulizia shaka alizokuwa nazo kuhusu kurithiwa kwa Natala na Wakene, Tila anauliza maswali kijazanda kwa njia ambayo Natala hakuelewa wazi na hivyo akamwita Tila wakili. Anasema; *“Naona leo nimo mahakamani, na mahakama kwenyewe nimekumbana na wakili stadi kabisa. Ametafuna na kumeza vitabu vyote juu ya utaratibu wa kuhoji”*. (uk42). Natala alitumia jazanda ya mahakama na wakili kwa sababu maswali aliyoulizwa na Tila kuhusu kurithiwa kwake na Wakene, hakuyaelewa na Tila naye hakuwa wazi hivyo mandhari ya maswali hayo yaliakisi mahakama huku Tila akiakisi wakili halisi.

#### **4.1.4 Maswali ya balagha**

Maswali ya balagha ni mbinu ambayo hujitokeza katika fasihi pale ambapo mtunzi au mhusika kwa lengo la kumtanabahisha msomaji au msikilizaji, anauliza maswali bila majibu.

Dhima ya maswali ya balagha ni kutoa mawazo au hisi za ndani za mhusika au kuweka jambo fulani wazi kwa hadhira na ambalo linahitaji kuangaziwa nao kwa makini. Aidha, maswali ya balagha hutumiwa kusesitiza wazo ambalo mwandishi hakudhamiria kulieleza tu au kulitaja bayana.

Mwandishi wa Natala anatumia maswali ya balagha ambayo yanaulizwa na wahusika kuangazia maudhui fulani. Kwa mfano:-

## **Ujane**

Natala ametumia uzungumzinafsia wa kibinafsi kutoa hisi za moyo wake kuhusu maisha yake baada ya kifo cha mumewe Tango. Anatumia maswali ya balagha kwa mfululizo kudhihirisha ujane uliomfika. Kwa mfano;

*Maskini watoto wangu na mjane mamao! Msiba ulioje? Huzuni na ukiwa!*

*Kukumbukumbu na uhalisi mchungu. (uk 34); Dhiki gani hii? Kwa nini*

*ninyang'anywe mume? Kwa nini Mungu wangu, kwa nini? Kwa nini*

*unanitenda haya? Dhiki kwa nini unanifuata hivi? Kwa nini; kama*

*kivuli kikifuata mwili? (uk 9)*

Maswali ya balagha yaliyotumiwa na Natala yanadhihirisha uchungu alio nao baada ya kifo cha mumewe hali ambayo inaonyesha ujane wa Natala.

## **Urithi wa wanawake**

Natala anatumia maswali ya balagha katika uzungumzinafsia wa kihadhira kuonyesha jinsi hangependa kurithiwa na Wakene; wakati Tila alimgombeza kwa tuhuma anataka kurithiwa na Wakene.

Natala anaizungumzia hadhira kwa kusema,

*“Dunia imeumbwaje? Vituko vyake, watu wake,*

*mambo yote ni kama ndoto. Ndoto bila busara.*

*Ndoto za mwenye kuugua malaria. Mimi, mimi,*

*Natala, nitake kurithiwa kama kifaa? Na*

*mrithi mwenyewe ni mumewe Tila! La,*

*Tila.” (uk 45).*

Maswali ya balagha anayouliza Natala yanajenga na kuendeleza maudhui ya urithi wa wanawake kwa njia ya kupingwa na Natala kwani hataki kurithiwa kama kifaa. Maswali hayo yanadhihirishia hadhira mwelekeo wa matukio hasa kuhusiana na urithi anaotarajia Wakene wa Natala.

Maswali ya balagha yanayoulizwa yana lengo la kuarifu na kuihamasisha jamii kuhusu matatizo na udhalimu unaomkumba mwanamke katika jamii.

#### **4.1.5 Methali, misemo na nahau**

Methali, misemo na nahau ni kunga za fasihi ambazo hutumia lugha kimapumbo. Kunga hizi zaidi ya kupamba lugha, zina kazi ya kufafanua maudhui.

Methali ni kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe na inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha hekima na busara. Methali huwa ni sehemu ya turathi za kimapokeo za jamii zinazobeba falsafa, mila, miiko na desturi za jamii (Mbatiah 2001). Kutokana na maelezo haya, methali basi inafafanua maudhui kupitia maana na ujumbe ibebao.

Misemo na nahau ni istilahi za fasihi ambazo huzaliwa, hukua na pengine hufa. Matumizi yake katika kazi ya fasihi sharti yategeme uhai wake katika matumizi yake ya kawaida katika jamii. Nahau ni misemo iliyojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida na aghalabu huwa imesetiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno (Msokile 1993). Kwa hivyo misemo na nahau huonyesha maana fiche iliyobebwa na maneno.

Mwandishi ametumia lugha ya mafumbo katika methali, misemo na nahau kufafanua maudhui ya umbea. Gane anatumia lugha fiche ili asimwudhi Natala akimwambia wazi ya kwamba kitendo cha chifu cha kutaka kumwona ni kutaka uhusiano wa kimapenzi. Anatumia methali “*palipo na moshi hapakosi moto*” (uk 3) kwa maana ya kuwa kitendo cha chifu cha kutaka ‘amwona’ ni dalili ya jambo la siri ambalo linaweza kuwa kuanzisha uhusiano wa kimapenzi.

Gane anatumia lugha ya kimaumbo kwa Natala kwa sababu anaelewa fika kuwa, umbea ni kitendo cha aibu katika jamii na kwamba ni kitendo kinachoshusha hadhi ya mwanamke na hivyo lengo lake si kushusha hadhi ya Natala.

#### **4.1.6 Takriri**

Takriri ni tamathali ya usemi ambayo huhusu kuisisitiza au kushadidia ujumbe ili msomaji apate athari ya msisitizo huo kwa kurudia neno au kifungu cha maneno (Wamitila 2003). Kwa kuunga mkono maelezo ya Wamitila, takriri huunda usambamba wa kisauti na kimawazo na hivyo kuongeza uzito wa ujumbe wa mwandishi.

Takriri imetumika katika *Natala* kujenga na kuendeleza maudhui ya ujane na urithi wa mwanamke.

## Ujane

Baada ya kujulishwa habari na bwana chifu kuhusu ‘kifo’ cha mumewe, Natala anaonyesha kutoridhika kwake na hali hiyo kwani amebakia mjane. Analaani kitendo cha kifo cha mumewe kwa kukiona kuwa dhiki kubwa na kuuliza maswali ya balagha yasiyokuwa na majibu, “kwa nini?” Anasema;

*Dhiki gani hii? Kwa nini ninyanganywe mume?.....*

*kwa nini Mungu wangu, kwa nini? Kwa nini unanitenda*

*haya? [kwa uchungu mwingi] Dhiki, kwa nini unanifuata*

*hivi? Kwa nini kama kivuli kikifuata mwili? (uk 9) [Angali*

*hohe sakafuni] Kwa nini? Mungu wangu, kwa nini? (uk 10).*

Uradidi wa maneno, ‘kwa nini’ ni dhahirisho kwamba Natala amesononeka sana moyoni kutokana na uchungu anaouliza nao na kuwa anauliza Mungu. Hafurahii kamwe hali ya ujane inayodhihirishwa na pengo la marehemu mumewe Tango.

Aidha Natala anadhihirisha hali ya ujane itakavyokuwa kwa watoto wake baada ya mazishi ya Tango walipokuwa wakuzungumza na Gane. Anasema;

*“Maskini watoto wangu. Hawajui maisha yao*

*yamekabiliwa na uhalisi mpya. Hawajui kuwa*

*kutoka sasa hawatakuwa na mikokomiwili ya*



*kuwahimili. Umebakia mkono mmoja tu*

(uk 23).

Kwa kurudia neno ‘hawajui’ Natala anataka kuonyesha ya kwamba, watoto hawaelewi ya kwamba, hali ya maisha imebadilika kabisa. Yeye ndiye atakayekuwa na jukumu la kuwatafutia riziki.

### **Urithi wa mwanamke**

Tila anapomwendea Natala kwa kumdhania anataka kurithiwa na Wakene, Natala anasisitiza kutokubali kurithiwa na Wakene kwa kusema haya:

Mimi, mimi Natala, nitake kurithiwa kama

kifaa? Na mrithi mwenyewe ni mumewe Tila!

La, Tila! Hata ningelikuwa nataka kuolewa upya,

hata mumeo hangelikuwa ameo, hangeliangukiwa

na jicho la Natala! La! La Tila sina haja na bata

wako! Mimi si matope kukaribisha mabata. (uk 45).

Uradidi huu unadhihirisha jinsi Natala anavyochukia kurithiwa hasa na Wakene.

Wimbo Wakene anaomwambia Natala (uk 11) ni takriri inayoleta utamu katika masikizi. Mwandishi ametumia takriri hii kuonyesha ya kwamba ujumbe unaowasilishwa ungeleta utamu katika maisha ya Natala kulingana na Wakene. Kwa hivyo ni, takriri ya kitaashira ambayo inavuta

makini ya msikilizaji na hivyo, kuisimua akili yake kuzingatia kwa makini furaha itakayotokana na mapenzi ya Natala na Wakene.

#### **4.1.7 Chuku/ mubaalagha**

Chuku ni tamathali ya usemi ambapo msemaji hutia chumvi maneno yake kwa nia mahsusi; kwa kusimulia jambo la kawaida kama jambo la kustaajibisha, jambo dogo kudunishwa kupita kiasi au jambo kubwa kukuzwa kupita kawaida (Kuhenga 1977). Lengo la matumizi ya chuku ni kutilia mkazo maelezo ya hali ya kitu, mtu au jambo fulani kama ilivyo.

Chuku imetumika katika Natala kuangazia masuala yafuatayo:

#### **Mfumo wa Ubabedume**

Gane na Wakene wanaonyesha na kudhihirisha umaskini wa Wakene kwa njia ya chuku. Wanaashiria hali ya umaskini kwa njia ya kinaya pale ambapo wanamwita Wakene ‘benki’ ilhali ni maskini hohehahe. Hali hii inaakisiwa na mazungumzo yao. Wakene anamwuliza Gane,

*“Una shilingi hamsini ambazo ungependa kuweka benki? .....Wakene Bank intenationa”*. Gane anamjibu, *“Wakene Bank ltd! Benki imara riba nzuri. Njia rahisi ya kuzalisha akiba”*. (uk 13)

Mazungumzo haya yanatokea nyumbani mwa Natala ambapo Natala alikuwa ameendea ‘maiti ya Tango’ huku Gane akibakia nyumbani. Hivyo basi,Wakenekwa kujua kakake Tango ameaga dunia, anajiwa na fikra za kujaza pengo lililoachwa wazi na Tango.La kusikitisha ni kwamba, Wakene ni mlevi wa kupindukia asiye na mbele wala nyuma na bado anataka amrithi Natala kwa kuongozwa na fikra za ki- ubabedume kuwa mwanamume ni kiongozi kwa kuzaliwa.

#### **4.1.8 Sitiari**

Sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi ambapo vitu vya aina mbili au zaidi au vyenye sifa tofauti hulinganishwa moja kwa moja pasipo kutumia viunganishi kama vile; kama, mfano wa, mithili ya, kana kwamba, sawa na au tamthili ya (Msokile 1993). Ulinganisho katika sitiari hufanya kitu kimoja kitemwe kuwa ni kingine. Dhima ya sitiari ni kutilia msisitizo kwa jambo linaloangaziwa.

Sitiari zimetumiwa na Kithaka wa Mberia kuangazia masuala yafuatayo:

#### **Kudunishwa mwanamke**

Tila anapoenda kwa Natala kuomba chumvi anazua ugomvi akidai amepewa chumvi kidogo. Anapoendelea na ugomvi, Natala anamwambia asimchokoze huku Tila akimwuliza kama yeye (Natala) ni Mungu kama inavyodhihirika (uk 4). Tila anatumia sitiari ya Mungu kwa Natala ili Kumdunisha kwa njia ya kumdharau na kumdhalilisha.

#### **4.1.9 Usemaji kando**

Usemaji kando ni mbinu ya kiusemi ambapo msemaji hususan mhusika mmoja katika tamthilia hutoa ujumbe fulani akiwa jukwaani ambao hulenga mhusika mwingine au hadhira (Wamitila 2005)

Mwandishi wa Natala ametumia aina mbili za usemaji kando kujenga maudhui: usemaji kando wakibinafsi na usemaji kando wa kimazungumzo. Usemaji kando wa kibinafsi hutokea pale

ambapo mhusika anayesema kando husema mambo yanayomhusu pasipo kulenga mhusika mwingine jukwaani.

Usemaji kando wa kimazungumzo hutokea pale ambapo usemaji kando unaohusika unalenga kuyaendeleza mazungumzo fulani katika tamthilia.

Mbinu ya usemaji kando imetumika katika ujenzi wa maudhui kama:-

### **Mahusiano katika ndoa**

Katika onyesho la kwanza, Natala anapata barua kutoka kwa mumewe Tango ambaye anafanya kazi mjini Ruma mbali na nyumbani. Katika barua hiyo, Tango anamweleza Natala kuwa angerejea nyumbani baada ya wiki moja. Natala anaonekana ameridhishwa sana na habari kuwa mumewe angerudi nyumbani baada ya siku saba. Anatoa hisia za moyo wake kupitia usemaji kando wa kibinafsi kwa hadhira kwa kusema; (kwa hadhira)

*“Wiki moja! Siku saba tu! Kisha...[Anasafisha koo kama*

*kwamba anamaanisha “nayajua mwenyewe!”]Siku saba ni*

*safari ndefu. Ndiyo! Hasa ndoto ya lililoko mwisho wa safari*

*inapotawala akili (Gane anaonekana mlangoni, anasikiza)*

*Lakini zitapita! Moja, mbili, tatu....kisha: Saba! Siku ya*

*saba itafika.(Gane anaanza kumkaribia.Anasimama karibu*

*naye) kungojea kutafikia kikomo. (Tabasamu kabisa: kwa*

ishara ya mikono na macho....) *waaa! Tango Wangu!*” (uk 6)

Kupitia usemaji kando wa kibinafsi wa Natala tunabainikiwa kwamba, Natala anafurahia ndoa yake na Tango. Anaona siku saba kuwa nyingi kabla ya kurejea nyumbani kwa kipenzi cha roho yake, ili waungane pamoja katika asasi ya ndoa.

### **Ukombozi wa mwanamke**

Katika onyesho la tano, Natala aidha anajihusisha katika usemaji kando wa kibinafsi katika kuonyesha hadhira jinsi hangekubali kamwe kurithiwa na Wakene kama anavyodai Tila. Natala anailinganisha dunia na ndoto huku akidai kuwa kila kitu duniani ni kama ndoto na hivyo wanaodhania kuwa anahitaji kurithiwa ni kama wako ndotoni kwani ni jambo ambalo katu halitatendeka kwake. Anajinasua kutoka mila nadesturi za jamii yake kwa kutumia sauti yake kama ngao kwa wanaomdhalilisha mwanamke. Kwa kutokubali kurithiwa, Natala anasimamia ukweli kuwa mwanamke ana uwezo wa kupinga maovu katika jamii na hivyo, kukomboa vizazi vya baadaye. Anasemea hadhira kwa kusema ;

*Dunia imeumbwaje? Vituko vyake, watu wake,*

*Mambo yote ni kama ndoto. Ndoto bila busara.*

*Ndoto za mwenye kuugua malaria. Mimi, mimi*

*Natala, nitake kurithiwa kama kifaa? Na mrithi*

*mwenyewe ni mumewe Tila! La, Tila!.....(uk 45)*

#### **4.1.10 Uzungumzinafsia**

Uzungumzinafsia ni mbinu ya kiusemi ambapo mhusika huzungumza peke yake pengine kwa kuyataja mambo yanayomhusu kwa kuwaza kwa sauti au kwa kuyataja yanayohusu jamii pana na huenda yakawa kielekezi cha mkondo wa matukio (Wamitila 2008)

Kithaka wa Mberia ametumia uzungumzinafsia kuyaangazia masuala kama vile ujane na urithi wa mwanamke katika jamii.

#### **Matatizo ya ujane na uyatima**

Mberia ameendeleza maudhui ya ujane na uyatima kupitia uzungumzinafsia wa Natala. Natala anawaza kwa kuonyesha jinsi alivyonyang'anywa mume na kifo. Uzungumzinafsia wa Natala unajitokeza baada ya kujulishwa kifo cha mumewe na chifu katika onyesho la kwanza na pia baada ya mazishi katika onyesho la tatu.

Anajizungumzia kwa kusema;

*Dhiki gani hii?Kwa nini ninyanganywe mume?Msiba*

*juu ya msiba!... (uk 9) Kipenzi mume wangu, kipenzi*

*cha moyo wangu! Ningekuwa na uwezo, hungelala*

*humo kaburini. Ningekuamsha na kukuinua. Ndio,*

*mume wangu, ningekushika mkono na kukuinua,*

*na kufukuzia mbali ujane wangu na uyatima*

*wa watoto wangu. Laitiningekuwa nayatamka*

*maneno mengine, badala ya haya mawili:*

*ujane na uyatima. Haya ni maneno mazito;*

*maneno yanayoleta machozi moyoni na*

*ukungu machoni. Maskini watoto wangu*

*na mjane mamao! Msiba ulioje? Huzuni na*

*ukiwa, kumbukumbu na uhalisi mchungu.*

*(uk 34).*

Uzungumzinafsiya wa Natala unaeleza hisia zake za ndani za jinsi ujane ulivyomwingia baada ya kufiwa na mume na jinsi hapendezwi na hali ya ujane kwani anaeleza ya kwamba, kama angekuwa na uwezo angemwinua mumewe kaburini amfukuzie ujane wake. Maneno ya Natala pia yanadhihirisha udunishwaji wa mwanamke. Ujane ni hali chungu kwa binadamu si kwa Natala pekee bali kwa wanawake kwa jumla katika jamii.

#### **4.2.0 Mandhari na Ujenzi wa Maudhui**

##### **4.2.1 Utangulizi**

Sehemu hii inaangazia jinsi mwandishi Kithaka Mberia ametumia mandhari tofautitofauti katika kujenga na kuendeleza maudhui katika *Natala*.

#### **4.2.2 Dhana ya Mandhari**

Mandhari ni mazingira ya utendaji au usimulizi. Matendo yanayofanyika katika kazi ya fasihi hufanyika mahali fulani na wakati maalum. Hivyo basi, mandhari ni ile elementi katika kazi ya fasihi inayomwezesha msomaji kujua ni wapi na lini matukio yanayowasilishwa yalitendeka.

Gills (1985) anasema kuwa mandhari ni dhana pana na jumuishi. Anaungwa mkono na Wamitila (2008) anayejumuisha dhana za mazingira, mwanda na wakati ndani ya mandhari. Kwao, mandhari si mazingira ya kijiografia tu bali hurejelea masuala mengine kama vile kipindi cha matukio au mwanda wa matukio kama inavyodhihirishwa na matendo ya wahusika.

Njogu na Chimera (1999) wanafasili mandhari kama mahali maalum yaliyojengwa na mtunzi na ambapo wahusika hukaa na kuingiliana na hivyo kuzua matukio ya kiutendaji.

Mbatiah (2001:42) anasema kuwa mandhari ni istilahi inayohusishwa hasa na utanzu wa drama. Anaelezea kuwa mandhari yanarejelea sura mahsusi inayotokana na mapambo na vifaa vilivyopangwa kwenye jukwaa. Sura hiyo huwa imedhamiriwa kuiga mazingira halisi yanayoelezwa katika tamthilia inayoigizwa. Mazingira kama hayo yanaweza kuwa ya nyumbani, njiani au kwenye uwanja wa vita.

Wamitila (2004) anaunga mkono maelezo ya Mbatiah kwa kusema mandhari yanaweza kurejelea mazingira ya jukwaani na hata wakati mwenyewe. Anataja vipengele muhimu vya mandhari katika uchambuzi wa tamthilia kuwa; sifa za jukwaa, eneo la uigizaji na uangazaji wa jukwaa.



Maelezo ya wataalamu hawa ni muhimu katika kuelewa suala la mandhari katika utanzu wa tamthilia. Mambo muhimu yanayojitokeza ni kwamba, mandhari ni eneo la utendaji linaloumbwa na mwandishi na utendaji huu huhusisha wahusika ambao wanaweza kutumia mapambo na vifaa jukwaani ili kukamilisha utendaji wao. Aidha, matendo ya wahusika yanahusishwa na wakati maalum ambapo yalitendeka.

#### **4.2.3 Mandhari Katika *Natala***

Mandhari huwa ni kipengele muhimu katika uchanganuzi wa maudhui. Sababu ya kimsingi ni kwamba, matukio katika kazi ya kifasihi na maudhui yanayohusishwa na matukio hayo hutendeka mahali, wakati na katika mwanda fulani. Nafasi ya mandhari katika kazi ya fasihi hutegemea nafasi yake katika uendelezaji wa maudhui. Kwa mfano, ikiwa tamthilia inawasilisha masuala ya kijamii, sharti mandhari yawe mandhari bayana ya kijamii ili kutia uzito uthabiti wa kimaudhui. Mandhari ya nyumbani kwa Tango Mwina katika *Natala* yanaakisi maisha ya kijamii na hivyo, kuwa kielelezo cha kuendeleza maudhui ya kijamii. Mandhari katika tamthilia hufungamanishwa na wahusika, matumizi yao ya lugha, matendo yao, usawiri wao wa mwandishi pamoja na hulka zao katika kukuza na kuendeleza maudhui kwani matukio ni zao la wahusika.

Azimio letu ni kuangazia jinsi Kithaka wa Mberia alivyotumia mandhari au vifaa mbalimbali kwenye jukwaa hadi vikafikia kuwa viwakilishi vya ulimwengu wa wahusika wake. Wazo hili linamaanisha kwamba, tumelizamia suala la jinsi mandhari yanavyofanikiwa kutangamana na miongoni mwa mengineyo, wahusika na kuweza kutuwezesha kuiona mandhari akilini mwetu. Mandhari yanayojitokeza katika *Natala* ni ya kiyakinifu kwani mazingira yanayorejelewa ni

mazingira yanayoakisi mazingira ya kawaida katika jamii tunamoishi ambayo ni mandhari ya kijiografia na ya kijamii.

#### **4.2.3.1 Sebuleni mwa Natala Tango na Tango Mwina**

Onyesho la kwanza ni sebuleni nyumbani mwa Natala Tango na Tango Mwina ambako kuna vyumba vinne; chumba cha watoto, chumba cha kulala cha wazazi, sebule na jikoni. Katikati ya sebuleni mna viti na meza na kabati lililoegemezwa pembeni, mandhari yanayoakisi maisha halisi ya nyumba za kisasa. Wakati unaodhihirika ni asubuhi kama saa tano hivi ambapo Natala anashughulika na kunga za nyumbani huku akipiga nguo za watoto pasi akiwa mchangamfu. Katika hali hiyo, Gane anaingia ghafla akiwa na lengo la kuwaalika watoto wa Natala katika sherehe ya watoto na pia kupitisha ujumbe wa chifu kuwa angempitia baadaye siku hiyo.

Onyesho la pili aidha limefanyika katika mazingira ya sebuleni mwa Natala lakini wakati huu, Natala hayuko kwani ameenda kushughulikia mwili wa mumewe Tango baada ya kupashwa ujumbe kuhusu kifo cha Tango na chifu.

Sebuleni nyumbani mwa Natala Tango na Tango Mwina ni mandhari yalipotendeka onyesho la nne na la tano. Onyesho la nne linaakisi wakati baada ya ‘kifo cha Tango’ nyakati za alasiri ambapo Natala anajishughulisha na kupikia watoto wake. Anapoendelea na kupara karoti, Mama Lime anaingia akilenga kumshawishi Natala kuitikia mwito wa wazee wa ukoo wake wa kurithiwa na Wakene. Onyesho la tano linaakisi mazingira ya wakati wa asubuhi huku watoto wa Natala, Alika na Bwanu wanacheza mpira kwa furaha. Punde tu, mgoto wa mlango unasikika

ambao ni wa Tila ambaye anakuja kumgombanisha Natala kwa kusema kuwa ameshagundua njama yake na Mama Lime kutaka kurithiwa na mumewe Tila.

Mandhari ya sebuleni mwa Natala yanaendeleza maudhui yafuatayo;

### **Uonevu wa mwanamke**

Mandhari ya sebuleni mwa Natala yanaakisi kubaguliwa na kuonewa kwa Natala. Gane anamfikiria kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na bwana Chifu kwa vile mumewe yuko mbali na nyumbani. Aidha Tila anakuja kuomba chumvi katika mazingira yayahaya na anapopewa chumvi kidogo, anazua ugomvi jambo ambalo linampelekea Natala kumfukuza kwake. Tila anakatalia pale kwa kumdharau Natala eti yuko kwa nyumba ya kaka ya mumewe. Uonevu unaoonyeshwa na Tila na Gane ni dhihirisho la jinsi mwanamke anavyoonewa na jamii nzima wakiwemo wanawake ambao katika hali halisi wanastahili kumuunga mkono kutetea haki ya jinsia ya kike.

### **Utetezi wa haki za mwanamke**

Natala anaonyesha ujasiri wake katika kutetea haki yake kama mwanamke na kuonyesha wazi kuwa yeye si kiumbe dhaifu kama anavyomchukulia Tila. Anamwambia Tila kwa ukakamavu aondoke kwake kwani anajichukulia kuwa ndiye mwakilishi wa mumewe wakati mumewe hayupo. Aidha anadhihirisha uwezo wake kama mwanamke anayeweza kutosheleza mahitaji ya familia yake kwani Tila na mumewe wanashindwa kuikimu familia yao kwa mahitaji madogo kama vile ya chumvi, sukari na mafuta ya taa na ndiyo sababu anaingia kuomba chumvi (uk 3) .

## **Urithi wa mwanamke**

Wakene anatawaliwa na ubabedume na utamaduni wa jamii yake kuwa, mwanamke anapofiwa anastahili arithiwe na ndugu ya mumewe. Hivyo basi anaingia sebuleni mwa Natala na kuchukua picha ya Natala na kuanza kuikagua kwa makini huku akiimba wimbo wa mapenzi kwa furaha.

*Waniua ua kipenzi waniua ua*

*Waniua ua Natala waniua ua*

*Waniua ua mrembo waniua ua*

*Waniua ua bure bilashi waniua ua*

*Waniua ua nakufa waniua ua*

*Waniua ua nalia waniua ua*

*Waniua ua mabusu waniua ua*

*Waniua ua naungua waniua ua*

*Waniua ua marashi waniua ua*

*Waniua ua nachemka waniua ua (uk 11).*

Wimbo huu unadhihirisha hisia za Wakene za ndani na matamano yake ya kumrithi Natala. Wimbo wenyewe unajitokeza kama wazo la ndani la Wakene mwenye nia ya kulidhihirisha baadaye.

#### **4.2.3.2. Jengo la ufuo**

Mandhari katika jengo la ufuo yameelezwa kupitia mchezo ndani ya mchezo baina ya Natala na Bala katika onyesho la pili.

Mchezo ndani ya mchezo ni mbinu ya uigizaji inayofanyika katika kazi ya fasihi ambapo kunafanyika mchezo mfupi ndani ya mchezo mrefu (tamthilia) kwa lengo la kuonyesha matukio yaliyofanyika awali au yatakayofanyika baadaye katika tamthilia.

Mchezo ndani ya mchezo uliofanyika katika *Natala* unahusu matukio yaliyofanyika katika jengo la ufuo wakati Bala na Natala walienda kuchukua mwili uliochukuliwa ni wa Tango kutoka jengo la ufuo. Mchezo wenyewe unatokea kama kiangaza nyuma kwa njia ya msisitizo.

Mchezo mchezoni huu unaibua maudhui yafuatayo;

#### **Urithi wa mwanamke na uasherati**

Mhudumu katika jengo la ufuo anaibua maudhui ya urithi wa mwanamke anapoeleza kuhusu alivyorithi mke wa kaka yake kupitia mchezo ndani ya mchezo. Anamweleza Natala waziwazi kwa majivuno kuwa alimrithi mke wa kaka yake.

#### **Upembezaji wa mwanamke katika ndoa**

Masuala-ibuka katika jamii kama vile ugonjwa wa ukimwi uliangaziwa katika tamthilia kupitia mchezo ndani ya mchezo. Mhudumu katika jengo la ufuo anamweleza Natala ya kwamba alimrithi mke wa kaka yake. Natala anapodadisi kifo cha kaka yake, mhudumu katika jengo la ufuo anaeleza kwamba aliuliwa na mambo madogo madogo ambayo baadaye yalikuwa makubwa kama vile kukonda, kukohoa, na vidonda vya kuchipuka hapa na pale. (uk 20). Vidokezo hivi

vinaonyesha wazi ya kwamba kaka yake alikufa kwa sababu ya ugonjwa wa ukimwi. Tukio hili ni dhihirisho la majanga yanayowapata wanawake kupitia maamuzi ya wanaume wao ambao huchukuliwa kuwa waamuzi katika familia kutokana na mfumo wa kijamii wa ki-babedume. Mkewe mtunza jengo la ufuo kwa hakika ataambukizwa ugonjwa wa ukimwi na mumewe kwani hana sauti wala uamuzi wowote katika ndoa.

Ugonjwa wa ukimwi ni suala-ibuka katika jamii ambalo wanajamii wengi hawalielewi barabara. Mhudumu katika jengo la ufuo ni kielelezo cha watu katika jamii ambao hawaelewi fika kuwa, ugonjwa wa ukimwi ni ugonjwa lakini wanauchukulia kama mazingaombwe kwani anaeleza dalili za ugonjwa wa ukimwi pasipo kujua kwa kusema kuwa ni mambo madogo yaliyogeuka kuwa makubwa.

Mwandishi ameibua ugonjwa wa ukimwi kupitia mchezo mchezoni ili kuhamasisha jamii kwa njia ya msisitizo kuhusu janga linaloikumba jamii pasipo kudhihirikiwa wazi. Anatumia mbinu hii ili kuteka makini ya mwanajamii, afahamikiwe kuwa ugonjwa wa ukimwi ni ugonjwa halisi unaoathiri watu wote katika jamii wanaume kwa wanawake na hivyo jamii isiuchukulie kama mchezo.

### **Udunishaji wa mwanamke**

Udunishaji wa mwanamke na mhudumu katika jengo la ufuo unadhihirishwa na maneno yake kwa maiti moja katika chumba cha kuhifadhia maiti. Anazungumzia maiti kwa kuiambia maiti isilale kipumbavu kama mwanamke (uk 19). Mazungumzo haya yanapitishwa kupitia mchezo ndani ya mchezo. Kwake mhudumu katika jengo la ufuo, mwanamke ni kiumbe duni kiakili akilinganishwa na mwanamume na huenda ikawa sababu ya kulala kipumbavu. Mwandishi ametumia njia hii ya kupitisha ujumbe huu kudhihirishia jamii kuwa, wazo la mtunza jengo la

ufuo kuhusu upumbavu wa mwanamke si kweli. Katika uhalisi, mwanamke ni kiumbe sawa na aliye na akili sawa na mwanamume na kwamba upumbavu ni wa mtu binafsi wala si wa kijinsia.

### **Ukombozi wa mwanamke**

Natala anatetea haki ya mwanamke kwa kumkemea mtunza jengo la ufuo anayemwita Natala 'mwanamke' na kutusi maiti kuwa imelala kipumbavu kwa kumwambia mwanamke si mjinga bali ni binadamu kamili. Kwa hivyo, mandhari haya yanampa mwanamke fursa ya kutetea haki yake. Hata kama lengo la mtunza jengo la ufuo ni kumdunisha mwanamke, ushindi wa mwanamke katika juhudi za kujikomboa kutoka kwa minyororo ya ubabedume unajitokeza. Natala anamdhahirishiamtunza jengo la ufuo kuwa hakuna tofauti biana ya mwanamke na mwanamume. Aidha mtunza jengo la ufuo anapomrukia Natala akimtakakimapezi, Natala anamkabili na kumwangusha chini tukio ambalo linadhahirisha ukakamavu na ushindi wa mwanamke.

### **4.2.3.3 Mazishini**

Mazingira ya mazishini yanapatikana katika onyesho la pili ambapo maiti ya mtu aliyedhaniwa kuwa Tango, inazikwa. Mandhari haya yanaakisi mazingira ya kijamii ambapo mazishi ni miongoni mwa desturi za jamii nyingi za Kiafrika. Mandhari haya yanachangia maudhuui ya utetezi wa haki za mwanamke.

## **Haki za mwanamke**

Mwanamke katika utamaduni wa Kiafrika, amekuwa akidhalilishwa na kunyamazishwa na hivyo kuwa kinyamale asiye na la kusema mbele ya mwanamume. Natala anakiuka hali ya unyamavu na kueleza hisia za moyo wake hata kama anajua jambo hilo linaweza kuzua ugomvi miongoni mwa wanajamii. Hivyo basi, Natala kwa kuelewa hali mbaya ya ‘mwili wa marehemu mumewe’, anaamua jeneza lisifunguliwe wakati wa mazishi. Hata kama Wakene na wenzake wanasisitiza jeneza lifunguliwe, Mzee Balu anamuunga mkono Natala kwa kusema hisia za Natala kama mke wa marehemu ziheshimiwe. Kitendo cha Natala cha kutonyamaza na kutoa wazo lake wazi mbele ya watu ni dhihirisho kuwa wanawake wajiamini kwa mambo wayatendayo kwani wana haki sawa na wenzao wanaume.

Aidha Natala anadhihirisha haki yake kwa kukataa kutoa hongo huku akimkataza Mzee Balu kutoa hongo kwa chifu ambaye anaitisha hongo ili awaruhusu kuendelea na mazishi ya ‘Tango’ katika onyesho la tatu. Anapinga utoaji hongo kwa wafanyikazi wa umma na hivyo anataka afanyiwe haki kwa kupewa kibali cha mazishi bila hongo. Kwa ukakamavu wake Natala, wanapewa kibali na chifu cha kuendeleza mazishi pasipo na utoaji hongo (uk 33).

## **4.4 Hitimisho**

Katika sura hii, tumejadili, jinsi lugha ilivyotumika katika kujenga maudhui na hivyo, kufanikisha lengo la mwandishi. Tumejadili tamathali za usemi na kunga nyingine za lugha ambazo zimeipa tamthilia hii sura yake. Aidha tumeangazia mandhari katika *Natala* na jinsi mwandishi ameoanisha mandhari na wahusika pamoja na matukio na hivyo, kuweza kujenga na kuendeleza maudhui.



## SURA YA TANO

### HITIMISHO

#### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tunashughulikia matokeo ya utafiti wetu na mikakati tuliyotumia ili kufikia madhumuni yetu. Tulikusudia kuchunguza mchango wa vipengele vya kimtindo katika ujenzi na uendelezaji wa maudhui katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Vipengele vya mtindo tulivyovishughulikia ni pamoja na wahusika, matumizi ya lugha na usawiri wa mandhari katika *Natala*.

#### 5.1 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti wetu umejikita katika uhakiki wa vipengele vya mtindo alivyotumia mwandishi na mchango wake katika ujenzi wa maudhui ya ukombozi wa mwanamke katika jamii iliyotawaliwa na mfumo wa ki-ubabedume.

*Natala* imejikita katika mfumo wa ki-ubabedume, mfumo ambao unamdhalilisha mwanamke. Inaiangazia jamii ambayo haimthamini mwanamke kama binadamu aliye na uwezo sawa na mwanamume. Mwanamke katika hali hii, anachukuliwa kama mtegemezi wa mwanamume, chombo cha mwanamume na ambaye hana uamuzi wowote katika jamii anamoishi. Mwandishi wa *Natala* anaonyesha wazi kuwa, mwanamke si dhaifu kwa sababu za kijinsia bali anavyochukuliwa kulingana na utamaduni unaotawala jamii anamoishi. Hata hivyo, *Natala* inachukua mkondo kupitia mhusika mkuu *Natala* ambaye anapinga mila na desturi za jamii yake

akiwa na lengo la kujikomboa, kujitambulisha na kupewa heshima katika jamii. Natala anapinga mila zilizopitwa na wakati kama urithi wa wajane huku akionyesha dhahiri uwezo wa mwanamke katika mfumo mzima wa jamii na hususan katika asasi ya ndoa inayokumbwa na matatizo chungu nzima.

Imebainika kuwa, wahusika katika *Natala* wamechangia pakubwa katika ujenzi na uendelezaji wa maudhui. Ufanisi wa mwandishi unatokana na wasifu wa wahusika wake, nafasi alizowapa pamoja na lugha wanayotumia. Mhusika mkuu Natala anakinzana na wakinzani wake katika kutetea haki za jinsia ya kike na anaibuka mshindi kwa sababu ya ujasiri wake. Anawapinga wanaume wanaoendeleza mfumo wa ki-ubabedume ambao ni Wakene, Mhudumu katika jengo la ufuo na chifu wanaomtaka kushirikiana naye kimapenzi. Aidha anakataa katu mila na desturi za ukoo wa mumewe za kurithiwa hata baada ya kutumiwa mshawishi. Amepingana na wanawake ambao ni viwakilishi vya urengwaji wa mwanamke kama Mama Lime na Tila huku akiwadhihirishia wazi kuwa, yeye ni binadamu kamili aliye na uwezo sawa na mwanamume kwani ana akili na nguvu kama alivyo mwanamume. Anayadhihirisha haya, anapong'ang'ania cheti cha shamba lake huku akiibuka mshindi kwa kumnyang'anya Wakene cheti (uk 57). Natala ameibuka kuwa kielelezo cha utetezi wa haki za mwanamke.

Imedhihirika kwamba, lugha iliyotumiwa katika *Natala* imefungamanishwa na wahusika na hususan ngazi zao za kimaisha, mazingira yao pamoja na elimu yao na mwonoulimwengu wao. Kwa kuifungamanisha lugha na wahusika, mwandishi ameweza kuyamudu mazungumzo ya wahusika na hivyo kufanikiwa katika ukuzaji wa maudhui. Sababu ni kwamba, tamthilia husika imepata kani kubwa ya ushabihikweli. Hali hii inatokana na jinsi Kithaka wa Mberia anatofautisha kati ya lugha ya watu wazima (Natala) ambayo inadhihirisha mawazo komavu; na

lugha ya watoto ambayo ni nyepesi inayojitokeza kupitia kujirudia kwao, ufupi wa sentensi na maswali wanayouliza. Lugha hiyo inashabihiana na hali halisi ya lugha ya watoto (uk 24).

Mhusika mkuu Natala amepewa lugha hisishi na husishi inayomwezesha kuupinga udhalilishwaji wa mwanamke na kuweza kutetea haki za mwanamke. Ametumia tamathali za usemi pamoja na kunga nyingine za lugha zinazoambatana na utamaduni wa jamii yake. Kwa upande mwingine, wakinzani wa Natala wanaoongozwa na mfumo wa ki-ubabedume wametawaliwa na lugha ya matusi na mabezo kama inavyodhihirishwa na maneno ya mhudumu wa ufuoni kwa maiti (uk 19) na kwa Natala kwa kumwita ‘mwanamke’ (uk 17) huku naye Wakene akimtusi Natala kwa kumwita ‘punda’ wanapokuwa waking’ang’ania cheti cha shamba (uk 56).

Mandhari katika *Natala* yameoanishwa na vitushi kujenga na kuendeleza maudhui. Mandhari yaliyosawiriwa ni pamoja na sebuleni nyumbani mwa Natala, mazingira ya mazishini na mazingira ya ufuoni. Mandhari ya sebuleni mwa Natala kwa kuoanishwa na vitushi katika mazingira hayo, yanaakisi matatizo anayoyapata mwanamke iwapo mumewe hayupo karibu kama inavyomfanyikia Natala. Natala anabezwa na kudharauliwa na Tila huku Gane akimdhania ana uhusiano wa kimapenzi na Chifu; naye Wakene akitaka kumrithi kama kifaa.

Mazingira ya mazishini yanaakisi mazingira yakinifu kwani mazishi ni tukio la kawaida katika jamii tunamoishi. Hata hivyo, katika Natala mazingira ya mazishi yanadhihirisha ushindi wa Natala dhidi ya ufisadi unaoelekezwa kwake na chifu ambaye ni mhudumu wa umma na angali anahitaji hongo kwa kazi ambayo analipwa mshahara na serikali kuifanya. Natala anasimama kidete kupinga ufisadi wa chifu kwa kumwambia wazi kuwa, yeye ni adui mkubwa wa utoaji hongo na akamkanya Mzee Balu katu kutotoa hongo kwa chifu ili awape kibali cha kujumuika mazishini (uk 32- 33). Mazingira haya aidha yanadhihirisha ukombozi wa mwanamke kutoka

minyororo ya kunyimwa haki ya uamuzi mbele ya mwanamume. Natala anatoa uamuzi kuwa jeneza lililokuwa na ‘mwili’ wa marehemu mumewe lisifunguliwe, uamuzi ambao unaheshimiwa hata kama Wakene na Mama Lime wanajitokeza kuupinga.

Mazingira ya ufuoni yanadhihirisha mfumo wa ki-ubabedume unaoendelezwa na mhudumu katika jengo la ufuo kumkandamiza mwanamke kimawazo. Matusi anayoielekezea maiti na Natala ni kielelezo cha jinsi anavyomchukulia mwanamke kuwa kiumbe duni na dhaifu akilinganishwa na mwanamume. Aidha anamchukulia mwanamke kama chombo cha kimapenzi kwa mwanamume. Natala amejitokeza na kumdhihirishia mhudumu wa ufuoni kuwa mwanamke ni binadamu kamili na wala si mpumbavu. Anapomkaribia kwa kumtaka kimapenzi, Natala anamwangusha chini na anapoinuka anamwonya kwa vidole tu bila kutaka kumkaribia (uk 22-23). Hali hii inaonyesha ushindi na ukombozi wa mwanamke.

Imebainika kuwa maudhui makuu katika *Natala* yanahusu utetezi wa haki za mwanamke na kumbainisha katika jamii iliyotawaliwa na mfumo wa ki-ubabedume. Natala anamtetea mwanamke asidunishwe wala kudharauliwa katika misingi ya jinsia yake, apewe nafasi sawa na mwenzake mwanamume pasipo kuwekwa pembeni katika kumiliki mali na kutoa uamuzi katika jamii na pia, asidhulumwiwe kimapenzi wala kurithiwa kwani mwanamke si kifaa bali ni binadamu kama alivyo mwanamume. Hata hivyo, utamaduni uliopitwa na wakati wa urithi wa wanawake umedhihirika katika *Natala* kupitia wawakilishi wa urengwaji mwanamke ambao ni Mama Lime na Tila pamoja na wanaume waliojawa na taasubi ya kiume kama Wakene na mhudumu katika jengo la ufuo. Maudhui mengine ni kama ufisadi wa wahudumu wa umma, umasikini uliosakini miongoni mwa wanajamii kutokana na ukosefu wa ajira na hususan kwa wanawake, uozo katika jamii unaojitokeza katika vitendo vya uasherati pamoja na kuwekwa pembeni kwa mwanamke. La muhimu ni kwamba Natala amepinga mila na desturi zinazomweka mwanamke pembeni

pamoja na mfumo wa ki-ubabedume katika kumkomboa mwanamke na akaibuka mshindi katika majaribio yake ya kujikomboa.

Mwandishi Kithaka wa Mberia, amefanikiwa kuoanisha vipengele vya kimtindo vya wahusika, mandhari na matumizi ya lugha katika ujenzi na uendelezaji wa maudhui. Ufanisi wake unatokana na jinsi alivyoimudu lugha ya wahusika wake, uteuzi mwafaka wa wahusika pamoja na usawiri wa mandhari yakinifu ya mazingira halisi katika jamii. Lengo kuu la mwandishi ni kuiumba jamii yenye wanawake walio na uwezo wa kujinasua kutoka minyororo ya mfumo wa ki-ubabedume. Amekuza lengo lake kuanzia mwanzo hadi kileleni mwa tamthilia tunapomwona *Natala* akionyesha ushindi wake kwa kumnyang'anya Wakene cheti cha shamba. Hata hivyo, tamthilia inafikia kikomo kwa mpomoko mkali sana pale ambapo juhudi za mwandishi zinaporomoshwa kwa kurejea Tango pale kileleni kama mwokozi wa *Natala* na kudumisha mtazamo kuwa, mwanamke daima ataendelea kumtegemea mwanamume maishani.

## **5.2 Mapendekezo**

Tumetumia Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika katika uchunguzi wetu wa masuala ya wanawake na tunapendekeza watafiti wa baadaye watumie nadharia nyingine zinazohusu masuala ya wanawake kama vile unisai wa Kiafrika katika uchanganuzi wa *Natala*. Aidha nadharia ya uhalisia wa kijamii inaweza kutumiwa kuhakiki tamthilia ya *Natala* kwani ni tamthilia inayohusu masuala ya kijamii. Aidha tumetumia Nadharia ya Umuundo kuonyesha jinsi vipengele vya mtindo vimeoanishwa katika kuunda tamthilia ya *Natala*. Tunapendekeza watafiti wa baadaye watumie nadharia nyingine kama vile urasimu kutafiti muundo wa kazi husika.

Kuna haja ya wahakiki wa baadaye kushughulikia vipengele vya kimtindo ambavyo hatujavishughulikia kama msuko na usimulizi aliotumia mwandishi katika ujenzi na uendelezaji wa maudhui katika tamthilia ya *Natala*. Sisi tumeshughulikia wahusika, matumizi ya lugha na usawiri wa mandhari.

### **5.3 Hitimisho**

Madhumuni yetu yalikuwa kuchunguza jinsi mtindo wa mwandishi umechangia katika ujenzi wa maudhui katika *Natala*. Lengo lingine katika utafiti wetu lilikuwa tuonyeshe vipengele vya mtindo vilivyotumika katika ujenzi wa *Natala*. Ni dhahiri kuwa, vipengele vya mtindo alivyovitumia Kithaka wa Mberia vimechangia pakubwa katika ujenzi na uendelezaji wa maudhui katika tamthilia ya *Natala*. Tumethibitisha kwamba, vipengele vya kimtindo vya wahusika, mandhari na matumizi ya lugha vimetumika katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi.

## MAREJELEO

Aristotle (1965): *Poetics* katika S.T.D. Aristotle / Horace / Longinus. Harmonds Worth: Penguin.

Bennet, T; (1979): *Formalism and Marxism*. London: Methuen and Co. Ltd.

Bertoncini, E. Z; (1989): *Outline of Swahili Literature*. Leiden / Boston: Brill.

Bertoncini, E. Z. na wengine; (2009): *Outline of Swahili Literature - toleo la pili*. Leiden / Boston: Brill.

Carter, R. A; Simpson, P; (1989): *Language, Discourse and Literature*. London: Routledge.

Culler, J. D; (1975): *Structuralist Poetics*. London: Routledge and Kegan.

De Beauvoir S; (1972). *The Second Sex*. London: Pan Books Publishers.

Eagleton, M; (1991): *Feminist Literary Criticism*. New York: Longman Inc.

Eagleton, T; (1992): *Marxism and Literary Criticism*. London: Routledge.

Ellman, M; (1968): *Thinking About Women*. New York: Harcourt.

Forster, E. M; (1949): *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.

Freidan, B; (1963): *The feminine Mystique*. New York: Dell.

Gill, R; (2006): *Mastering English Literature. Toleo la Tatu*. Houndmillls: Palgrave Macmillan.

Greer, G; (1963): *The Female Eunuch*. London: Grafton Books.

Holman, (1936): *A Handbook to Literature*. New York: Odyssey.

Kiango, D; (1992): “Taswira ya Mwanamke Katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya zilizochapishwa- katika Baragumu juzuu 1 na 2”. Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu cha Maseno.(Haijachapishwa).

Kitsao, J; (1982): “An Investigation of Themes in Swahili Literature and an Application of Stylististics to Chosen Texts”. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Krugger (1996): *Female Characters in Contemporary Kenya’s Women Writers. Figures Subdued Voices* .Madison: University Of Nairobi.

Kuhenga, C; (1977): *Tamathali za Usemi: Mtaala wa Kiswahili*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Lugano, R, (1989): “Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi”. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).



Magare, F. A; (2002): “Uhakiki wa Tamthilia ya 'Amezidi' Kama kazi ya Kiubwege”. Tasnifu ya M A: Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mbatiah, M; (2001): *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Millett, K; (1970): *Sexual Politics*. London: Virago.

Momanyi, C; (2001): “Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Fasihi ya Kiswahili Baada ya 2000: Kuyumbisha Uhalisi”: katika Makala ya Kongamano la Kimataifa; *Kiswahili 2000 Proceedings*, J.S. Mdee na H.J.M. Mwansoko (wahariri). Dar es Salaam: TUKI.

\_\_\_\_\_ (2002): “Swala la Uana Katika Fasihi ya Kiswahili” Katika toleo la Inyani Simala- *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Mosoti, Z. M; ( 1993): “Maudhui katika Tamthilia Nne za Emmanuel Mbogo”. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Msokile, M; (1993): *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugambi, P. J. M; (1982): “Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya Zilizochapishwa”.Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Musyoka, F. M; (1996): “Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za Jay Kitsao”.Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mwangi, D. K; (2005): “Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za K.W. Wamitila.” Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Nnaemeka, O; (2005): *Bringing African Women into Classroom: Rethinking Pedagogy and Epistemology in African Gender Studies*.[http:// Mojubaolu.blogspot.com](http://Mojubaolu.blogspot.com).

Njogu, K. na Chimerah, R; (1999): *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Nyamberi, H; (1997): “Mwamko wa Wanawake katika Tamthilia za Penina Muhando”.Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Nyaosi, K. N; (2008): “Taswira ya Asasi ya Ndoa katika Riwaya ya Kiu na Msimu wa Vipepeo”.Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa).

Ntarangwi, M; (Ph.D) (2004): *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustina College.

Ogundipe, M; (1994): “*Recreating Ourselves: African Women and Critical Transformation.*” Trenton: African World Press Inc.

Okome, M. O; (1999): *Listening to Africa, Misunderstanding and Misinterpreting Africa: Reformist Western Evangelism on African Women*: [htt: // Mojubaolu.blogspot.com](http://Mojubaolu.blogspot.com).

Onyoni, J. K; (2012): "Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Tamthilia za Natala na Mama Ee". Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Rimmon-Kenan, S; (2002): *Narrative Fiction: Comparative Poetics*. Second Edition. London: Routledge.

Sarara, M. M; (1997): "Maudhui katika Tamthilia Za S.A.Mohammed". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Scholes, R; (1974): *Structuralism in Literature*. New Haven: Yale University Press.

Senkoro, F. E. M; (1982): *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Short, M; (1980): *Style in Fiction*. London: Longman.

Showalter, E; (1971): *Woman Liberation and Literature*. New York: Harcourt Brace.

Steady F.C; (1981): *Reflecting on the Politics of Sisterhood*: New York: African World Press.

Strobel, M; (1979): *Muslim Women in Mombasa (1890-1975)*: New Haven and London: Yale University.

Wafula, R. M; (1999): *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. na Njogu, K; (2007): *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

wa Mberia, K; (1997): *Natala*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Wamitila, K.W; (2002): *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

—————(2003): *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

—————(2008): *Kanzi ya Fasihi: Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide - Muwa Publishers.

Wellek, R. Warren, A; (1949): *Theory of Literature*. New York: Penguin.

Were, E; (2012): “Fani Katika Tamthilia ya Kiswahili: Uchanganuzi wa Kilio cha Haki na Kijiba cha Moyo.” Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Woolf, V; (1929): *A Room of One's own*. London: The Hogarth Press.

Wollstonecraft, M; (1792): *A Vindication of the Right of Women*. Boston: Peter Edes.